ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Saba – Tarehe 31 Machi, 2011

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani, muhtasari wa hotuba juu ya ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani, ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naomba kuwasilisha.

Naomba kuwasilisha hati Mezani.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Ahsante, Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha ripoti ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 60

Udhibiti wa Tatizo la Madawa ya Kulevya

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Pamoja na jitihada mbali mbali za serikali za kupambana na uingizaji na utumiaji wa madwa ya kulevya ikiwa ni pamoja na kuimarisha ulinzi katika viwanja vya ndege na bandari zetu, bado uingizaji na utumiaji wa madawa hayo umeendelea kushamiri katika visiwa vya Zanzibar.

(a) Je, ni kwa nini imeshindikana kuzuia na kukomesha uingizaji na utumiaji wa madawa hayo.

(b) Serikali ina mikakati gani madhubuti na inayotekelezeka kwa haraka katika kutokomeza kabisa biashara ya madawa ya kulevya ili kuwanusuru vijana wa Kizanzibari katika janga hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, pamoja na jitihada mbali mbali za serikali za Kupambana na uingizaji na Utumiaji wa madawa ya kulevya ikiwa ni pamoja na kuimarisha ulinzi katika viwanja vya ndege na Bandari zetu, bado utumiaji wa madawa hayo umeendelea kushamiri katika visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba duniani kote harakati mbali mbali za usafirishaji na uingizaji wa madawa ya kulevya hufanywa katika njia na mazingira ya usiri mkubwa. Wahusika hutumia kila mbinu ili kuhakikisha kwamba wanazotoresha harakati za mapambano dhidi yao. Hivyo kudumisha na kuendeleza biashara haramu na usafirishaji wa madawa ya kulevya kwa nguvu zote. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia nayo imejikuta ikiwa na changamoto nyingi katika harakati za udhibiti wa uingizaji wa madawa ya kulevya nchini.

Mhe. Naibu Spika, sababu kubwa iliyopelekea kutopata mafanikio makubwa katika harakati za kuzuwia na kukomesha uingizaji wa madawa nchini tunaamini ni kukosekana kwa muundo madhubuti wa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya nchini kwani muundo huo umezingatia zaidi kurekebisha tabia na kutoa taaluma kwa waathirika wa madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa mapambano dhidi ya madawa ya kulevya yanahusisha taasisi mbali mbali, imebainika kutokuwepo kwa ushirikiano wa dhati na nguvu za pamoja baina ya taasisi zetu husika yaani Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevya ambayo ipo chini Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ambayo ndio yenye jukumu la kuratib mapambano dhidi ya dawa za kulevya, vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mahakama pamoja na raia wema

wote. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeanza kujipanga kulitekeleza hili nguvu zetu zote.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kama nilivyooeleza hapo awali kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeanza kujipanga vyema ili kukabiliana na tatizo hili. Tumeanza kukutana na wadau mbali mbali kukusanya maoni yao, tumepitia katika maeneo ambapo vijana wetu wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya wamekuwa wakiendelea kupata nafuu na wao wametupa maoni yao. Tumeangalia upungufu uliomo katika Sheria yetu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Sheria Nam. 9 ya mwaka 2009. Mchakato wa kuifanyia marekebisho umeanza na itafikishwa katika Baraza lako tukufu katika Kikao cha Septemba mwaka 2011.

Sasa hivi mkakati wa udhibiti unaendelea kuandaliwa lakini wakati huo mapambano ya udhibiti tumeanza kuyachukua.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar inatajika kwamba ni nchi ambayo ina *Airport* ya Kimataifa pamoja na kuwa tuna na bandari ambayo ina ulinzi wa vyombo vyote husika. Lakini madawa haya ya kulevya yanapoingizwa katika nchi yetu yanapita katika maeneo haya makuu kwa ajili ya kuja kuwaathiri wananchi ambao tunao katika maeneo yetu.

Je, katika kipindi cha mwaka wa Fedha, unaokwisha Juni mwaka huu. Ni viongozi wa taasisi za polisi na maeneo mengine ambayo yanahusika na udhibiti wa madawa ya kulevya. Ni viongozi wangapi ambao wamechukuliwa hatua baada ya kubainika kwamba haya madawa yamepita yakaweza kukamatwa katika maeneo yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama nilivyoeleza katika jibu langu mama, kwamba njia ambazo zinatumiwa na wahalifu wa madawa ya kulevya ni kupitia Bandari na Viwanja vya Ndege ambavyo ndio njia ya kuingilia katika Visiwa vyetu.

Kwa hivi sasa Mheshimiwa takwimu ambayo anaitaka naomba nimletee kwa maandishi, kwa sababu inabidi niwasiliane na vyombo husika ambavyo ndivyo hisa vinavyoshughulikia, ukamataji na uendeshaji wa kesi hizi ili niweze kumpatia jibu lake sahihi.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri hivi karibuni wizara yako kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi limekuwa likiwakamata washukiwa wa matumizi ya madawa ya kulevya na kuwapima mkojo. Endapo anathibitika kwamba wao ni watumizi kweli wa madawa ya kulevya wanapelekwa mahakamani kwa ajili ya kushtakiwa na kupewa adhabu. Badala yake wanapelekwa sehemu ya uhifadhi kwa ajili ya kufanyiwa hatua ya kuacha madawa hayo ya kulevya.

Je, Mhe. Waziri kwa sasa kwa kuwa sheria hiyo mpya bado haijapitishwa, kuna sheria ambayo inaturuhusu sisi kuwakamata hao na kuwachunguza na badala yake kuwashtaki na ikithibitika kuwapa adhabu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kinachofanyika katika kuwakamata vijana wetu ambao wamejihusisha na utumizi wa dawa za kulevya baadaye kuwapima mkojo, ikithibitika kuwapeleka mahakamani na kuweza kuwaweka jela kwa kipindi cha miezi sita na baadaye kuwapeleka katika vituo vya kuwarekebisha tabia. Hilo linafanyika chini ya sheria ya udhibiti wa madawa ya kulevya ambayo tunayo. Halipo kinyume cha sheria, sheria ipo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na uingizaji wa madawa ya kulevya katika nchi yetu, lakini yapo madawa ya kulevya ambayo yanatengenezwa kienyeji katika nchi yetu.

Je, Mhe. Waziri katika masuala haya ya madawa ya kulevya kwa mfano kama pombe ambazo ni kali zinazotengenezwa kienyeji na hili wana mpango gani wa kulishughulikia.

Je, kuna aina gani ya pombe za kienyeji ambazo zimeruhusiwa na serikali yetu kutumika katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Subeit afahamu kwamba Ofisi wa Makamo wa Kwanza wa Rais inashughulikia madawa ya kulevya yale yaliyoainishwa katika Sheria ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya yaani *alicity drags*. Hata hivyo pombe ambavyo ni haramu anazozizungumzia ni kinyume cha sheria na zina sheria yake ya udhibiti na serikali inazidhibiti ipasavyo.

Nam. 103

Fedha kwa Ajili ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya hualikwa na wananchi katika hafla mbali mbali za kijamii ambapo huombwa kusaidia kuchangia hafla hizo.

Na kwa kuwa Wakuu hao hushindwa kuchangia kutokana na kukosa kifungu cha fedha katika Afisi zao kwa ajili hiyo.

Je, serikali haioni kuwa ipo haja ya Afisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwa na kifungu hicho cha fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 103 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wamekuwa na utamaduni wa kuwaalika Viongozi wao wa Kitaifa wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika shughuli zao mbali mbali za kijamii. Hata hivyo, wakati wa shughuli za wananchi zikiendelea, viongozi hao huombwa kuchangia shughuli hizo za kimaendeleo. Kutokana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutokuwa na fungu la kuchangia, viongozi hao hushindwa kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa serikali inalifahamu suala hili na inalifanyia kazi kwa lengo la kuwasaidia viongozi Wakuu na hasa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili waweze kushirikiana kikamilifu na wananchi wao.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambayo tayari amekwisha kuyatoa. Kwa ufahamu tulionao Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa ni wasaidizi wa karibu sana kwa maeneo husika wa Rais wa Nchi yetu.

Rais kwa mujibu wa taratibu ana mfuko wake ambao unamsaidia katika kuendeleza shughuli zake. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba iko haja ya kutumia mfuko ule wa Rais katika kuwasaidia Wakuu hawa wa Mikoa katika kutekeleza kazi ambazo Raisi zinamuhusu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni Wasaidizi wa Mhe. Rais katika maeneo yao. Lakini katika suala la kutumia mfuko wa Rais, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba huo mfuko wenyewe wa Rais sio mkubwa sana kiasi ambacho cha kuruhusu viongozi wengine waweze kuutumia.

Nataka nimwambie kwamba tumwachie Mhe. Rais atumie mfuko wake na sisi Wizara ya Fedha tunaandaa utaratibu na viongozi wetu hawa ili wawe na kasma ya kutumia kwa ajili ya shughuli hizo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa waziri amesema serikali imeliona tatizo hili. Sasa hivi lipo katika mchakato wa kulifanyia kazi. Lakini masuala kama haya yana kawaida ya kuchukua muda mrefu katika utekelezaji wake.

Je, Mhe. Waziri ni lini suala hili litafanyiwa kazi. Katika Bajeti hiyo inayokuja anatuahidi fungu hilo litakuwapo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakilishi amenitega kidogo. Suala hili litafanya kazi haraka iwezekanavyo. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba lengo letu lianze kazi katika Bajeti ijayo.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nianze kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa jibu lake la mwisho kuwa tamaa karibu ipo ya mambo haya kufanikiwa. Katika uzoefu wangu nilipokuwa nikitembelea pamoja na Kamati yangu. Tuligundua kuwa misaada mingi inatolewa kwa maslahi ya wananchi, lakini kwa sababu inapitia katika ngazi za Mkuu wa Wilaya. Mtekelezaji Mkuu huwa ni Masheha. Tumebaini kuwa baadhi ya miradi badala ya kuwasaidia wananchi kiuchumi inatumika kisiasa. Mara nyingi huwa ineleta migogoro.

Je, Mhe. Waziri ameiwekea Miswada hii mipango mahususi kuona kuwa itatumika kwa lengo lililokusudiwa kwa wananchi wote kwa sababu hii ni serikali ya wananchi wote.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba lengo

la serikali ni kuwasaidia wananchi wake katika maeneo mbali mbali. Katika msaada wowote ambao serikali inautoa isingependa msaada huo utumike kisiasa. Msaada huo tungependa utumike kijamii zaidi na kuwasaidia wananchi zaidi kuliko kisiasa.

Lakini hata hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Makilishi kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye ndiye anayesimamia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, tutahakikisha kwamba kifungu hiki kitakapoanzishwa kitatumika kwa lengo la kuwasaidia wananchi na sio vyenginevyo.

Nam. 132

Kufufua na Kuanzishwa Viwanda Vipya

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Ili nchi iendelee inahitaji mambo mengi kufikia hatua ya maendeleo moja kati ya mambo hayo ni nchi kuwa na viwanda.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kuhusu suala la kufufua viwanda vyetu na kuanzisha viwanda vyengine.

(b) Je, serikali ina mpango gan wa kuwasaidia wananchi kuanzisha viwanda hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 132 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa sekta imara ya viwanda ni muhimili madhubuti wa Maendeleo ya nchi. Kwa bahati mbaya mchango wa sekta hii katika pato la Taifa la Zanzibar kwa mwaka 2009 lilikuwa ni asilimia nne nukta moja (4.1%) tu, ambao ni mchango mdogo sana. Kwa hivyo ipo haja ya kuongeza shughuli za viwanda nchini.

Mhe. Naibu Spika, serikali iliamua kushajiisha sekta binafsi kuendesha miradi ya biashara na ya uzalishaji kwa kufungua milango ya uchumi kwa kupitia Sheria ya Uekezaji ya mwaka 1986. Kufuatia uamuzi huo, ndipo serikali kidogo kidogo ilijiondoa kutoka kwenye shughuli za uzalishaji wa moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, baada maelezo hayo naomba sasa nimjibu Mhe. Mtando swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali itaendelea na kazi za kuwatafuta na kuwashajiisha Wawekezaji binafsi kuvifufua baadhi ya viwanda vilivyokuwa vya serikali ambavyo haviko katika hali mbaya sana, sambamba na kuanzisha viwanda vyengine vipya kufuatana na mahitaji yetu lakini pia na upatikanaji wa soko kwa bidhaa zitakazozalishwa.

(b) Kwa kuwa SMZ kupitia Wizara yake ya Biashara, Viwanda na Masoko na kwa kushirikiana na taasisi husika kama ZIPA inawajibika kuandaa mazingira bora kwa wawekezaji kwa kuzirekebisha na kuziimarisha sera, sheria na vivutio vinavyotolewa kwa sekta ya viwanda, ili kuifanya sekta ya viwanda ivutie zaidi kwa wawekezaji na wananchi wenye azma ya kuekeza katika sekta hiyo.

Mhe. Mbarouk Ali Mussa (Mtando): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize swali la Nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu yake mazuri amesema kwamba serikali ina mpango wa kufufua baadhi ya viwanda ambavyo kwa hivi sasa vimekufa.

Ningependa kujua viwanda hivyo ni vipi ambavyo vinataka kufufuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, tokea serikali hii ianze sasa ni miezi mine tu. Kwa hiyo tupo kwenye kujipanga kuvipitia na kuviangalia viwanda ambavyo havipo katika hali mbaya sana.

Hatuna budi sote kufahamu Mhe. Naibu Spika, kwamba viwanda vingi vimeshapitwa na wakati katika uwekezaji wake. Kwa hivyo zana zinazotumika katika viwanda vile si rahisi kufanya kazi katika karne hii ya sasa. Serikali inajipanga kuangalia vile ambavyo vinaweza kufufulika basi tunavifanyia bidii kuvitafutia wawekezaji ili tuweze kufanya kazi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Tunacho kiwanda cha Sukari sehemu ya Mahonda, kiwanda hiki amepewa mwekezaji. Lakini mpaka muda huu hatuoni hatua zozote za maendeleo za uzalishaji.

Ni lini kiwanda hiki kitazalisha sukari ili tufaidike na wananchi wetu waweze kupata ajira.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwamba suala hilo nitalijibu mara baada ya suala hili.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa alitaja katika majibu yake ya msingi kwamba watashirikiana na ZIPA katika kuhakikisha kwamba sera inapatikana na inatekelezwa. Kwa kuwa ZIPA ndio kitengo kikuu kinachoshuhulikia wawekezaji.

(a) Kwa kuwa muwekezaji Mkubwa ambao ungesaidia uchumi wa nchi ni viwanda na sio hoteli peke yake. Je, wizara inachukua mkazo gani kuishindikiza ZIPA ili karibishe wawekezaji wa viwanda zaidi na sio hoteli peke yake.

(b) Kwa kuwa viwanda vinahitaji nyenzo nyingi na rasilimali kubwa. Ni jitihada gani inayochukua wizara, kuwashajihisha wawekezaji wa ndani ili waweze kuwekeza katika viwanda.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, katika jibu langu, kama alivyofikiri yeye na swali la msingi nimesema kwamba serikali inajipanga kuvipitia viwanda na kuviangalia vizuri. Katika kufanya hivyo Mhe. Naibu Spika, ni pamoja na kukaa na *ZIPA*. Wakati wa kukaa na *ZIPA* madhali ni serikali hii tunafanya jambo kwa pamoja, ili kuhakikisha kwamba serikali inafufua viwanda na kuanzisha vyengine kufuatana na mahitaji na soko katika ulimwengu. Maana yake bidhaa zitakazozalishwa Mhe. Naibu Spika, zitakuwa hazina wajibu zikubalike katika soko.

Mhe. Naibu Spika, kazi kubwa ya serikali kupitia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko ni kuandaa mazingira. Mhe. Naibu Spika, nilishasema katika jibu la swali la msingi kwamba tuko katika kuandaa mazingira ikiwemo kupitia sheria, kupitia sera pamoja na kuandaa vivutio mbali mbali, na hili tunalifanyia kazi.

Nam. 109

Muwekezaji wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza**:-**

Muda mrefu umepita tangu Kiwanda cha Sukari cha Mahonda apewe Mwekezaji hakuna sukari inayozalishwa na kiwanda hicho. Badala yake Mwekezaji huyo amekuwa na migogoro kila siku na wananchi wa Mahonda.

(a) Mhe. Waziri, unafahamu kwa nini Mwekezaji huyo hazalishi sukari.

(b) Nini chanzo cha migogoro kati ya Mwekezaji na wananchi wa mahonda.

(c) Kwa kua Muwekezaji huyo anaonekana kuwa mbabaishaji; Je, wizara haioni sababu ya kupitia upya mkataba wake na Muwekezaji huyo na ikiwezekana kuuvunja.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 109 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inafahamu kwamba Kiwanda cha Sukari Mahonda hakizalishi sukari, na ni kwa sababu zifuatazo:-

Kutokana na uchakavu wa kiwanda kumekua na kasoro katika mtambo wa kuzalisha mvuke (*boiler*) ambapo unatoa kiwango kidogo cha joto ambacho hakifikii kiwango kinachotakiwa ili kukausha sukari ipasavyo. Kiwanda kiliwahi kuzalisha kiasi cha tani 100 za sukari katika mwaka wa 2008, lakini sukari hiyo haikuwa na ubora unaostahiki kutokana na kasoro za huo mtambo wa mvuke (*boiler*), ambao ni wa zamani na unaotumia kuni nyingi na mafuta ya dizeli nzito ambayo ni ghali. Hivi sasa mwekezaji kwa msaada wa wataalamu wa *UNDP* anaendelea na juhudi za kutafuta mtambo muafaka wa ajili ya uzalishaji wa sukari huku akiendelea na uzalishaji wa spiriti pekee.

(b) Mhe. Naibu Spika, migogoro kati ya Mwekezaji au uongozi wa mradi na wananchi wa Mahonda pamoja na vijiji vyengine vinavyopakana na mashamba ya miwa inatokana zaidi na masuala ya matumizi ya

ardhi ya mashamba hayo ambayo ingawa mradi umekabidhiwa rasmi kwa ajili ya upandaji miwa, baadhi ya wananchi hao huyatumia mashamba hayo kwa kulima bila ya ridhaa ya uongozi wa wenye mradi. Baadhi ya wakati zinajitokeza dalili za wazi za hujuma za uchomaji moto wa miwa, au uchungaji wa mifugo katika mashamba, jambo ambalo linasababisha hasara kwa kiwanda na kuendeleza migongano zaidi na ni wananchi ndio wanaoshutumiwa kuhusika na hujuma hizo nzito.

(c) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kufuatilia kwa kina masuala ya Kiwanda cha Sukari Mahonda chini ya Mwekezaji aliyepo sasa kweli inaonekana kuna matatizo mengi, lakini hakuna dalili yoyote inayoashiria kuwa Mwekezaji huyo ni mbabaishaji. Matatizo anayokumbana nayo ni ya kweli na ya kimsingi ambayo yangeweza kuathiri mradi mwengine wowote wa aina hiyo.

Mhe. Naibu Spika, seriakli inaamini kuwa kuendeleza mradi wa kuzalisha sukari Mahonda ni jambo la faida kwa taifa, kwa Mwekezaji mwenyewe na kwa wananchi wa Zanzibar, na zaidi wale ambao wanapata ajira katika mradi huo. Jambo la msingi kwa sasa ni kuendelea na juhudi za kuziondoa kasoro zinazojitokeza na kutoa msaada unaohitajika kwa wenye mradi ili mradi uweze kuzalisha sukari kama inavyotarajiwa.

Katika kufikia hali hiyo, mashirikiano ya viongozi na wananchi wanaopakana na maeneo ambayo mradi huu upo ni muhimu sana, na kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nawaomba viongozi wa ngazi zote wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge na Viongozi wa Serikali za Mkoa na Wilaya za Kaskazini, washirki kikamilifu kuwaelimisha na kuwashajiisha wananchi kuunga mkono juhudi zitakazopelekea kiwanda kufanikiwa kwa faida yetu sote.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka kujua kasoro hizo za mtambo wa mvuke tangu zimejitokeza ni kipindi cha miaka mingapi na ni muda gani ambao unatarajiwa unaweza ukafanyiwa marekebisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba katika jibu langu mtambo huu ni wa siku nyingi, Kiwanda cha Sukari sote tunajua kimejengwa siku nyingi tokea wengine tulikuwa skuli tunasoma miaka hiyo. Kwa hivyo, teknolojia iliyotumika wakati huo Mhe.

Naibu Spika, mitambo yake ni dhahiri kwamba katika teknolojia ya sasa si rahisi kuleta ufanisi na ndio maana tukasema *boiler* hili huyu Mwekezaji anafanya utaratibu kwa msaada wa *UNDP* ili aweze kubadilisha vifaa vya aina hiyo ndani ya kiwanda hicho ili kiweze kuzalisha kama tunavyotegemea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba mkataba ambao waliofungiana kati ya serikali na Mwekezaji ulikuwa una muda gani wa kuanza kutengeneza hiyo sukari.

b) Kwa nini katika mkataba huo umeeleza sehemu ya sukari au atengeneze spiriti, na kama ikiwa ni sukari je akitengeneza spiriti wizara yako ina hatua gani ya kumchukulia Mwekezaji huyo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, mkataba baina ya Mwekezaji na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulifanywa mwaka 2005 na mkataba huu ulikuwa na vipengele mbali mbali. Suala la matatizo ya Kiwanda cha Sukari wizara yetu pamoja na Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo tumeyafanyia kazi hivyo tumeunda kamati maalum ambayo imekwenda katika kiwanda kuangalia matatizo yoyote kama ilivyooneshwa katika mjadala huu unaoendelea hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili mkataba tumeusoma tumebaini viko vipengele ambavyo kwamba sisi serikali wenyewe tumevikiuka hatukuvitimiza na viko vipengele ambavyo vile vile Mwekezaji hakuvitimiza. Tathmini yote iko tayari tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote wawe na subra ili tupate kupeleka serikali tathmini yote iliyofanywa na kamati yetu iliyofanya kazi hiyo kwa muda wa miezi miwili katika kiwanda hiki, kuanzia katika mashamba, mkataba wenyewe na suala zima la uzalishaji wa sukari katika kiwanda hiki.

Mhe. Naibu Spika nawaomba wawakilishi wote wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar wajue kwamba Kiwanda hiki cha Sukari kwa Zanzibar ni kiwanda kimoja cha aina ya pekee kinachozalisha kutokana na *Agro Base Processes*. Kwa hivyo, ni kiwanda muhimu sana katika visiwa vyetu, kiwanda hiki tukikibeza au kikiwa hakifanyi kazi basi kitatoa indecation kwamba viwanda vyote vya *Agro Base Industries* kwa Zanzibar ni tatizo na Mwekezaji yeyote atakayekuja kuja kuekeza katika sekta hiyo atakuwa ana sita sita.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo ndio serikali imeandaa utaratibu huo na naomba wawakilishi wawe na subra ili serikali ipate kutoa uamuzi juu ya suala hili. Lakini lengo la serikali ni kuona kwamba kiwanda kinafanya kazi na sukari inazalishwa.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzwa habari ya suala la spiriti, spiriti ni *by product* katika kila kiwanda kunakuwa na *by products*. Kwa hivyo, spiriti ni *by products* ya sukari ingaje kumejitokeza tatizo jengine duniani sasa hivi, sasa hivi wenye viwanda vingi vya sukari hasa Brazil wanazalisha zaidi *ethanol* kuliko sukari, ndio maana katika ulimwengu sasa hivi kuna ugumu wa sukari kwa sababu viwanda vingi duniani vinazalisha zaidi *ethanol* kuliko sukari. Kwa hivyo, naomba tujue suala hili limeikumba dunia nzima sio hapa peke yake lakini katika mkataba ule hatujaona kipengele cha kuzuia Mwekezaji asizalishe by products za sukari.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na *boiler* hilo kuwa haliwezi kutoa mvuke wa kutosha na kiwanda kile kina *turbines* mbili ambazo zinatoa *two mega walts* za umeme ambazo *mega walt* moja zinatumika kwa kazi za kiwanda na moja ikaweza kutumika kwa kazi nyengine. Lakini kwa bahati mbaya *boiler* ziko tatu pale, *boiler* mbili haziwezi kuendesha hata *turbines* moja lazima boiler ya tatu ishirikiane na boiler mbili hizi. *Boiler* hiyo imeharibika mwanzo ilikuwa inaonesha kwamba inafanya kazi lakini wakati wa *production* ndio ilipoharibika na ndio maana mwekezaji akakwama na juhudi zinaendelea.

Mhe. Naibu Spika, *UNDP* wamekuja wameangalia mradi wameona kwamba vifaa ambavyo kuwa zile *by products* ambazo zinazalishwa pale zinatosha kutumia boiler hiyo ya aina mpya litaweza kutumika na kutoa umeme zaidi utakaosaidia katika maeneo ya Mahonda. Kwa hivyo, naomba tuwe na subra kwani serikali itatoa kauli rasmi juu ya suala hili mara tu ripoti hii itapofika katika *cabinet* na kujadiliwa. Ahsanteni sana.

Nam. 53

Wavuvi wa Mtambile Kupatiwa Zana za Kisasa

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:-

Uvuvi ni shughuli kubwa ya kiuchumi na wananchi wengi wanaoishi ukanda wa Mashariki wa Jimbo la Mtambile mnamo maeneo ya Kangani, Kuukuu, Likoni na Chole. Hata hivyo, wananchi hawa bado wanatumia zana duni za uvuvi.

Je, wizara yako ina mpango gani wa kuwapatia wavuvi hawa zana za kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi na kujikwamua na umasikini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Aljibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu swali lake naomba nikubaliana nae kwamba uvuvi ni shughuli kubwa ya kiuchumi ya wananchi wengi sio tu Wajimbo la Mtambile lakini wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, zaada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika juhudi zake za kuwaendeleza wavuvi wa Ukanda wa Mashariki ya Jimbo la Mtambile, imewapatia miradi kupitia fedha za *MACEMP/TASAF* kama ifuatavyo:-

- Kijiji cha Chole kimepatiwa boti ya uvuvi yenye thamani ya sh. 12 milioni.
- Kijiji cha Kuukuu kimepatiwa mradi wa uvuvi wenye thamani ya shs. 9.6 milioni.
- Kijiji cha Kangani kimepatiwa mradi wa uvuvi (boti, nyavu na mashine) vyenye thamani ya shs. 16 milioni.
- Kijiji cha Likoni wamewa boti, *machine* na nyavu vyenye gthamani ya shs. 35 milioni.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo naomba nikiri kwamba miradi hiyo ni michache sana isiyokidhi kiu ya mahitaji ya zana za kileo za uvuvi kwa wananchi wote wa Jimbo la Mtambile na Majimbo mengine ya Zanzibar. Wizara yangu inatazamia kuwaendeleza wavuvi wote wa Zanzibar kupitia mradi wa *MACEMP* na miradi mengine ambayo sasa imo katika ngazi ya kuibuliwa na matayarisho, ikiwemo kuwaalika wawekezaji katika sekta ya uvuvi wa maji ya ndani, uvuvi wa Bahari Kuu na Ufugaji wa Mazao ya Baharini.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inamuahidi Mhe. Mwakilishi kwa niaba ya wavuvi wake wa Jimbo la Mtambile kwamba mara zana za kisasa za uvuvi zitakapopatikana au fursa za uwekezaji katika sekta ya uvuvi zinazotarajiwa zitakapokamilika basi wavuvi wake na wavuvi wengine wa Zanzibar watafaidika.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na mikakati mizuri ya serikali ya kuwaanzisha watu katika masuala ya uvuvi. Je, serikali imepanga mikakati gani ya kuweka maeneo ya kuhifadhia samaki.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika ni kweli kwamba tuna maeneo ambayo wizara yangu imeyafanyia kazi kwa umakini zaidi, suala la kuekeza katika masuala ya *cold room* na pia viwanda vya *ice plant* hilo linazingatiwa na linafanyiwa kazi. Pia katika maeneo ya bandari za uvuvi. Kwa hivyo, hayo ni maeneo mawili tunayashughulikia, lakini eneo moja muhimu ni suala la uundaji wa boti hapa Zanzibar suala hilo tunalizingatia na hata katika ziara ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais juzi alipokwenda Iran alizungumza hilo na kwa kweli tuna matarajio makubwa kulikamilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Idara ya Uvuvi hasa katika awamu ya sita ya nchi hii ilijitahidi sana kutoa vifaa vya uvuvi kama vile maboti na machine zako, naomba kujua kwa Zanzibar nzima idara yake ilitoa boti ngapi na je, hadi sasa ngapi hazijauzwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wizara yangu katika awamu iliyopita ilijitahidi sana kutoa zana mbali mbali za uvuvi katika shehia takriban zote za Zanzibar kila shehi wizara ilijitahidi kwamba ipate aina moja ya zana ama boti au *machine*, au nyavu. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli imefanya kazi kubwa kama alivyosema yeye mwenyewe na suala lake linahitaji takwimu ili zilizofanyiwa kazi vizuri. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba naahidi mbele yako kwamba nitaleta jibu hilo kwa maandishi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, tunakumbuka kwamba katika awamu ya sita ya utawala wa serikali hii, Serikali ya Japan ilitaka kusaidia Idara ya Uvuvi ujenzi wa bandari ya wavuvi ambayo bandari hiyo mfano kama iliyokuwepo pale Dar es Salaam ambayo ingeliweza kusaidia kuweza kuweka wavuvi watakaporudi baharini pamoja na kujenga *cold rooms* ambazo zitasaidia wavuvi wote wanaorudi kuvua samaki kuweza kuwahifadhi.

Je, mradi huu Mhe. Waziri umefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika awamu iliyopita kulikuwa na mpango wa kujengewa bandari ya uvuvi na soko kubwa hapa Zanzibar. Lakini mradi ule haukuweza kukamilika kwa sababu eneo ambalo wafadhili walitaka lijengwe kimazingira ilikuwa

haiwezekani kujengwa kwa sababu lingeleta matatizo makubwa ya kimazingira katika mji wetu wa Zanzibar. Katika mvutano huo mradi ule haukukamilika, lakini wizara yangu kwa kupitia mfadhili huyo huyo tumo katika mazungumzo ya kuona kwamba soko la kisasa na bandari ya wavuvi inajengwa katika eneo ambalo zamani ilikuwa ni Shirika la Uvuvi – Malindi. Kwa hivyo, michoro imeanza, tathmini ya kimazingira imeshafanywa na mazungumzo baina ya wizara na mfadhili Serikali ya Japan inaendelea na tuna imani kwamba ikifika mwishoni mwaka huu basi jitihada zitakuwa zimeanza kuonekana.

Nam. 57

Mikopo ya Ng'ombe wa Maziwa

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni, baadhi ya wafuagaji walibahatika na mikopo ya ng'ombe wa maziwa kupitia mpango wa "Kopa ng'ombe lipa ng'ombe ambapo hata hivyo wenig wa ng'ombe hao walikufa mapema na baadhi yao kushindwa kutoa maziwa kama ilivyokusudiwa.

(a) Je, nini kilikuwa chanzo cha ng'ombe hao kufa mapema na wengine kushindwa kutoa maziwa.

(b) Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wafugaji ambao ng'ombe waliokopeshwa walikufa kwa lengo la kuwaendeleza wafugaji hao na sekta ya mifugo kwa ujumla

(c) Wizara ina mikakati gani ya kuimarisha zaidi mpango huo wa "Kopa ng'ombe lipa ng'ombe" kwa kuwakopesha wafugaji ng'ombe bora zaidi watakaoleta tija kwa wafugaji.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu naomba nieleze kwamba katika jitihada za Serikali za kuwaendeleza wafugaji. Programu mbali mbali zimekuwa zikiibuliwa kwa lengo lenye dhamira njema ya kuinua hali za maisha ya wafugaji. Miongoni mwa program hizo ni hii ya "kopa ng'ombe lipa" ambayo ilianza mwaka 2001 na uliendeshwa na iliyokuwa Idara ya Maendeleo ya Mifugo chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la nguvu za Atomiki Duniani

(*IAEA*) kwa nia ya kuendeleza sekta ya mifugo baada ya maangamizi ya Ndorobo katika kisiwa cha Unguja. Kabla ya wafugaji kupatiwa ng'ombe hao walitakiwa waoneshe robo eka ya majani ya kupanda, na aidha walipatiwa mafunzo juu ya utunzaji bora wa ng'ombe wa maziwa. Aidha programe nyengine akama *HPE,PADEP,TASAF* na nyengine zilishiriki baadae.

(a) Mhe. Naibu Spika, chanzo cha baadhi ya ng'ombe hawa kufa ni pamoja na matunzo hafifu waliyokuwa nayo ikiwa ni pamoja na kutoshiba vizuri kwa ng'ombe, malisho yenye lishe duni, kutoshughulikiwa kutibiwa na kuwekwa kwenye mazingira machafu. Vyanzo hivi vilisababisha ng'ombe kuwa katika mazingira hatarishi yenye kukaribisha ng'ombe kushambuliwa na maradhi yaliyosababisha udhaifu ya afya ya ng'ombe na kusababisha vifo.

(b) Naomba ifahamike kwamba hakuna mfugaji aliyelazimishwa kulipa ng'ombe baada ya ng'ombe aliyopewa kufan na kwamba wizara ilichokifanya iliendeleza taaluma ya ufugaji kupitia mashamba darasa ili kuimarisha huduma za ushauri, taaluma ya Kinga na Tiba kwa wafugaji na kuwashajiisha kuunda vikundi vya ufugaji kuwapatia mikopo midogo midogo, na kuwawezesha kuwa na muamko ili kuweza kusaidiana na Serikali katika kubuni na kuendeleza mipango na program endelevu za kuendeleza sekta ya mifugo.

(c) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu sasa ina mpango madhubuti wa kuendeleza sekta ya mifugo zaidi kwa utaratibu wa ufugaji wa mkataba (*Contract Farming*) ambapo wafugaji au vikundi vya wafugaji watatiliana mikataba wa ufugaji baina yao na mwekezaji, kwa lengo la kushirikiana baina ya mwekezaji na mfugaji, katika mambo kadhaa yakiwemo:-

- Upatikanaji wa mbegu bora ya wanyama
- Namna ya ufugaji bora
- Utaratibu wa kumtibu mnyama
- Namna ya kupata soko la uhakika wa mnyama au bidhaa.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inaendelea kushajiisha na kuhamasisha watu mbali mbali wakiwemo wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika uzalishaji wa mifugo na mazao yake. Aidha, Jumuiya za Wafugaji pamoja na wafugaji wadogo

wadogo wataendelea kupewa umuhimu katika kuendeleza sekta ya mifugo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Waziri swali hili ni mara nyingi wananchi wanalalamikia kupata ng'mbe waliokuwa sio wazuri halafu wanakufa mara moja. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa wanafanya makusudi maafisa wako kuwaletea ng'ombe waliokuwa *grade* ya chini ili kupoteza pesa kwa makusudi.

b) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wizara yake imejilinda vipi na masuala haya ya kuwa hizi fedha zisiendelee tena za wafadhili kupotea.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, sio kweli hata kidogo kwamba Maafisa wa Idara ya Mifugo wamekuwa wakifanya uzembe katika kuwapatia wafugaji ng'ombe ambao hawana sifa au ng'ombe hafifu. Usahihi ni kwamba katika suala la kuagiza au kununua ng'ombe kamati zenyewe za wafugaji ndio ambazo huenda kununua ng'ombe wenyewe. Kwa hivyo, katika kikundi ambacho labda cha wafugaji wamo afisa mmoja wa mifugo, anachofanya yeye ni kuwashauri kwamba ng'ombe huyu tusimchukue au ng'ombe huyu tumchukue.

Lakini uamuzi wa mwisho si wa Afisa wangu wa Mifugo uamuzi wa mwisho ni wa vikundi vyenyewe vya ushirika ambavyo pesa wanazo wenyewe na wao ndio wanaofanya maamuzi ya manunuzi. Kwa hivyo, kuwashitumu Maafisa wangu wa Idara ya Mifugo au Idara yenyewe ya Mifugo kwamba ilishiriki kununua ng'ombe hafifu kwa kweli hilo sio sahihi ni juu yao wafugaji baada ya kupewa ushauri na mtaalamu wetu kuona kwamba ushauri wenyewe wanauchukua. Kwa hivyo, ningependa sana kupitia Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kuwaambia wafugaji wote wa Zanzibar mara zote wachukulie maanani ushauri uliotolewa na wataalamu katika kuendeleza sekta ya mifugo katika nchi yetu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, wavuvi wanapokuwa baharini kufanya shughuli zao za uvuvi mara nyingi huwa wanakumbwa na dharuba, lakini wanapopita katika visiwa kama Chumbe kwa Unguja na Pemba ni Misali huwa wanakwenda kujificha kwenye visiwa hivyo lakini huwa hawaruhusiwi kujificha upepo na hatima yake wakifika sehemu

kama hizo huambiwa wamevuwa katika maeneo hayo ambayo hayaruhusiwi kuvuwa na badala yake kupata majanga kama ya kuzama.

Je, ni lini kero hii itawaondokea wavuvi katika shughuli zao za kikazi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kushirikiana na wavuvi wenyewe imeunda hifadhi ya ukanda wa bahari kwa lengo la kuhakikisha kwamba bahari yetu inaendelezwa na kuhakikisha kuwa hakuna uharibu wa mazingira katika maeneo ya bahari yetu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili suala muhimu na naomba sana Wajumbe wa Baraza hili tukufu tusaidiane katika hili, hili sio suala la wizara yangu tu ni suala ambalo kila Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kila mwananchi wa Zanzibar lazima awe na mwamko nalo kuona kwamba mazingira ya bahari yanatunzwa ili kuona mazalio ya samaki yaliyomo yanakuwa kwa maslahi ya sisi tuliopo na vizazi vijavyo.

Kwa hivyo, kinachotokea ni kwamba baadhi ya wavuvi wetu huamua kufanya uvuvi usiotakiwa katika maeneo ya hifadhi, hili naomba tusikubaliane na sheria ipo tumeitunga wenyewe katika Baraza hili tukufu na ndio inayofuatwa kuona kwamba shughuli hizi zinadhibitiwa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi badala ya kuwatetea wahalifu wanaovunja sheria katika bahari yetu ingeshirikiana zaidi na Maafisa wa Uvuvi na Mifugo kuona kwamba sheria tuliotunga katika Baraza hili tukufu imekuwa *enforced* ili kuona mazingira ya bahari yetu yamekuwa salama.

Nam. 66

Kuendeleza Zao la Karafuu

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Zao la Karafuu ambalo ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya mapato katika uchumi wa Zanzibar, linaonekana kudorora kutokana na mikarafuu mingi kufa au kuzeeka na hivyo kushindwa kutoa mazao kama inavyostahiki.

(a) Kufuatia hali hiyo, wizara yako ina mpango gani wa kuliendeleza zao hili kwa kuhakikisha karafuu nyingi zaidi zinazalishwa na hivyo kusaidia katika uchumi wa Zanzibar.

(b) Wizara ina mpango gani wa kufanya utafiti ili kujua ubora wa miche ya mikarafuu inayotayarishwa na wizara yako, hasa kwa kutilia maanani madai ya kuwa miche hiyo inakufa haraka.

(c) Wizara yako imechukua juhudi gani za kutoa motisha na kuwahamasisha wakulima wa zao hilo ili kuongeza uzalishaji.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.66 lenye vifungu (a),(b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu ina mpango ufuatayo kuendeleza zao la Karafuu:-

- Kutoa Elimu ya Kilimo Bora cha Mikarafuu pamoja na kuchanganya na mazao mengine hususan yenye kupenda vivuli kama vile Vanilla, Hiliki, Manjano na Tangawizi.

- Kutafuta fedha za ziada kwa mradi wa kuendeleza zao la karafuu ambapo kwa sasa unafadhiliwa na serikali tu. Fedha zinazopatikana husaidia kuzalisha miche tu na kuwapa wakulima bila ya malipo.

- Kufanya tathmini kujua idadi ya mikarafuu yote iliyopo Zanzibar pamoja na maeneo yaliyokuwa matupu ambayo yanawezwa kupandwa mikarafuu. Tathmini ya mwisho imefanyika mwaka 1997 ambayo imeonyesha kuwa kuna mikarafuu 5,833,100 kati ya hiyo, 5,042,700 kwa Pemba na 990,400 ipo Unguja.

- Kufanya mashamba darasa ya maonesho, madarasa hayo ya maonesho yatakuwa Unguja na Pemba.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. imebainika kwamba mikarafuu mingi sasa inakufa kwa sababu ya upungufu wa maji katika ardhi. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani kwa kuwashajihisha wakulima lakini na kuwapa msaada kidogo wa kuweza kupata maji ya kutilia mashamba yao.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoelewa sote mkarafuu ni mti ambao una thamani kubwa sana kwa sisi Wazanzibari kwa uchumi wetu na mustakabali mzima wa watu wetu, na kwa historia ya

kutambulika kwetu. Lakini mkarafuu ni mjiti mgumu sana, unahitaji matunzo ya hali ya juu, hauna wepesi katika kupanda kwake na kulelewa kwake. Kwa hivyo, unataka umakini na mkulima kujituma.

Maji kutokana na hali halisi ya kubadilika kwa hali ya nchi, imekuwa ni sehemu moja sasa inayoongezea katika kuendelea kuteketeza mikarafuu yetu. Lakini si dhani kama maji pekee ndio sababu kuu ya hali halisi ya zao letu la karafuu kwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kumalizia na swali lake la nyongeza nieleze tu, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hivi karibuni imefanya maamuzi thabiti ya kuhuisha namna tunavyosimamia zao letu la karafuu. Imebainika kwa kipindi kirefu kwamba lilikuwa zao lenyewe halina mwenyewe, kwa maana Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikuwa na majukumu ya kutafuta miche, *ZSTC* inauza, lakini usimamizi hasa juu ya kuhakikisha kwamba zao hili linastawi kwa mustakabali wa maslahi ya nchi yetu kuanzia mche kupandwa kwake, kulelewa kwake, kuwatunza wakulima na kuwapa motisha, kuwashajihisha wananchi wetu kulima na kuliendeleza zao lenyewe.

Kwa hivyo, hivi sasa serikali imeshaamua kwamba, *ZSTC* itafanya mageuzi makubwa ya kitaasisi na kisheria ikisimamiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili kuhakikisha kwamba hili zao sasa lina mwenyewe kikamilifu kuanzia a hadi z. Kwa maana yote tunayoyatambua yanayohusiana na zao letu la karafuu sasa yatasimamiwa ipasavyo na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na taasisi yake ya *ZSTC*, ikiwemo fidia kwa wakulima wanapopata ajali, bila zao na utunzaji wa wakulima na kadhalika. Kwa hivyo, maamuzi hayo yameshafanyika na tunategemea sasa tutakuwa na mwelekeo mzuri zaidi wa zao letu hili kuu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa Mhe. Waziri alikiri kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa katika zao zima la karafuu. Namuuliza kwamba je, kuna utaratibu wowote ulioandaliwa kuweka takwimu ya *population* ya mikarafuu angalau kila baada ya miaka 10 ili kuionesha ile *petal* yote ya nchi inavyokwenda kuhusu zao hili la karafuu na kuipa picha nzima serikali au wizara itakayohusika hasa kuweza kuchukua hatua zinazofaa katika kulishughulikia hili zao wenyewe.

Mhe. Waziri waKilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, zao letu la karafuu tunalitambua kwa maana la kwetu, tunalijua tangu asili yake na hapa tulipo. Kam anilivyokwishaeleza kwamba sensa ya mwisho ilifanywa mwaka 1997, siku nyingi zimepita na tuligundua kwamba kuna mikarafuu 5,833,100 mingi ya hiyo ikiwepo Pemba 5,042,700 na Unguja ikiwepo 790,400.

Kwa misingi hiyo na yale niliyokwishaeleza awali, serikali imeona kwamba sasa wakati umefika hii hali tunayokwendanayo ilikuwa inapelekea aidha nchi yetu kukosa tina na zao lake hili kuu, wakulima kupoteza imani na kulima zao la karafuu na hilo lilionekana serikalini kwamba si jambo la busara kwa nchi yetu, hatma ya watu wake na uchumi wake. Kwa mnasaba huo, hayo mageuzi niliyoyazungumzia sasa yatasimamiwa na Wizara ya Biashara kwa kufikia malengo ambayo tunayazungumza.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lenye a na b.

a) Wizara ya Kilimo inajitahidi kutoa miche kwa wakulima, lakini katika utafiti wetu miche hii ukuaji wake kunachukua muda mfupi na hatimaye inakufa, ni bora ile ambayo wakulima wanang'oa misituni katika mashamba kuliko ile inayotunzwa na Wizara ya Kilimo. Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha miche yao ina ubora zaidi kuliko ile ya kienyeji.

b) Katika miaka ya 80 Wizara ya Kilimo ilileta dawa ya *dieback*. na kwa kule Pemba mikarafuu mingi baada ya kupatiwa matibabu yale ndipo mikarafuu ilipokufa mingi zaidi badala ya kupona. Je, ile ilikuwa ni dawa au ni njama za kitaalamu za kuhujumu uchumi wetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu na kupitia kwao wananchi wetu wa Zanzibar hasa wakulima wetu, kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili ina uhakika na kile ambacho kinasimamia na kukifanya. Miche ya mikarafuu ina ubora wa hali ya juu kabisa, kwa maana ya taaluma, uzoefu na ujuzi katika kuiatika miche hiyo. Hata mimi mwenyewe mwaka uliopita nilipanda mikarafuu 200 shambani kwangu, mwaka huu ninaendelea kupanda karibu ya 300.

Ni dhahiri kwamba yale niliyozungumza awali mkarafuu mgumu sana, sana, mkarafuu unataka malezi ya hali ya juu na matunzo. Sasa kwa vile hoja imetoka Baraza la Wawakilishi juu ya ubora, mimi nasema ubora tuna uhakika nao, lakini katika kuendeleza zao hili na kutengeneza nchi tutaendelea kutizama hivyo tunapokea hoja hiyo ya Mhe. Mwakilishi na tunaendelea kuhimizana kuhakikisha kwamba ubora huo tunauendeleza.

Kuhusu habari ya maradhi ya *dieback*. Mhe. Naibu Spika, taarifa niliyonayo mimi mikarafuu inasumbuliwa na maradhi mawili, moja ni *sudden death*

ambapo mkarafuu huwa unakufa ghafla na wa pili ni *dieback* ambapo unaanza kileleni kule na kuanza kufa kidogo kidogo. Miaka ya 80 naelewa kwamba palikuwa na utaratibu wa hizo dawa zilizoletwa na ni kweli pakawa na malalamiko mengi sana. Hata hilo shamba nililozungumzia mimi kulipanda ambalo nimelirithi kwa Marehemu Baba yangu Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema, mikarafuu yote ilikufa. Kwa hivyo, hilo lilitokea lakini sina taarifa sahihi kwamba juhudi zile zilizofanywa zilichangia katika kuuwa hiyo mikarafuu au palikuwa na sababu nyenginezo.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri nafikiri atakubaliana na mimi kwamba zao la karafuu ni uchumi wetu kitaifa, katika majibu yake mama amezungumzia sana juu ya kuhuisha au kuzalisha mikarafuu mipya. Je, Mhe. Waziri una mikakati gani na wizara yako ya makusudi kwa wale wanaochukua jitihada ya kuikata mikarafuu mibichi kwa ajili ya kuijengea.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba zao la karafuu kwa asilimia kubwa sana linachangia katika uchumi wa Zanzibar na ni zao letu kuu na lina faida kubwa sana kwa wakulima wa nchi yetu. Nimekwishakueleza katika jibu langu la msingi na majibu ya nyongeza ambayo nimekuwa niyajibu, hili nafikiri linafika la tano sasa. ni kwamba serikali imeona mapungufu haya na serikali inatambua kwamba kunahitajika mwelekeo mahsusi na thabiti katika kulilinda zao hili la karafuu.

Katika hayo mageuzi ambayo yatafanywa katika taasisi ya *ZSTC,* hayo yote yatazingatiwa. Kwa hivyo, tunaomba tuendelee kuwa na subira naamini wakati utafika na wakati huo hautokuwa mkubwa sana kwa kusubiri kwetu, mazingira hayo yote yatasimamiwa ipasavyo.

Nam. 69

Kudhibiti na Kuongeza Maeneo ya Hifadhi ya Misitu

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Pamoja na juhudi mbali mbali za serikali katika kulinda misitu na rasilimali zilizopo bado kuna wimbi kubwa la uharibifu wa hifadhi za misitu hasa kwa ukataji wa miti kwa kutumia misumeno maalum ya moto.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kudhibiti tatizo hilo baada ya hatua zote zilizochukuliwa awali kushindwa kulimaliza.

(b) Serikali ina mipango gani madhubuti na inayotekelezeka ya kuongeza hifadhi za misitu ili kuhakikisha rasilimali hiyo inadumu kwa vizazi vijavyo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako, ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.69 lenye vifungu (a), na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inakiri kuwepo kasi kubwa ya ukataji miti kwa kutumia misumeno ya moto (*Chain saws*) baada ya kuimarika kwa teknolojia hiyo katika miaka ya hivi karibuni. Misumeno hutumika hasa katika maeneo yaliyo nje ya misitu ya hifadhi na badala yake imekuwa ikitumika zaidi kwa ukataji wa miti ya matunda na mazao ya biashara, ikiwemo Minazi, Miembe, Midoriani, Mifenezi, Mishelisheli na Mizambarau.

Naweka bayana kwamba, suala la kuzuia matumizi mabaya ya misumeno ya moto linahitaji kuungwa mkono na wananchi wote, kwani madhara yake ni makubwa kimazingira na kuadimika upatikanaji wa matunda sio tu huwapunguzia kipato wakulima, bali pia hupelekea kukosekana kwa lishe muhimu itokanayo na matumizi ya matunda mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, wizara yangu inaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

- Kuelimisha jamii juu ya madhara ya kutumia misumeno ya moto katika kukata miti, kwani hupelekea kuteketea miti mingi kwa muda mfupi na kusababisha uharibifu wa mazingira na ongezeko la kuadimika miti muhimu kwa muda mfupi.
- Kuchukua hatua za kuwakamata na kuwatoza faini au kuwafikisha katika vyombo vya sheria wanaohusika na ukataji miti ovyo.
- Kutayarisha sheria ya kudhibiti uingizaji na utumiaji wa misumeno ya moto.

Mbali na hayo yote, tunawaomba wananchi wote waendelee kushirikiana na wizara yangu hii katika juhudi za kuwafichua na kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote wanaokata miti bila kufuata taratibu halali za serikali.

(b) Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Zanzibar ina misitu mitatu mikuu inayotambulika kimataifa, ambayo ni Hifadhi ya Taifa ya Jozani – Ghuba ya Chwaka (5,000 hekta), Hifadhi ya Msitu wa Hakiba wa Kiwengwa – Pongwe (3,325 hekta) na Msitu wa Hifadhi ya Kimaumbile wa Ngezi – Vumawimbi (hekta 2,900). Msitu wa Hifadhi wa Msitu Mkuu Micheweni (hekta 280) na Msitu wa Hifadhi wa Ras kiuyu (hekta 200).

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda kulitambulisha Baraza lako tukufu kwamba wizara imeshaanza maandalizi ya kuongeza maeneo ya misitu ya hifadhi, ambapo hatua za kuyatangaza maeneo hayo itafuata.

- Msitu ulipo upande wa Mashariki ya Muyuni (baina ya kijiji cha Jambiani na kijiji cha Muyuni) kwa hapa Unguja.

- Msitu ulipo mashariki ya Kijiji cha Umbuji na Uroa/Ndudu, Unguja.

Mhe. Naibu Spika, fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli hizo zipo kwa ufadhili wa Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Kanda ya Pwani, chini ya ufadhili wa *GEF/UNDP* na kusimamiwa na wizara hii kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka tunategemea zoezi hilo kukamilika kwa kuchelewa ndani ya miaka miwili hivi (2011-2014).

Nam. 98

Ajira kwa Vijana

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Tatizo la ajira kwa vijana wa Zanzibar ni kubwa na la muda mrefu, kutokana na serikali ikitambua tatizo hilo Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika iliandaa mpango wa utekelezaji wa ajira kwa vijana (*Youth Employmnet Action Plan*).

(a) Je, mpango huo umefikia hatua gani.

(b) Kama mpango huo bado haujaanza, sababu gani zilizokwamisha mpango huo na lini utekelezaji wake utaanza rasmi.

(c) Nini unawaahidi vijana wa kizanzibari katika kupunguza tatizo la ajira nchini kutokana na mpango huo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake Nam. 98 lenye vipengele a, b na c kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa mpango wa ajira kwa vijana ulitayarishwa maalu ili kusaidia upatikanaji wa ajira kwa vijana wa Zanzibar kwa lengo la kupunguza tatizo la ajira nchini. Mpango huu uliandaliwa sambamba na sera ya ajira na mpango wa kutengeneza ajira.

b) Mhe. Naibu Spika, mpango huo wa ajira kwa vijana unaendelea kufanyiwa kazi ili kufiikiwa madhumuni yaliyokusudiwa ya kuwapatia ajira vijana. Hata hivyo, mpango huo ambao utekelezaji wake utahusisha sekta mbali mbali kwa sasa, unaratibiwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na wizara yangu, ni miongoni mwa washiriki wakuu wa utekelezaji wa mpango huo.

c) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyozungumza katika kipengele (a), mpango huo umeanza kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na wahisani mbali mbali, wakiwemo Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) na Serikali ya Norway. Mfuko wa kusaidia vijana kujiajiri umeanzishwa kupitia misaada ya mashirika hayo. Aidha, kupitia Mfuko wa AK na JK na ule wa kujitegemea, walengwa wakubwa ni vijana ambao husaidiwa fedha kwa kuwawezesha kujiajiri katika shughuli mbali mbali za kiuchumi.

Hata hivyo, suala la ajira kwa vijana bado ni changamoto, kwani vijana wengi wanategemea wakimaliza masomo waajiriwe na serikali wakati nafasi za ajira kwenye serikali ni finyu, na sekta binafsi hapa Zanzibar haijakomaa vya kutosha kuweza kutoa nafasi za kutosha za ajira kulingana na mahitaji.

Wizara yangu inaifanyia kazi changamoto hii kwa kubuni mikakati ya kuimarisha programu ya kuwawezesha wananchi wakiwemo jijana. Programu hizo zitahusisha kupanua fursa ya upatikanaji mikopo, elimu ya biashara kwa wajasiria mali, mafunzo juu ya mbinu bora ya uzalishaji ili kuleta tija zaidi pamoja na uimarishaji wa vyama vya ushirika na vikundi vya kuweka na kukopa (*SACCOS*).

Mhe. Naibu Spika, lengo la mpango wa ajira kwa vijana ni kuwasaidia vijana wetu kupata ajira au kujiajiri na hivyo kupunguza pengo la ukosefu wa ajira nchini. Hivyo, kwa kushirikiana na wizara inayohusika na masuala ya vijana tutaendelea na hatua za kutekeleza mpango huu kwa kuwajengea uwezo vijana kujiajiri au kuajiriwa katika maeneo mbali mbali ya kazi. Aidha, wizara yangu imo katika mchakato wa kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa za soko la ajira ambao utawawezesha watafutaji kazi wakiwemo vijana kupata taarifa kwa urahisi juu ya fursa za ajira zilizomo katika wakati husika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wetu wa maswali unakaribia kumalizika na bado tumebakiwa na maswali matatu, namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais alete utaratibu ili tumalize maswali yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobaki kumalizia maswali yaliyomo kwenye *order paper* ya leo hautoshi, naomba Baraza lako tukufu liridhie tuweke kando kanuni hii ya maswali ili tuweze kuongeza muda.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwaombe wajumbe wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda. Tunaendelea.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba wananchi na vijana kwa ujumla hawajui majukumu ya wizara yako. Kama hivyo ni kweli, wizara yako itachukua jitihada gani ya kuwaelimisha wananchi kwamba wizara yako iko kw ajili ya kuwawezesha wananchi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, swali sikulifahamu.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba wananchi na vijana kwa ujumla hawajui majukumu ya wizara yako. Kama hivyo ni kweli, wizara yako itachukua jitihada gani ya kuwaelimisha wananchi kwamba wizara yako iko kwa ajili ya kuwawezesha wananchi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Amina Iddi na sasa niko tayari kujibu swali

lake. Mhe. Naibu Spika, napenda nimhakikishie kwamba taaluma hizo sasa zimeshaanza. Jana tumeanza Mkoa wa Kaskazini Unguja, leo tuko Mkoa wa Kusini na semina hiyo niliifungua mimi jana na leo wanaendelea watendaji kwa sababu imeshafunguliwa. Mkoa wa Mjini Magharibi na Mikoa miwili ya Pemba itafuatia katika siku za karibuni.

Ni kweli kumekuwa na utata mkubwa wa kuelewa utekelezaji wa kazi za wizara hii, lakini moja katika wizara nyeti na muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu hasa katika suala zima la kupunguza umasikini.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu Mhe. Waziri mwenyewe amekiri tatizo kubwa lililokuwepo la ajira hasa ikizingatiwa wengi wa vijana wetu wanategemea ajira kutoka serikalini, lakini baada ya kuundwa wizara hii ambayo lengo lake ni kusaidia kupunguza tatizo hili. Kupitia katika vyombo vya habari tumesikia kwamba Mhe. Waziri alifanya ziara ya nchi kama za Qatar hivi karibuni katika sehemu ya ujumbe wa Makamo wa Kwanza wa Rais katika ziara ya Nchi ya Oman.

Kwa sababu katika ripoti zilizoripotiwa na vyombo vya habari ilielezwa kwamba katika mazungumzo yake huko yamehusiana na suala la kuinufaisha Zanzibar hasa vijana kwa upande wa ajira. Sijui anaweza kuwaeleza wananchi wa Zanzibar kupitia Baraza hili kwamba ni manufaa yepi yaliyopatikana katika ziara zake hizo za nchini Qatar na Oman ili vijana waweze kuwa na mategemeo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, jambo lolote zuri halitaki haraka na ziara ndio zimekwendwa hivi karibuni. Jambo lolote kama hili ambalo tunalijenga hivi sasa linahitaji kuwa na subira kidogo. Lakini napenda nimuhakikishie kwamba, katika ziara ambayo nilipata heshima kubwa mimi Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi nikiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika nilipata mwaliko wa Mfalme wa Qatar kwa madhumuni ya kwenda kuhudhuria mkutano unaohusiana na mambo ya *Community Development.* Nashukuru nilipata nafasi ya kwenda kumuona katika *palace* yake na miongoni mwa mambo tuliyozungumza ni uwezekano wa kuwa na utaratibu maalum wa kuwa na miradi ambayo itawezesha wananchi kiuchumi na kuondokana na tatizo la umasikini pamoja na masuala ya elimu, afya na mambo mengineyo.

Hivi ninavyosema ni mapema mno kutaja yale mambo ambayo tuliyazungumza. Kwa sababu kuna kamati maalum imeachiwa jukumu hilo na wanashirikiana na hasa katika suala zima la kuanzishwa programu hizo. Kwa hivyo, ni mapema kutoa taarifa kwa sababu bado hazijawiva.

Lakini pia napenda nimhakikishie katika ziara ambayo nilikuwemo Oman pamoja na Makamo wa Kwanza wa Rais nilipata nafasi ya kuonana na Waziri anayehusika na *Manpower* na miongoni mwa mambo tuliyoyazungumza ni uwezekano wa kuwachukua Wazanzibari na kwenda kufanya kazi za heshima katika nchi hizo.

Tatizo lililojitokeza kumekuwa na matatizo na minong'ono na pengine hata malalamiko kwamba vijana wetu wakifika katika maeneo hayo huwa wanapata shida kweli. Imethibitika ni kweli hata Ubalozi wetu pale Omani walituthibitishia kwamba kweli kuna matatizo wanachukuliwa watoto au vijana hapa hakuna mikataba.

Sasa mikataba hiyo tumeshafanya *draft* na tukijaaliwa tutaipeleka kwa wenzetu wa Oman kwa kuiangalia ili kushirikiana na hivi karibuni tunatarajia kusaini makubaliano *(Memorandum of Understanding)* kati yetu sisi na wizara inayohusika ili kuwa na utaratibu mzuri wa kuwapeleka vijana wetu katika nchi hizo na nyenginezo.

Nam. 54

Ongezeko la Wanafunzi Skuli ya Kengeja

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza**:-**

Skuli ya Ufundi Kengeja ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 56 tu, lakini hivi sasa ina wanafunzi takriban 150 jambo linalopelekea msongamano mkubwa kwenye mabweni ya wanafunzi hao na kupelekea maambukizi ya magonjwa mbali mbali yanapoingia.

Kwa kuzingatia hali hii. Je, Wizara haioni kuwa sasa ipo haja ya kujenga mabweni ya wanafunzi ili kwenda sambamba na ongezeko la wanafunzi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Skuli ya Sekondari ya Ufundi ina madarasa matatu tu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120. Pia dakhalia zilizopo zina uwezo wa kuchukua wanafunzi 56, kati yao wavulana 32 na wasichana 24. Hivi sasa skuli ina wanafunzi 160. Ongezeko la wanafunzi limetokana na kuongezeka kwa wanafunzi wanaofaulu na kujiunga na mchepuo wa ufundi. Ni kweli kuwa

dakhalia zilizopo hazitoshi kuhudumia wanafunzi wote na kusababisha baadhi ya wanafunzi kulala katika majengo ambayo hayakukusudiwa kuwa dakhalia kama vile msikiti.

Mhe. Spika, Wizara imeiona kasoro hiyo na imeshachukua hatua ya kujenga madarasa manne ambapo kazi imefikia hatua ya upigaji wa plasta na utiaji sakafu. Wizara inakusudia kuanza ujenzi wa dakhalia katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika swali la msingi kuliuliziwa suala la ongezeko la wanafunzi zaidi ya uwezo wa skuli kutoka wanafunzi 56 hadi kufikia 150, hali ambayo sio tu inaongeza matatizo katika madakhalia lakini pia usomaji katika skuli. Kwa sababu vyama vyote viwili vikubwa vilivyoshiriki katika uchaguzi huu na kutueleza katika uchaguzi viliahidi kwamba vitashughulikia suala la ukubwa wa darasa kwa kupunguza idadi ya wanafunzi katika kila darasa.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako imejipanga kiasi gani kupitia serikali hii ya awamu ya saba kulitekeleza hili ambalo limeahidiwa na vyama vyote viwili vilivyoundwa serikali hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ni kweli serikali kati ya moja ya ahadi yake katika awamu hii ya saba ilizungumzia kupunguza ule wingi wa wanafunzi katika madarasa.

Mhe. Naibu Spika, suala hilo wizara yangu tunalifanyia kazi kama nilivyoeleza kwenye jibu mama ambapo kuna madarasa manne tayari yako katika hatua ya kutia plasta na kuweka saruji.

Lakini kwa skuli nyengine Mhe. Naibu Spika, juzi hapa nilizungumza kwenye jibu langu Nam. 91 kwamba kuna skuli 13 Unguja na Pemba ambazo ni skuli za kisasa kabisa inazojenga Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Kwa hivyo, naamini skuli hizo zikimalizika tutakuwa na uwezo mzuri wa wanafunzi wetu kupata nafasi nzuri na ya utulivu kabisa wa kuendeleza masomo yao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, mimi kama mwanakamati nilitembelea Skuli ya Kengeja. Mhe. Naibu Spika, mbali na majibu mazuri ambayo amesema Mhe. Naibu Waziri kwamba majengo yako katika hali nzuri ya kuendelea kumalizika katika skuli ile lakini iko katika hali mbaya ya uchafu kabisa. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba skuli ile inakuwa

katika hali ya usafi na wanafunzi wanalala katika madakhalia ambayo yako katika hali ya usafi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli ile skuli hususan dakhalia haiku katika hali nzuri. Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi na Mhe. Waziri tulifanya ziara ya kutembelea skuli ile na tukaona tatizo ambalo lipo katika dakhalia. Kuna matatizo ya uchafu licha ya kuwa wizara niseme kama wasimamizi lakini wao wenyewe wanafunzi na walimu wao wanahusika zaidi kwa usafi katika skuli yao.

Lakini katika upande wa matengenezo Mhe. Naibu Spika, ni wiki moja iliyopita tumepeleka shilingi milioni 20 kwa ajili ya kufanyia matengenezo ya dakhalia ile kwa sababu kuna tatizo la tangi linavuja. Kwa hivyo, kutokana na kuvuja kule *ceiling* ya baadhi ya vyumba imeroa na imefanya maharibiko makubwa. Kwa hivyo, tumepeleka hizi pesa ili kuhakikisha matengenezo yale yanafanyika mara moja.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa skuli inayozungumzwa ya Kengeja ni skuli ya ufundi. Kwa kuwa madarasa yaliyoongezeka ni mengi na sasa yanajengwa na mengine. Je, kuna ongezeko gani la zana za ufundi lililopelekwa, ili wale wanafunzi wasome kweli ufundi na sio maneno.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, zana zilizopo katika chuo kile niseme kwamba ni zana ambazo kwa sasa zinatosheleza kwa mahitaji ya skuli ile. Tatizo lilikuwa ni madarasa na nimezungumza kama tumeongeza madarasa manne ya ziada.

Nam. 92

Wananchi wa Pemba Kufaidika na Vipindi vya TVZ

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza**:-**

(a) Je, ni lini wakaazi wa Pemba wataiona TVZ na kufaidika na vipindi vyake.

(b) Ule mpango wa TVZ kuelekea katika matumizi ya *digital* umefikia hatua gani.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika,

(a) Wananchi wa Pemba wataiona TVZ na kufaidika na vipindi vyake mara tu baada ya kukamilika kwa ufungaji wa mtambo wa kurushia matangazo, mtambo huo unatarajiwa kuwasili nchini kuanzia April 15, 2011.

(b) Kazi hiyo ya ufugaji itaambatana na ufungaji wa *antenna* mpya baada ya mnara uliopo Mkoroshoni kufanyiwa marekebisho katika sehemu yake ya juu.

Mpango wa TVZ kuelekea katika matumizi ya utangazaji wa mfumo wa *digital* umefikia katika hatua ifuatayo:

- Kuagiza mitambo miwili ya kurushia matangazo pamoja na *antenna 2 AVR (Automatic Voltage Regulator)* na *UPS (Uninterupted Power Supply)* mbili, mtambo mmoja kwa ajili ya Pemba na mwingine utafungwa Unguja.

- Kuihuisha Studio ya *Karume House* kwa kuipatia vifaa ambavyo tayari vimeshaagizwa.

Mpango mzima wa kuingia kwenye urushaji kwa njia ya *digital* ni endelevu na unakwenda hatua baada ya hatua.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa televisheni hii ya Zanzibar ni televisheni ya umma na wananchi wa Pemba wangekuwa na haki ya kuona vipindi vyake kama wanavyoona televisheni nyengine.

(a) Je, ni kwa nini inachukua muda mrefu sana kwa kifaa kimoja kuagizwa na kuja wakati vitu vya duniani vinapatikana kwa njia ya mtandao tu bila ya mtu kwenda tena sasa.

(b) Tuliambiwa hapa moja katika hotuba za Waheshimiwa Mawaziri waliopita kwamba inatarajiwa kufikia mwaka 2012 nchi yetu iwe tayari imeshaingia katika mtandao wa *digital* maana *analogue*

watafuta duniani hakuna tena. Je, kwa hii *speed* tunayokwenda tutafika kweli sisi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakumbuka nilieleza suala hili la vifaa kwa studio ya Pemba na tukasema si kwamba imechukua muda mrefu. Tulitaka kukiagizia hichi kifaa lakini kwa sababu tayari limeshakuja agizo la duniani kwamba ikifika mwaka 2012 iwe tayari nchi zote za Afrika Mashariki na Kati zimeshaingia katika mfumo wa *digital*.

Kwa hivyo, tukaona hakuna haja ya kununua kifaa hicho wakati kesho kutwa *system* inabadilika nafikiri itakuwa ni upotevu wa fedha, tukaona bora tusubiri ili tukija kununua tunanunua kwa pamoja ikiwa tunaingia katika *system* ile.

Mhe. Naibu Spika, swali (b) kwa kweli nafikiri niliwahi kulitamka awali kwamba tayari vifaa vimeshaagiziwa na ukifika mwezi unaokuja vinafungwa vifaa hivyo. Kwa sababu suala hilo Mhe. Rais kauona umuhimu wake ili tusije tukaachwa nyuma. Kwa hivyo, tayari fedha zimeshatolewa na tayari vimeshaagizwa vifaa na tunaomba subira nafikiri hivi karibuni vitafungwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ni muda mrefu sana Pemba tumekosa umeme na mara zote tunapokuwepo katika Baraza hili tukiuliza maswali hatujapata hata siku moja jibu la kuvunja moyo, siku zote tunapata majibu mazuri tu. Hata hivi karibuni tuliambiwa kwamba umeshaagizishiwa mtambo na karibuni unakwenda kuwekwa. Tukasubiri sana tukauliza vipi, tukaambiwa aaa sasa hivi tunaingia katika *digital* huu mtambo ni wa *analogue* tukiingiza ni hasara bure. Hivi sasa tunaambiwa tunasubiri mtambo wa *digital* na *antenna*.

Kwa sababu mtambo ule kule Pemba umeshakaa miaka mingi haufanyi kazi umeshachakaa na naomba radhi kwa kusema mpaka wale wafanyakazi wenyewe ukiwatembelea wameshachakaa hata kimawazo.

Je, hivyo Mhe. Waziri ana uhakika hasa ukija huu mtambo wa *digital* ukiingizwa pale pamoja na *antenna* kutokana na ile hali ilivyo kule kweli itaweza kufanya kazi, au tutakuja kuambiwa aaa ngoja kumbe kulikuwa na chombo chengine kimeshachakaa tukiagizie tena.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, mimi ninachoomba kwa Mhe. Mwakilishi atupe subira wakati tumeshasema kwamba vifaa vipo na vitafungwa, basi awe na uhakika kwamba hivyo vifaa vitafungwa. Kwa sababu nimeshatembelea wafanyakazi wote na kituo nimeona

hali yake, wafanyakazi wenyewe kwa kweli wamejenga subira na wamejenga imani kubwa kwamba hii shughuli itafanyika karibuni tu.

Mhe. Naibu Spika, hili suala mwenyewe Mhe. Rais ameliona na amelipa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba isifike mwaka 2012 ikawa bado hatujaingia katika mfumo mpya. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi usiwe na wasi wasi mambo mazuri tu.

Nam. 43

Kuzuiliwa Chuo cha *Zanzibar Commercial* Kutoa Mafunzo ya Uuguzi

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza**:-**

Chuo cha *Zanzibar Commercial* kimeanzisha Mafunzo ya Uuguzi Unguja na Pemba. Kutokana na sababu mbali mbali Serikali ililazimika kuizuia Taasisi hiyo binafsi kuendelea kutoa mafunzo hayo.

(a) Kwa kuwa Taasisi hii pamoja na kuzuiliwa kwake inaendelea kutoa huduma hiyo. Ni hatua gani zaidi zilizochukuliwa na Serikali ili kuona kuwa amri iliyotoa inaheshimiwa sambamba na kuwanusuru wananchi kuzidi kutumia gharama zisizo za lazima.

(b) Nini hatima ya wanafunzi hao ambapo kwa sasa wanatarajia kuingia mwaka wa pili wa mafunzo yao.

(c) Kwa kuwa mwekezaji huyu ana nia ya kuipunguzia mzigo Serikali katika fani ya Afya na kwa kuwa Serikali yetu imepanua wigo wa kushirikiana na Taasisi za Watu Binafsi. Je, Serikali ina mpango gani katika kumsaidia mwekezaji huyu ili aweze kufanikisha lengo alilolikusudia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, taarifa ya kuanzishwa kwa mafunzo ya Afya katika Chuo cha Biashara *(Zanzibar Commercial Institute)* tumeipata miaka ya hivi karibuni. Mhe. Nailbu Spika, naomba ieleweke Wizara ya Afya haihusiki na usajili wa vyuo vya taaluma ya juu. Hata hivyo, kwa vile wizara ina wajibu wa kuwasajili wataalamu wa afya wanaofanya kazi Zanzibar ilionelea kuna haja ya kufanya mawasiliano na taasisi hiyo.

Kwa nia njema tu, kupitia Baraza la Wauguzi na Wakunga, Wizara iliunda Kamati ndogo ambayo ilifanya mawasiliano na ziara rasmi ya ukaguzi wa chuo hicho. Baraza liliwaelekeza juu ya utaratibu na matakwa mbali mbali ya uanzishwaji wa Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya. Kwa bahati mbaya sana, taasisi hiyo haikuweza kutimiza masharti waliyoshauriwa. Ni imani yetu kwamba iwapo wangeweza kufuata taratibu na masharti waliyoelekezwa, chuo hicho kingelikuwa katika hatua nzuri ya kuruhusiwa kutoa taaluma.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumuona anaendelea na kukaidi maagizo aliyopewa na Baraza, Wizara yangu ikalazimika kuchukua hatua zifuatazo ambazo ni majibu kwa maswali aliyouliza Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Naibu Spika,

(a) Wizara yangu imechukua hatua ya kumuonya kwa barua na pia kuwatangazia wananchi kuwa chuo hicho hakitambulikani na Wizara ya Afya na wahitimu wa chuo hicho hawatasajiliwa na Baraza la Wauguzi la Zanzibar. Ninamaanisha hawataweza kufanya kazi Wizara ya Afya wala hospitali za binafsi ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Afya.

(b) Hatima ya wanafunzi hao haiko chini ya Wizara yangu kwani Wizara ya Afya ilitoa taarifa rasmi kupitia Baraza lako tukufu la awamu iliyopita kuwa chuo hicho hakitambuliwi.

(c) Kuhusu kumsaidia mwekezaji huyo, Wizara yangu iko tayari kumsaidia iwapo atafuata masharti yote aliyopewa kama nilivyoeleza hapo awali katika maelezo ya utangulizi wa suala hili ikiwemo kukaguliwa chuo kabla kuanza masomo, kuwa na walimu wenye sifa, kuongeza ukubwa wa madarasa, kuchukua wanafunzi wenye sifa na uwezo wa kujiunga, kutayarisha mtaala utakaokubaliwa na Baraza la Taifa la Taaluma *(National Council for Technical Education – NACTE)* pamoja na kupata usajili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia Baraza lako tukufu naomba kutoa wito kwa wananchi kutowapeleka vijana wao katika chuo chochote ambacho hakijapata ridhaa ya vyombo husika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali alisema kwamba wao kama wizara waliwapa masharti hawa watu wa chuo ambayo wameshindwa kuyatekeleza. Je, Mhe. Naibu Waziri, ni masharti gani hayo ambayo mliwapa na wakashindwa kuyatekeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya hatupaswi kuwapa masharti kwa sababu hatukuwasajili na hawako chini ya himaya yetu. Tulichokifanya kama nilivyoeleza hapo nilipotangulia kwenye jibu (a) kwamba tuliwasaidia, tukawaelekeza waongeze ukubwa wa madarasa, wafanye shughuli ambazo zinatakiwa kufanywa, wawe na mitaala.

Hivyo ndivyo tulivyowashauri, hatukuwapa masharti ni ushauri tuliotoa. Wakishafuata mashauri hayo watakwenda kwenye vyombo vinavyohusika watakubalika, watasajiliwa, watasomesha, tutapokea wanafunzi wao kufanya kazi katika Wizara yetu ya Afya.

Nam. 42

Ujenzi wa Daraja Maeneo ya Uzi na Unguja Ukuu

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza**:-**

Suala la uimarishwaji wa miundombinu ikiwemo barabara lina umuhimu mkubwa kwa jamii. Lakini hadi wakati huu kuna baadhi ya maeneo ya visiwa vyetu bado hali hairidhishi jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hususan akinamama. Kwa kuwa wananchi wa Uzi na Ng'ambwa hupata msaada nje ya maeneo yao inapobidi kufanya hivyo.
Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja litakalounganisha eneo la Uzi na Unguja Ukuu ili maeneo hayo yafikike kwa urahisi muda wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, wazo la ujenzi wa daraja litakalounganisha eneo la Uzi na Unguja Ukuu ni wazo la msingi na wizara yangu inalitambua hilo. Eneo ambalo lingepaswa kujengwa daraja hilo lina urefu wa kilomita mbili ambapo ujenzi wake ingelikuwa ni sawa ama unakurubiana na ule ujenzi wa daraja la Mkapa liliopo Rufiji.

Lakini zaidi daraja lile la Mkapa limepita katika maji ya baridi na daraja la uzi ambalo kama lingejengwa lingepita katika maji ya chumvi.

Ujenzi wa daraja hilo la Uzi kwa vyovyote ni dhahiri kwamba lingehitaji utaalam zaidi na gharama zingekuwa kubwa. Hivyo, wizara yangu kwa muda huu bado inaendelea kufanya utafiti na kuimarisha barabara iliyopo kwa lengo la kuimarisha na kuiboresha zaidi ili iweze kutumika kwa urahisi na kwa ufanisi zaidi kwa wananchi wa eneo husika.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo (Mhe. Salmin Awadh Salmin): Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo ndani kwa kuendelea kutupa neema yake na uhai tukiwa salama na wenye afya tele.

Aidha, nichukue nafasi hii vile vile kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi japo kidogo kutoa muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya kazi ambayo tumeifanya mara tu baada ya Kamati hii kuundwa upya.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imeundwa chini ya Kanuni ya 104 ya Kanuni za Baraza, na majukumu yake yakiwa yameainishwa kwenye Kanuni ya 108 ambayo naomba uniruhusu niyataje kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati ya mwaka uliotangulia.
b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yalivyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine alizotoa Mhe. Waziri Barazani.
c) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
d) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa na miradi ya wananchi wa Wizara husika.
e) Kuchunguza na kufuatilia mapato ya Serikali ya Wizara husika
f) Kufikiria jambo lolote litakalopelekwa kwake na Mhe Spika.
g) Kufikiria miswada ya sheria itakayokabidhiwa kwake na Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu ina Wajumbe wafuatao:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Mohamed Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa - Mjumbe
4. Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mjumbe
8. Ndg. Amour Moh'd Amour - Katibu
9. Ndg. Asha Said Mohamed - Katibu

Mhe. Naibu Spika, Niruhusu pia niwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa mashirikiano yao ambapo kwa kipindi kifupi tu tangu kuchaguliwa wameonesha uzoefu na upeo mkubwa wa kuelewa mambo mengi. Aidha, sinabudi kuwashukuru pia Makatibu wetu wa Kamati ambao wameweza kuwa msaada mkubwa na muhimu sana katika kukamilisha kazi na kuziratibu shughuli zetu ili ziende kwa wepesi na kwa ufanisi, wametushauri vyema na kwa busara mno.

Kuhusu Utekelezaji

Mhe. Naibu Spika, Katika utaratibu uliowekwa Kamati yetu ilipanga kufuatilia utekelezaji wa malengo hayo katika Wizara zifuatazo:-

i) Wizara ya Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
ii) Wizara ya Kilimo na Maliasili.
iii) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nne za kazi, mbili kwa Unguja na wiki mbili nyengine kwa Pemba. Muda huo ulikuwa mdogo kiasi cha kwamba Kamati haikuweza kupata taarifa hizo za utekelezaji kwa baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inawapongeza na kuwashukuru sana viongozi wa wizara hizo tatu wakiongozwa na Mawaziri wao, Naibu Waziri, Makatibu na Manaibu Katibu wao, Makamishna, Wakurugenzi na wafanyakazi wao wote kwa kuonesha mashirikiano ya hali ya juu kwa Kamati.

Tunawapongeza kwa juhudi zao ambazo wamekuwa wakizifanya kila leo pamoja na wakati mwengine kuzifanya katika mazingira magumu ya upungufu wa nyenzo.

Yaliyojitokeza

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nieleze kwa ufupi kabisa baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika kazi za Kamati kwa Wizara moja moja kama ifuatavyo:-

Wizara ya Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo

Wizara ya Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ina jukumu kubwa la kupanga namna ya taratibu za kukusanya mapato yetu, lakini vile vile katika suala zima la matumizi. Tunajua fika kwamba mahitaji yetu ni makubwa kuliko mapato, lakini kwa utaratibu tunajaribu kugawana kwa kadri hali inavyokuwa.

Mhe. Naibu Spika, **v**ipo vyombo vya kukusanya mapato kama Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Vyombo hivi vyote vina changamoto zinazolingana ambazo tumeziainisha kwenye ripoti yetu, lakini maeneo mawili makuu naomba niyataje kwa msisitizo nayo ni upungufu wa makusanyo, kwa sababu ya magendo ya mafuta ya magari, misamaha mingi ya kodi hasa katika maeneo ya uwekezaji, na jengine ni suala la watu kutolipa kodi vizuri, kutokana na utitiri wa vyombo vya kulipa kodi hizo. Suala la kutoa risiti kwa wafanyabiashara wa bidhaa wanazouza, nalo linachangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa mapato.

Sekta nyengine za Fedha kama vile Mabenki (PBZ na BOT) zimefanya vizuri, isipokuwa zile tafiti na ushauri mbali mbali unaohusiana na ukuzaji wa uchumi wetu, unaotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwa serikali tunashauri ufanyiwe kazi, pengine ushauri huo utasaidia kuinua uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar nalo limejitahidi sana kwenye ushindani wa biashara hiyo. Limefungua matawi yake Tanzania Bara, lakini pia limeanzisha mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ambayo pia ni sehemu ya utekelezaji wake.

Aidha, kwa upande wa Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi (ZIPA), bado ile dhana ya kuwa na huduma ya pamoja kwa wakati mfupi yaani (*One Stop Centre*) haijatimia. Washiriki kutoka taasisi mbali mbali wa mikutano ya kupitisha maombi ya miradi, hawawi wenye maamuzi ya moja kwa moja kwa niaba ya taasisi zao, na hivyo nenda rudi nenda rudi inaongeza urasimu usio na sababu.

Mhe. Naibu Spika, lengo la serikali ni kuona kwamba miradi inayoidhinishwa iwe endelevu na ilete tija kwa wananchi wetu. Lakini cha kushangaza ama

baadhi ya miradi hukwama njiani au mingine uanzaji na uendelezaji wake ni wa mashaka.

Kwa mfano, mradi wa Hoteli ya Venta Club, mradi huo sasa umekwama hautoi huduma, wenyewe hawajulikani walipo, wafanyakazi wao wamewatelekeza na wameacha madeni tele kwa wale wananchi waliokuwa wakichukua tenda mbali mbali za kutoa huduma.

Mhe. Naibu Spika, kamati inasisitiza tena kwamba juhudi za makusudi zifanyike kuhakikisha wananchi wanapata haki zao. Mmiliki atafutwe au Hoteli ifilisiwe ili madeni yalipwe. Aidha, kwa upande wa mkwamo uliopo katika Mpapindi *Resort* huko Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba, unahusiana na mgogoro wa Waekezaji, nao ni vyema serikali ikaingilia kati ili kupata ufumbuzi wa jambo hilo.

Mhe. Naibu Spika, tatizo jengine katika masuala ya uekezaji linahusiana na Kiwanda cha Sukari Mahonda. Bado kuna utata ambao uko pande zote mbili. Upande mmoja ni kwa Muekezaji kwamba hajazalisha sukari tangu alipokabidhiwa. Upande wa pili ni wa wananchi ambao wanafanya hujuma kubwa kwenye mashamba kwa kuiba miwa, kuitia moto na kulishia mifugo yao. Aidha, maeneo mengine wanayatumia kwa kilimo. Waliokaa kwenye nyumba za kiwanda nao pia hawataki kuondoka.

Mhe. Naibu Spika, malalamiko haya ni ya muda mrefu na hayajafanyiwa kazi kikamilifu. Tunaiomba serikali itoe maelezo ya uhalisi wa jambo hili na ichukue hatua ya kulitatua.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukisikitika sana juu ya uwezo wetu kiuchumi, huku tukiamini kwamba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuweza kuratibu vyema matumizi ili angalau yale mahitaji yetu muhimu yaweze kupatikana. Ni dhahiri kwamba moja ya tatizo letu kubwa la muda mrefu ni majengo ya Afisi za Serikali. Mawizara mengi yamekuwa kwenye majengo ya kurithi ambayo hayana nafasi ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba ina tatizo hili ambalo limedumu kwa muda mrefu. Mwaka juzi kamati yetu imepata changamoto hii, halkadhalika mwaka jana tatizo limejirejea na mwaka huu hadithi ndiyo hiyo hiyo. Tuna wasi wasi kwamba hadithi hii itaendelea mwakani na mtondogoo.

Mhe. Naibu Spika, **j**uhudi za kuhakikisha tatizo hili zimefanywa, lakini utekelezaji wake ndio hasara zaidi. Afisi hiyo ujenzi wake umetumia fedha nyingi tu za Serikali lakini imejengwa katika eneo ambalo ardhi yake ni ya maji

maji haiwezi kuhimili ujenzi huo. Ni eneo ambalo hata asiye mtaalamu anajua kwamba siyo muafaka kujenga. Jengo lenyewe limeanza kuanguka kabla halijaanza kutumika kabisa, na hivi sasa limewekekewa miundi ya miti eti kulizuia. Kamati imeshindwa kuelewa kama kweli ujenzi ule ulifata taratibu zote ikiwemo pia ushauri wa kitaalamu.

Mhe. Naibu Spika, Cha ajabu ni kwamba hata ushiriki wa anaetaka kutumia jingo hilo, yaani Afisa Mdhamini hakushirikishwa na hakuwa na majibu yoyote juu ya hilo, kwani taratibu zote zimefanywa Unguja peke yake. Lake yeye ni kujulishwa kwa mjenzi ili aweze kumpa misaada midogo midogo pindi akiihitaji.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu hakuridhishwa hata kidogo na tukio hilo na bado inahitaji maelezo ya ziada kutoka kwa Mhe. Waziri, juu ya hatua gani inayochukuliwa kwa waliyohusika na ubadhirifu huo, lakini pia hii Afisi ya Pemba ni lini itaondokana na tatizo hilo.

Wizara ya Kilimo na Maliasili

Mhe. Naibu Spika, msemo wetu kama nchi kwa kilimo kitaendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wetu. Pamoja na juhudi nyingi za kuwa na miradi mbali mbali ya kusaidia uwezeshwaji wa kufikia malengo katika hili, lakini pia kuwa na chuo cha kutoa elimu hii ya kilimo, malengo hasa bado hatujayafikia, na serikali inatarajia sana kuyafikia malengo haya kwa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji, ambapo mpango mkuu umewekwa kwa madhumuni hayo.

Mhe. Naibu Spika, ni hakika kwamba mafanikio haya hayatafikiwa kwa sababu tu ya juhudi za serikali pekee, lakini ni lazima mchango wa wakulima wenyewe uwe ni mkubwa. Inasikitisha kusema kwamba maeneo mengi yaliyotayarishwa kwa kilimo hiki, baadhi ya wakulima hawapendi kujitolea katika utayarishaji wa miundo mbinu ya kusambaza maji katika mabonde yao. Wangependa kila kitu kifanywe na serikali.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwenye eneo hili, ni mashirikiano madogo baina ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na wizara inayohusiana na Maji. Kuna kila dalili zinazoonesha kwamba hakuna kuaminiana baina yao katika kazi za uchimbaji wa visima au kuna mvutano baina yao.

Mhe. Naibu Spika, katika sura hii hii ndio inayosababisha upungufu wa maji kwenye vituo vya kuoteshea na kuimarisha vitalu vya miche na maeneo ya kufanyia utafiti wa mbegu kama vile Kituo cha Matangatuani.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la wizara hii ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira mazuri ya wafanyabiashara na wateja wao. Mazingira hayo yawe katika kila hali ikiwa ni ubora wa bidhaa, bei muafaka na upatikanaji wake kwa muda wote.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu bado inahisi kwamba pamoja na juhudi za serikali kujenga mazingira hayo kwa kutunga sheria na sera mbali mbali, ufanisi haujafikiwa kabisa. Tatizo la bidhaa zisizo na viwango bado lipo ikiwa ni bidhaa za kula na za matumizi mengine kama vile za nishati. Bei nazo zimekuwa kikwazo kikubwa. Chakula kipo bei ya juu tofauti na matarajio ya wananchi wetu walio wengi.

Mhe. Naibu Spika, Ni kweli kuna biashara huru, lakini uhuru huo ni lazima uwe na mipaka yake. Si kwa sababu hiyo tu ndio iifanye serikali isiingilie masuala ya kupanga bei, kwa ile dhana ya kwamba bei zitapangwa na soko lenyewe tukisahau kwamba wafanyabiashara wanayo mahusiano yao, ambayo yanaweza kabisa yakajenga umoja ambao utaifanya ile dhana ya bei kupangwa na soko isifanye kazi.

Kwa vile, serikali ndio inayowapangia mazingira mazuri ya kufanya biashara, ikiwemo nafuu ya kodi, basi kamati inashauri wizara iwe pamoja na wafanyabiashara, ili bei za bidhaa ziwe ndio bei halisi na zisiwe za kuwapa faida kubwa wafanyabiashara hao.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kwa upande wa bidhaa za Nishati kama vile mafuta ya kuendeshea mashine (Disel, Petroli, Mafuta ya taa n,k) nayo yanahitaji kuangaliwa sana ubora na ujazo wake kupitia vipimo vinavyotumika. Maeneo yanamowekwa pamoja na hata magari ya kuyabebea.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) kwa upande wa Kamati kubwa ambalo inalisisitiza ni kwamba magendo ya Karafuu yanalimaliza. Kumekuwa na wimbi kubwa la magendo ya karafuu ambayo hayatoi nafasi hata kidogo kwa shirika kuweza kununua kwa wingi karafuu, hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Hili ni sisi viongozi ndio wa kufunga mkaja kuweza kuliokoa. Si la kuwaachia askari wa KMKM peke yao.

Mwisho

Mhe. Naibu Spika, Maelezo mengi tumeyatoa kwenye ripoti yetu na mengi mengine tumeelekezana na watendaji pamoja na Viongozi wakati tulipokutana. Tunawapongeza kwa mara nyengine tena kwa mashirikiano na uvumilivu wao

wakati wa kazi zetu. Aidha, ni matarajio yetu kwamba watajitahidi kutekeleza majukumu yao ili malengo yaliyokusudiwa yafikiwe.
Mhe. Naibu Spika, tunaupongeza uongozi wa Afisi yako ya Baraza la Wawakilishi kwa uratibu wao mzuri wa kazi hizi za kamati zetu. Hata hivyo, bado muda unaopangiwa kamati hizo ni mdogo mno kulinganisha na shughuli zilizopangwa. Tunaomba tujitahidi muda uwe angalau wiki tatu badala ya mbili za sasa kwa awamu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu kwa utulivu na usikivu wao, kwa muda wote ambao nimekuwa nikitoa muhtasari wa taarifa hii ya ripoti hii, nikitarajia kwamba watatoa michango yao ya busara katika kuona kwamba serikali inatimiza wajibu wake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

TAARIFA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimwa Wajumbe, kabla hatujaanza majadiliano, nina tangazo moja na maelezo kidogo. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya PAC kaniomba niwatangazie wajumbe wake wakakutane sasa hivi chumba nambari 2, kuna mambo muhimu. Kwa hivyo, kama bado wamo ndani humu wajumbe wa kamati ya PAC basi wanaombwa waende chumba nambari 2.

Halafu jengine ni utaratibu, nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na wizara tatu, ambao tayari taarifa imesomwa wakae ili waweze kusikiliza hoja zile zilizotolewa na baadae watakuja kutoa maelezo kadiri wajumbe watakavyotaka kuhoji. Mwisho nitamwita mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, kuja kufanya majumuisho. Kwa hivyo, sasa natoa nafasi kwa mjumbe yeyote aliyekuwa tayari kuichangia kamati hii basi namkaribisha, sina jina hata moja huku juu. Kwa hivyo, mjumbe anayetaka kuchangia alete jina lake huku juu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba niokowe jahazi kwa kuwa mtu wa mwanzo. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mimi nianze kwanza kwa kuipongeza kamati na mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa ripoti hii waliyoleta ambayo imetaja mambo mengi sana ambayo yanahusika na wizara hizi tatu ambazo wanazisimamia.

Mhe. Naibu Spika, ripoti ni ya kina na ina takwimu nyingi ambazo zinaweza zikasaidia sana wizara zinazohusika na Baraza. Hii hasa Mhe. Naibu Spika,

ndio kazi moja muhimu sana za Baraza hili ni hii ya kusimamia utendaji wa shughuli za serikali kwa kupitia kamati hizi za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaomba kidogo kusaidiwa maelezo na pengine Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati atakapokuja kutoa majibu mbali mbali, basi pale kwenye ukurasa wa mwanzo wa ripoti tuliyopewa, katika kuizungumzia Bodi ya Mapato Zanzibar yaani (ZRB) zimetajwa sekta kadhaa ambazo zimesababisha ukusanyaji wa mapato ya ndani yanayosimamiwa na ZRB kushuka. Mambo yaliyotajwa pale ni pamoja na;

1. Kutokufanya vizuri kwa kianzio cha mapato ya wizara,
2. Kupungua kwa idadi ya watalii wanaolipa VISA hapa nchini, baada ya watalii wengi kulipia VISA zao kwenye Balozi za nchi za nje Tanzania; na
3. Kukosekana kwa mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Naibu Spika, ninaomba masuala haya tupewe maelezi kidogo. Nianze na hili suala la kwanza, kama nimeelewa vizuri nategemea imekusudiwa kwamba ni mapato ya jumla ya wizara na sio labda wizara hizi ambazo ziko chini ya kamati hii au Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inayohusika hapa.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba kusaidiwa kwa mfano, ziko taarifa kwamba kuna hatua nzuri ambazo tumepiga katika kukusanya mapato, lakini zimeanza kuathirika kutokana na kurejea katika mtindo wa zamani.

Moja katika maeneo ambayo tunayasikia yakitajwa ningeomba nikapatiwa maelezo baadae kwa mfano, Shirika la Umeme. Shirika hili lilikuwa linachangia vizuri mapato ya serikali, kwa sababu serikali ilikuwa imeanzisha utaratibu mzuri wa kulipa gharama zake za kutumia umeme. Lakini tuna taarifa kwamba kwa muda sasa ule utaratibu mzuri uliokuwa umeanzishwa na serikali wa kulipa kila mwezi ada ya malipo ya umeme umesita na kwa hivyo kupelekea kuliathiri shirika hili. Sasa pengine kwa sababu linaathirika hata ule mchango wake wa mapato katika nchi pia unapungua. Sasa sijui kama hii ni sehemu ya hayo mambo yanayosemwa ya kutokufanya vizuri kwa vyanzo vya mapato ya wizara ambayo imetajwa hapa. Kama ni hivyo, kuna maeneo gani mengine wizara zimekuwa zinasua sua kaatika kukusanya mapato yake, ningeomba kupatiwa ufafanuzi, waziri anayeshughulika na masuala ya fedha au mwenyekiti wa kamati atakapokuja kufanya majumuisho basi atusaidie vizuri zaidi.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, lililotajwa hapa ni hili la kupungua kwa mapato kutokana na watalii kutolipa VISA hapa wanapoingia na badala yake kulipia katika Afisi za Balozi za Tanzania ziliopo nje ya nchi. Suala hili limeulizwa mara kadhaa katika Baraza hapa na majibu yamekuwa yakitolewa. Miongoni mwa majibu yaliyokuwa yakitolewa ni kwamba baadae kunafanywa utaratibu kwa wale ambao wanalipia VISA zao katika Afisi za Kibalozi Tanzania ziliokuwepo nje, ili kurejesha mapato yale yanayohusu Zanzibar basi yarudi Zanzibar. Kwa maelezo haya Mhe. Naibu Spika, ni kwamba ikiwa kuna utaratibu kama huo, basi mapato yasingepungua, kwa sababu kinachomalizika ni ukusanyaji tu badala ya kukusanywa uwanja wa ndege au bandarini Zanzibar, yatakuwa yanakusanywa katika Afisi za Kibalozi, lakini kama zinarejeshwa maana yake mapato yatakuwa ni yale yale kulingana na idadi ya watalii walioingia.

Sasa kama leo ZRB inaripoti kwa kamati kwamba mapato yanapungua kutokana na suala hili, maana yake kuna tatizo katika hayo marejesho ya fedha hizi zinazotokana na VISA huko nje ya nchi kwa kupitia afisi zetu za kibalozi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba na hili nalo tupatiwe maelezo yake.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, pametajwa suala la kukosekana kwa mapato kutokana na kushindwa kukusanya mapato kutokana na uvuvi wa bahari kuu. Mhe. Naibu Spika, hili ni suala ambalo linaonekana linaathiri sehemu kubwa ya nchi yetu, lakini pia kwa upande wa Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Waziri wa nchi anayeshughulikia masuala ya fedha, atakumbuka kwamba suala hili limekuwa likiripotiwa sana katika Bunge, juu ya upotevu mkubwa wa mapato kutokana na kushindwa kusimamia kulinda bahari yetu kuu. Sasa najua kumeundwa mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu ya Jamhuri ya Muungano na baada ya mvutano wa muda mrefu juu ya vipi Zanzibar itanufaika kuwepo utaratibu wa kuweza kugawana mapato yanayoingia kwenye mamlaka hii. Mamlaka hii ndio iliyopewa dhamana ya kusimamia masuala yote yanayohusika na uvuvi wa bahari kuu, halafu kwenye fomula iliyowekwa kama nakumbuka vizuri ilikuwa asilimia 60 kwa upande wa Tanzania Bara kwa Serikali ya Muungano na asilimia 40 kwa upande wa Zanzibar.

Kwa hivyo, leo ZRB inavyoripoti kwamba tunashindwa kukusanya. Je, hii inaeleza kufeli au kushindwa kazi kwa mamlaka hii ya mapato au hii fomula ambayo imewekwa ya mgawanyo wa mapato imebakia katika vitabu tu kama kawaida yetu, kuorodhesha kwamba kasoro za Muungano zimepungu au kero za Muungano zimepungua, lakini bado inapokuja kunufaika kwa Zanzibar kivitendo halifanyiki. Ndio nilikuwa naomba nipatiwe maelezo yake.

Halafu Mhe. Naibu Spika, katika vyombo hivi, hata kwenye ripoti hii kuna ZRB na kuna TRA. Kwa muda mrefu kulikuwa na maoni kwenye Baraza hili hili katika mikutano ya Baraza lililopita na Mabaraza yaliyopita, kwamba pengine katika kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kuna haja ya kuwa na mkusanyaji mmoja tu wa mapato hapa Zanzibar, kati ya ZRB na TRA wa kusimamia mapato yote. Suala hili kwa muda mrefu limenyamazwa, sijui kamati ilikuwa na mtazamo gani kuhusu suala hili nap engine labda waziri pia anaweza kutusaidia kwamba ni lipi linaweza kuleta ufanisi zaidi Zanzibar, kuwa na mamlaka mbili zinazokusanya mapato TRA na Bodi ya Mapato (ZRB) ama kuwa na mamlaka moja ambayo itakusanya mapato yote kwa Zanzibar na pia baadae kuyagawa kwa mujibu wa utaratibu ulivyo wa mapato yenyewe.

Jengine Mhe. Naibu Spika, lipo katika suala la ZSSF. Mhe. Naibu Spika, mifuko kama hii duniani siku hizi, inasaidia sana kupunguza baadhi ya matatizo katika nchi kwa kuekeza katika yale maeneo ambayo yanahitaji uwekezaji na pengine labda Serikali Kuu inashindwa au hakujajitokeza wawekezaji wa nje. Nchi kama Malaysia imenufaika sana na mifuko kama hii. Kwa mfano, kuwekeza katika suala zima la uzalishaji wa umeme. Hata hivi sasa kwa upande wa pili Bara kunazungumzwa juu ya haja ya mifuko kama hii hasa kupitia Kamati ya Bunge inayohusika na Mashirika ya Umma, juu ya kuwekeza katika suala hili.

Sasa nilikuwa nauliza Zanzibar pia tunakabiliwa na tatizo hili, mpaka sasa tumeona ZSSF tumeona ikiekeza katika ujenzi mara nyingi. Inajenga majumba inakodisha na inapata mapato bila shaka. Lakini zaidi uwekezaji huo haionekana kwamba kuna haja ya kuangalia uwekezaji mkubwa zaidi ambao utainufaisha nchi na kusaidia kuinua uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, sisi Zanzibar tunatumia umeme, suala hili nililizungumza tulipokuwa tukichangia mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Tunatumia umeme kutoka kwa ndugu zetu wa Bara. Lakini kila siku zinavyokwenda uzalishaji wa umeme Bara unapungua, wao wenyewe hauwatoshelezi seuze sisi. Serikali imefanya kazi nzuri ya kununua majenereta. Mimi nataka niipongeze sana serikali sana kwa majenereta ya akiba yanayozalisha angalau zaidi kidogo kuliko nusu ya mahitaji yetu. Sasa pengine kuna haja ya kuangalia kwa upana zaidi suala la mifuko kama hii kuekeza katika miradi kama hii mikubwa ambayo itasaidi kupunguza matatizo yetu, lakini pia itasaidia kuekeza katika sekta ambazo zitakuza uchumi kwa maana pana zaidi, sijui kamati imeliona hili na wizara husika inalitazamaje kuusaidia mfuko huu wa hifadhi ya jamii iweze kuangalia maeneo kama haya.

Nimetoa mfano mmoja tu wa umeme, lakini pengine kuna maeneo mengine ambayo tunashindwa kupata wawekezaji wakubwa kutoka nje, au pengine sio

busara kuwa na wawekezaji wakubwa kutoka nje, tumeona masuala ya *DOWAS* yanavyowasumbua mpala leo Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Lakini pengine kuna haja ya sisi wenyewe kuekeza katika maeneo hayo. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kusaidiwa ni kwa kiasi gani mifuko kama hii inaweza kututoa hapa tulipo.

Mhe. Naibu Spika, pia limezungumzwa suala la ukosefu wa afisi hasa kwa upande wa Pemba. Suala hili Mhe. Naibu Spika, pia tunaweza kuliona katika ripoti za kamati nyengine, inaonekana ni moja ya miongoni mwa matatizo makubwa sana kwa upande wa Kisiwa cha Pemba.

Kwa kweli tunakitupa kisiwa hiki katika masuala mazima ya kuyapatia huduma za kuwa na afisi zenye hadhi za kuitwa afisi za serikali, kwa sababu hili pengine halisaidii hata kukuza shughuli zenyewe za uchumi kwa upande wa Kisiwa cha Pemba.

Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii ya kamati ya kusema kwamba kuna haja ya wizara zinazohusika na kwa hapa imetajwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo juu ya kujenga au kutafuta jengo jengine la kununua ambalo lenye hadhi na litasaidia. Kwa mfano, ukipita pale Chakechake na ukiambia hii ndio Afisi inayoshughulikia Masuala ya Fedha kwa upande wa Pemba, kwa kweli Mhe. Naibu Spika inasikitisha sana.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo limetajwa hapa ni kuhusu hawa wawekezaji kama vile wanaowekeza kwenye mahoteli ya kitalii. Kwa kweli limetajwa suala la *Venta Club* na jambo hili limeleta manung'uniko au mazungumzo makubwa sana katika nchi yetu juu ya ukweli wawekezaji tunakuwa nao.

Nafikiri hili kuna haja ya Mamlaka inayohusika *ZIPA* kuangalia kwa undani wawekezaji kama wanaokuja, kwa sababu kama ilivyozungumzwa kwamba tulikuwa tukiona kupitia vyombo vya habari TVZ wakati ule, wale wananchi waliokuwa wakitoa huduma kwa hoteli hii wamepeleka huduma na mapaka leo hawakulipwa na hatimaye tunaambiwa muekezaji huyu haonekani.

Kwa hivyo, suala hili na mimi nataka kulitilia nguvu kusema kwamba tuna haja ya kuwa na upembuzi mkubwa zaidi wa nani anayekuja kuwekeza katika nchi yetu, ili baadaye wasijekuathiri wananchi wetu na pia kuiacha nchi yetu katika madeni badala ya kunufaika kwenye uwekezaji ambao wanaokuja kuufanya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutoa mchango wangu mfupi kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ambayo imetoa ripoti yake na inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwa lengo la kusaidia ufanisi wa ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niunge na wenzangu kwa kumpongeza Mhe. Mwenyekiti pamoja na kamati yake, kwa jinsi walivyoitayarisha na kuitoa ripoti hii, ripoti ambayo kwa kweli imeeleza wazi wazi juu ya changamoto ambazo serikali yetu inakabiliana nazo.

Nianze na mchango wangu kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato, ambapo ripoti hii imeeleza kwamba mapato yameshuka na kamati imeeleza kuwa mapato yameshuka kutokana na sababu tatu ambazo zimeandikwa.

Lakini kamati imeshindwa kutueleza kwa kiasi gani mapato hayo yamepungua kutokana na mianya ya uvujaji wa mapato. Kwa kweli wametueleza tu kwamba kuna sababu ambazo wamechangia. Je, tunaomba kujua hakuna mianya ya uvujaji wa mapato haya au ni sababu zile za utendaji zaidi.

Nafikiri wangetueleza kamati wameridhika vipi na jinsi mapato haya yanavyokusanywa yanahifadhika. Je, hakuna mwanya wa uvujaji wa mapato hayo. Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri au Mwenyekiti wa Kamati anaweza kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, sababu nyengine ambayo inaonekana wazi wazi ni kuhusu upungufu wa vyanzo vya mapato. Suala hili nadhani ni jukumu la serikali kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato.

Katika hili Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atusaidie kujua kwamba kuna mawakala wa usafirishaji wa vifurushi na wako wengi katika dunia, Tanzania pamoja na Zanzibar wameingia katika biashara hii ya usafirishaji wa vifurushi. Kwa mfano, kuna *DHL* wanasafirisha vifurushi kutoka nje ya nchi hadi Tanzania, wale wafanyabiashara na wanachangia mapato ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, juzi tuliangalia kwenye mtandao tukaona kwamba kifurushi kimetoka Dubai hadi Tanzania kwa siku moja, yaani kutoka saa 2 za asubuhi hadi saa 11 jioni tayari kifurushi kimefika Dar-es-Salaam, lakini mzigo huo kutoka Dar-es-Salaam hadi Zanzibar umechukua siku nne.

Kwa hiyo, kuna urasimu upo mkubwa, yaani kutoka Dubai hadi Dar-es-Salaam, lakini kutoka Dar-es-Salaam hadi Zanzibar ni siku nne na mzigo ule ulikusudiwa kufika Zanzibar, kwa kiasi gani kunakuwa na *delaying* na kwa kiasi gani mapato yanapoteka kutoka na urasimu uliopo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe tu, kwa nini mawakala hawa wasilete mizigo yao moja kwa moja Zanzibar na lazima mizigo ile ipitie Dar-es-Salaam, jambo ambalo pale kuna mapato yanapotea na wafanyabishara wetu wanakuwa na usufumbu wa upatikanaji mizigo yao kwa haraka.

Suala jengine ambalo ripoti imelizungumza ni kuhusu ujenzi wa afisi za serikali. Kwa hivyo, na mimi nizungumzie moja kwa moja kuhusu ujenzi Afisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba. Mhe. Naibu Spika, nadhani serikali iwe wazi na ituambie kwa sababu hatuwezi kujenga jengo kama lile kwa gharama kubwa za fedha za umma na baadaye serikali ikakaa kimya, kwa kweli jengo haliekewi miega kama mgomba wa ndizi.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika ni lazima serikali itueleze ni kwa kiasi gani jengo lile limefeli kuwa ni jengo madhubuti na wala wasisite kutueleza kuwa kwa kiasi gani serikali imeingia hasara kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, jengo lile inaonesha wazi kwamba serikali pamoja na mkandarasi wameshindwa kuwajengea Wazanzibari jengo la Afisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba, kwa namna yoyote jengo lile tunaamini halitofaa tena. Kwa hiyo, kiasi gani serikali imeingia hasara na hatua gani serikali itachukua, ili Wazanzibari wapate kulinda fedha ambazo zimepotea kwa mradi ule ambao haukuwa na umakini kwa watendaji wa serikali.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Naibu Spika suala hili atuekee wazi ili tuweze kulijua.

Vile vile suala jengine ambalo kamati hii imelizungumza kuhusu utendaji mzuri wa Benki yetu ya *PBZ* hasa kusambaza vituo vya kutolea fedha kwa mitambo ya *ATM*. Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza *PBZ* kwa jinsi walivyoeneza huduma hii kwa Unguja na Pemba, kwa kweli wamerahisisha udumu na vikwazo vya upatikanaji wa fedha kwa wananchi ambao wanahitaji fedha ndogo ndogo. *(Makofi)*

Lakini kuna changamoto ambayo nimeiona kwamba benki bado kupitia Idara yake ya Masoko haijakuwa makini katika kutangaza biashara za kibenki hapa Zanzibar. Kwa mfano, tukiangalia kwenye soko la mabenki wateja wengi wanahamia katika mabenki ambayo matawi yake ni Zanzibar na zaidi ya Muungano, kama vile *NMB* na mabenki mengine.

Suala hili ni kutokana na kwamba Benki yetu ya *PBZ* haijakuwa na Idara makini ya Masoko ambayo ingetangaza huduma za kibenki hapa Zanzibar. Kwa mfano, tukiangalia Zanzibar nzima kuna bango moja tu ambalo linatanga matangazo ya Benki yetu ya *PBZ* katika eneo la Mombasa kwa Mchina. Kwa hiyo, bango moja tu Zanzibar nzima ndilo ambalo linalotoa taarifa za huduma za *ATM* kwa benki yetu ya Zanzibar, tukiangalia mabenki mengine wanayo matangazo kila sehemu.

Mhe. Naibu Spika, nadhani Idara ya Masoko ya Benki ya *PBZ* ingejipanga kutangaza huduma hizi kwa ajili ya wananchi wetu mijini na vijijini kwa lengo la kutoa huduma nzuri pamoja na kuongeza mapato.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kamati imeeleza ripoti hii kwa uwazi na lazima serikali iwajibike kutoa ufafanuzi, ili wananchi wa Zanzibar wapate taarifa muhimu ambazo kamati hii wamezileta kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kukaa.

Mhe. Mahmuod Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nizidi kuchangia katika Ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Kwa kweli kazi kubwa tumeshaifa katika kamati na ninaikubali kamati hii moja kwa moja kwamba haya maelekezo yote ni sahihi na ndio hasa tuliyokubaliana pamoja na kuyaona, lakini zaidi ninapenda kuongeza nyama kidogo tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa maoni yangu nahisi kwamba jina la kamati kidogo lina matatizo kwa mara nyengine tena naweza kusema. Kwa kweli jina la kamati yetu ni Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo nadhani katika utendaji
kamati hii itakuwa tunampunguzia baadhi ya nguvu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kufanikisha suala zima la uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ili nchi iendelee duniani inahitaji kuwa na uchumi endelevu, lakini kwa muundo ambao tunauona na nguvu ambazo anapewa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika harakati na utaratibu wa kuweza kufahamu taarifa za kina za uchumi nahisi zina mapungufu kidogo.

Kwa kweli ili tuweze kwenda vizuri katika nchi tunahitaji kukusanya mapato pamoja na kuweza kufanya matumizi. Sasa kuna vyanzo vya mapato ambavyo Katibu Mkuu anahusiana navyo moja kwa moja, yaani anavijua na kuvielewa

pamoja na uwezo mzuri wa kuweza kuvifanyiakazi. Lakini kuna baadhi ya maeneo Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hana uwezo hayo, nina wasiwasi hata zile takwimu sahihi za uchumi wa nchi itakuwa si endelevu kutokana na utaratibu ambao nimeuona upo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Kiwanda cha Mahonda pamoja na *Venta Club*. Kwa kweli maeneo haya Mhe. Naibu Spika, tumeyatembelea na tumeona na baadhi ya wahusika na tumefanya mahojiano na wao, tumeangalia baadhi ya nyaraka ambazo zipo.

Kwa hivyo, kwa uoni wangu nahisi hususan katika shamba la Mahonda pamoja na maelekezo mazuri ambayo muda mfupi yametolewa na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nadhani ipo haja ya kufanya *review* kuhusiana na ule mkataba ambao upo. Mhe. Naibu Spika, lakini zaidi Mwanasheria Mkuu suala hili aliangalie kwa makini zaidi, nafikiri kuna matatizo ya kisheria kwenye Mkataba wa Mahonda pamoja na ule wa *Venta Club*.

Suala jengine ni kuhusu viwanda. Kwa kweli wawekezaji wengi wamekuwa wakilalamika kuhusiana na gharama kubwa za ulipaji wa umeme katika viwanda vyao hususan katika maeneo ya Amani. Mhe. Naibu Spika, wawekezaji hawa wanasema kwamba Zanzibar kwa sasa malipo wanayolipa katika umeme ni tofauti hata na Bara. Kwa hivyo, tumefanya utafiti na tumegundua kwamba hilo lina ukweli fulani ndani yake.

Kutokana na hali hiyo, naziomba wizara zinazohusika na masuala haya kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kukaa pamoja na hawa wawekezaji, ili kuweza kutafuta njia muafaka yakuweza kulitatua tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni kuhusu suala zima la ushukaji wa mapato kwa *TRA*. Kwa kweli pamoja na juhudi zinazofanywa na ndugu zetu wa *TRA* Zanzibar pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa na wafanyabiashara ambao wanaleta mizigo yao kupitia bandari zetu za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuchukua nafasi hii kuelezea tena wananchi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote waliopo katika Baraza lako tukufu hili, kwamba bado usumbufu wa kuhaulisha mizigo kutoka eneo moja la Muungano kwenda jengine ni tatizo. *(Makofi)*

Kwa kweli tatizo hili kwa bahati mbaya halipo kisheria. Mhe. Niabu Spika, tunaomba mamlaka husika kuchukua hatua za dharura, ili tuhakikishe tunafikia *target* ya malengo yetu katika kutayarisha Bajeti yetu ya Mwaka 2011/2012 kama ambavyo itakuwa tumejipangia.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi kwa ajili ya kutoa mchango wangu mdogo kutokana na Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Kwanza naipongeza sana kamati hii kwa kazi yao nzuri waliyoifanya pamoja na michango yao waliyoitoa katika kufanikisha shughuli nzima za wizara yenyewe, kuhusiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa upande wa wizara nyengine zilizobaki nataka nichangie jambo la kwanza kuhusiana na mikataba ya ujenzi inayofikiwa na mawizara.

Kwa kweli wizara nyingi zinaingia katika mikataba ya ujenzi, lakini baadhi ya mikataba inakuwa inaleta matatizo. Kwa hivyo, labda kwa sababu Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio inayotoa fedha, basi ingeliweka utatatibu maalum wa kuhakikisha kwamba fedha zilizotolewa zinatumika vizuri na wala sio vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pale Tibirinzi Chakechake linasikitisha. Kwa kweli kama walivyosema wenzangu tunaomba wizara itoe msimamo wao halisi hivi sasa, kwa sababu mara nyingi ilikuwa ikizungumzwa kwamba tutamwita tena Mshauri Mwelekezi tuweze kupata ufafanuzi wake.

Kwa hivyo, nadhani kwa jengo lilivyofikia kwa mara nyengine naweza kusema kwamba, Mshauri Mwelekezi atazidi kutoa pamoja na kuongeza gharama, ili jengo limebaki pale.

Mhe. Naibu Spika, tunaiomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo itupe kauli rasmi kuhusiana na mambo matatu. Kwanza ni nani aliyesababisha kasoro ile hata ikatokezea jengo kufeli, pili gharama iliyopatikana, tatu maamuzi rasmi ya serikali yako vipi na nani atakayebeba jukumu lile. *(Makofi)*

Suala jengine ni kuhusiana na mishahara ya Zanzibar pamoja na kwamba niliuliza swali, lakini Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio yenye vyanzo vya fedha. Mhe. Naibu Spika, tungependa kuchangia kwamba hali ya uchumi wa Zanzibar na pato la taifa ni dogo sana.

Kwa hivyo, tunaiomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, ikatueleza ni vipi wamepanga mipango ya

kuongeza pato la taifa la Zanzibar, ili baadaye lije lichangie katika kumuwezesha mwananchi mmoja mmoja.

Kwa kweli kutegemea kukusanya kodi tu pamoja na mianya iliopo pamoja na mambo mengine. Lakini kutegemea kukusanya kodi peke yake hakutoshi, kwa sababu Zanzibar ni nchi ndogo sana na kodi zinakusanywa za aina nyingi, nyengine zikiwa katika maneno ndani ya mabano, michango mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nadhani ikiwa hapakuelezwa halafu ukamwambia mwananchi achangie kujenga skuli, basi hiyo ni aina ya kodi, kwa sababu hukueleza katika sera yako kwamba katika ujenzi wa skuli mwananchi anatarajiwa atoe kiwango fulani. Kwa hivyo, wananchi wamebebeshwa kodi nyingi.

Sasa tunaiomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango kupitia kwako Mhe. Naibu Spika itueleze ili kukuza pato la taifa la Zanzibar, Wizara ya Fedha ndio iliyokabidhiwa majukumu haya, imejiandaa kiasi gani na sisi tuweze kupata matumaini kuwa baada ya miaka au kipindi fulani tutakuwa na uwezo wa kuendesha maisha yetu kwa uzuri.

Mhe. Niabu Spika, suala la tatu katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni kuhusu *Joint Finance Committee (JFC)*. Kwa kweli kila siku majibu ni yale ripoti imeshatolewa na iko serikalini. Lakini wataalamu hao ndio wanaotuambia kwamba moja katika mambo ambayo yangeiwezesha Zanzibar kupata mapato yake ya kihalali ni kukamilika kwa mpango ule uliotajwa katika *JFC*.

Sasa ikiwa tokea mwaka 2006 ilipoanza kazi, kwa sababu sheria ile ilipitishwa mwaka 2003 na *JFC* ilitoa ripoti yake ya mwanzo mwaka 2006 mpaka leo 2011. Kwa kweli ni jambo ambalo hivi sasa imefika wakati tuseme kwamba Ripoti ya *JFC* ndio hii na moja, mbili, tatu tayari yameshaanza kutekelezwa na bado nne, tano, sita kwa sababu fulani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni moja katika sehemu nzito ya kututafutia vyanzo vyengine vya mapato, tunataka kujua *Policy* ya Serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha ya kujiunga na Jumuiya ile ya Kiislamu ya *OIC*. *(Makofi)*

Nadhani itakumbukwa katika Baraza hili Mhe. Naibu Spika, kwamba nilitoa mchango mimi kupitia kazi za kamati au bajeti nimesahau kidogo. Kwa kweli yupo mtaalamu mmoja mkubwa sana wa Saudia ambaye yeye ni Rais wa. *Chamber of Commerce* ya Saudia, pia ni Rais wa *Chamber of Middle East*, yaani *Emirate*. Kwa hivyo, alikuwa akitoa mchango wake kuhusu namna gani

wanasaidia nchi changa kujiendesha kupitia hizi *Chamber of Commerce*, lakini kupitia Jumuiya ya *OIC*.

Mhe. Naibu Spika, Mozambique na Uganda nchi hizi ni wajumbe wa *OIC* na sisi tulijiunga na tuliambiwa tujitoe. Kutokana na hali hiyo, nadhani serikali itupe msimamo wake kwa ajili ya kufaidika kiuchumi katika Jumuiya ya *OIC*, kwa sababu tusiseme tunajitoa tu kwani wenzetu walituambia watajiunga wao kwa Tanzania nzima, lakini huu ni mwaka wa 16 bado hatujajiunga. Sasa sisi tunakula makombora na wenzetu wanatutizama macho. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nadhani serikali itoe msimamo hasa kwamba tutajiunga au vipi na hiyo *OIC* kwa ajili ya kufaidika na sisi. Mhe. Naibu Spika, ikiwa ni kwa sababu ya Uislamu Mozambique na Uganda hazina hata *population* kubwa ya Waislamu na wao wameingia. Kwa mfano, Uganda wamejengewa Chuo katika eneo la Mbale.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi yangu nimeshuhudia Rais wa *OIC* anahutubia Uganda na kuaambia tayarisheni ekari 300 za ziada kwa ajili ya kukitanua chuo kile. Sasa leo tunasema hapa *SUZA* sijui kitu gani, lakini jumuiya hizi hatuzishughulikii.

Suala la Wizara ya Kilimo na Maliasili nasema kwamba bado Karakana za Matrekta hazijakuwa *serious*. Mhe. Naibu Spika, ni sehemu nzuri ambazo ni muhimu sana na wala sio kwa kutoa ajira kwa vijana wetu, isipokuwa ni kwa kukibadilisha hata kilimo chetu, kwa sababu hatuwezi kutegemea kwamba hatuna karakana za matrekta na matrekta yatakwenda kwenye gereji za binafsi kwa ajili ya kutengenezwa na wala haiwezekani lazima tuwe na karakana yetu.

Kwa hivyo, ili kuimarisha uhakika wa chakula pamoja na lishe basi jambo moja linalohitajika ni kuzienzi pamoja na kuziweka katika hali nzuri karakana zetu za matrekta zilizopo moja Unguja na nyengine Pemba.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine bado hatujaona juhudi ya ukusanyaji wa maji ya mvua, yaani bado umwagiliaji wetu tunaekeleza katika uchimbaji wa visima. Sasa katika uchimbaji huo wa visima na watu wanategemea maji kwa ajili ya matumizi yao mbali mbali, lakini juhudi ya ukusanyaji wa maji ya mvua bado hatujaiona.

Kwa hivyo, tunaiomba sana wizara kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, iweze kufanya juhudi ya kuona kwamba hususan katika maeneo ya Micheweni kama vile *East Coast* kule ambapo baadaye mvua ni ndogo hata zile za Vuli.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri kwa kuanzia tunaweza kuanzia zile sehemu za maweni na kuendelea sehemu nyengine. Lakini suala hili bado halijaonekana tokea lilipotajwa, kwa sababu wataalamu wa kilimo wanasema kuna ukusanyaji au umwagiliaji maji wa aina mbili, yaani umwagiliaji maji kutoka chini ya ardhi na yale yaliyokusanywa kutokana na mvua.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Naibu Spika, kama jana ulitembelea zile Taasisi za Kiraia kuna kazi kubwa za kufanya kwa ajili ya kuweza kujiendesha kibiashara, kwa sababu hatuna tunachozalisha.

Sasa labda ni *create* jambo moja ambalo tulilipata pale Bandarini, ambalo moja kwa moja litahusiana na uzalishaji wetu ndani ya nchi. Kwa mfano, kontena inaposhuka Dar-es-Salaam na ikapakuliwa mzigo wake pale Dar-es-Salaam wakati mwingi inakuwa na mzigo mwengine wa kupakiliwa na meli inalichukua kontena lile na mzigo ikiirudishe huko katika nchi yengine inakokwenda.

Lakini kontena inaposhuka Zanzibar inaondosha bidhaa yote na inabaki pale tupu kurudishwa inakotoka. Kwa hivyo, hali hii wataalamu wanasema inazidisha gharama ya kusafirisha ile kontena kuja hapa, kwa sababu hairudi na bidhaa.

Mhe. Naibu Spika, hata chumvi jamani ipo tele sasa hivi hebu hizi wizara mbili naomba tushirikiane, bahati nzuri ziko katika hii *cluster* moja. Wizara ya Kilimo na Wizara ya biashara hebu tushirikiane tuone tunasafirisha angalau hii chumvi, juzi nilipokwenda pale mimi niligundua moja katika tatizo hawana utaalam wanasema mashine yetu haitoi chumvi iliyokuwa kavu nikamwambia nyie mnatoa madini fulani, kuna madini yanaitwa *magnesium sulphate* yamo ndani ya chumvi mnayatoa haya. Kwa sababu *magnesium sulphate* ina tabia ya kunyonya maji katika hewa wakasema hatuyatoi tunaikausha tu. Sasa nikajua kwamba lipo tatizo la kitaalam nawaomba sana jamani chumvi inahitajika katika soko la *SADEC* tuna bidhaa nzuri ya kusafirisha hebu tufanye angalau kwanza tusafirishe chunvi, kwabla ya kwenda kwenye hiyo sukari iliyoko Mahonda angalau tusafirishe hiyo chunvi kwanza.

Lazima vichwa vyetu tuvivunje ili tuweze kujua ni kitu gani na bidhaa gani mimi nasema *serious* watu wanaitaka chunvi kweli kweli, lakini haiajapata utaalam wala ushughulikiaji, tunawaomba sana wiraza zote mbili washirikiane tusafirishe chumvi angalau tunaze na tani mia moja kwanza.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nizungumze kwa ufupi na nitajitahidi nizungumze kwa ufupi. Mimi kwanza nataka niongeze nizipongeze kamati kwa kazi nzuri inazofanya au iliyofanya, lakini bado kwa upande wangu naona kuna mapungufu mengi ambayo kamati inahitaji kuweza kuyafuatilia.

Lakini kwanza nitoe masikitiko yangu na masikitiko yangu ni kwamba kutokana na huu muondo wa Kamati zetu sijaona kamati ambayo imesimamia, kufuatilia uchumi wa Zanzibar, siku zote sisi kazi yetu ni kulalamika tu serikali haina fedha sasa serikali kwa utaratibu huu haitokuwa na pesa kwa sababu hakuna kamati ambayo inaangalia uchumi wa Zanzibar na kuweza kutoa ushauri. Bado narejea tena kusema kamati hii jina libadilishwe na hata taasisi zilizokuwa chini yake tuweze kuzifanyia marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, nilidhani kamati hii ingeendelea kuwa na jina la Kamati ya Fedha na Uchumi kwa sababu hawa sasa hivi wanashughulikia fedha tu hawashughulikii uchumi, kama tungeliwakabidhi masuala ya uchumi nadhani kamati hii ingelileta maoni mengi na ushauri kuishauri serikali, kuweza kuona maeneo ambayo serikali inaweza kukusanya fedha na yale maeneo ambayo fedha zinavuja. Sioni sababu ya suala la utalii kutokuwepo chini ya kamati hii na ndio maana nikasema Mhe. Naibu Spika, kwamba hakuna kamati inayosimamia uchumi, leo hata muunda wa Wizara zetu tukiangalia utalii ambao ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu umekwenda kuwekwa kwenye Wizara ya Habari Utamaduni na Utalii, wakati utalii zaidi katika serikali ya awamu ya sita serikali ilijitahidi sana kuhakikisha kwamba mapato ya utalii yanakua na utalii unakuzwa mpaka ikafika pahala kwa ushauri wa waheshimiwa hapa Barazani Rais akakubali akaunda Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa sababu amekusanya mambo ya uchumi akayaweka pamoja.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri serikali bado tuangalie tena utalii utadumaa na mapato ya utalii yataendelea kudumaa kwa sababu yako katika Wizara ambayo siyo inayoshughulikia uchumi wa nchi, sasa Mhe. Naibu Spika, naomba sana tuangalie suala hili kwa sababu kamati hii ya fedha. Kwa sababu mimi sioni kamati ya uchumi mpaka sasa hivi haja yetu uchumi wa nchi ukue, kwa hivyo tunataka kamati hii tuangalie uwezekano wa kuweza kubadilisha taasisi zilizokuwepo chini yake na utalii uwe chini ya kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, nataka niendelee katika kutafuta au kuangalia maeneo ambayo tunaweza kuimarisha uchumi wetu Zanzibar, bado naiomba kamati hii ingalie katika bidhaa zinazoingia nchini, hasa bidhaa za vyakula ambazo zinalipiwa ushuru. Tuangalie namna ya meli zetu bidhaa zinazoleta na ile mizigo namna inavyoorodheshwa yani tani zinazoingia na meli katika nchi yetu

kwa ajili ya kuteremshwa bidhaa hapa Zanzibar, kwa sababu bado Mhe. Naibu Spika, namuomba Mwenyekiti wa Kamati hii ya Fedha kwamba ajaribu kuangalia eneo hili bado alisimamie kuhakikisha kwamba mapato ya uchumi wetu yanaendelea kukusanywa kwa vizuri.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, naiomba sana kamati kwa kuwa inashughulikia mambo ya fedha bado iendelee kusimamia na kuishauri serikali kusisitiza kwamba gawio la Zanzibar katika Muungano lije kama Zanzibar tunavyohitaji, wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi kwa muda mrefu wamesema kwamba gawio la Zanzibar haki yetu tupatiwe 11.5 na sio 4.5. Mhe. Naibu Spika, tunaendelea kulalamika uchumi wa Zanzibar ni mdogo lakini uchumi wa Zanzibar ni mkubwa ukiangalia kama tutaweza kufuata hasa yale maelekezo ambayo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanayatoa hapa barazani, kwa sababu ukiangalia 4.5 katika *hundred percent* ukweli ni *percentage* ndogo, lakini vile vile kamati hii pamoja na suala hili kuwemo katika kero za Muungano bado tunaomba kamati hii iendelee kufuatilia hisa za Zanzibar katika uanzishwaji wa *BOT*.

Kwa sababu haya ni maeneo ambayo kama tutaweze kuyasimamia kwa vizuri sisi hatuna sababu ya kulalamikia uchumi wa Zanzibar kuwa ni mdogo, wananchi wetu Mhe. Naibu Spika, wanaishi katika hali ya umasikini lakini kumbe kuna maeneo ambayo tukiyasimamia kidete basi hali za wananchi wetu zinaweza kuboreka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika masuala mazima ya muungano sasa hivi ingawa kuna vugu vugu la mchakato wa kuanzisha katiba mpya na marekebisho ya katiba, lakini sisi kwa upande wetu Zanzibar yale maeneo yetu ambayo tunayaona yameandikwa ndani ya katiba hayatekelezwi basi bado tunayo nafasi ya kuweza kuyasemea ili yakaweza kutekelezwa kimuungano.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la bandari ukiangalia kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala la bandari ni suala la muungano, lakini je utekelezwaji wake unatekelezwa kimuungano. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika suala zima la muungano mapato yanayogawanywa kimuungano kwa upande wa bandari ni eneo moja tu ni suala la moja tu ni suala la minara, meli zinapoingia katika bandari zetu aidha zitapitia Zanzibar au Mtwara na sehemu nyengine yale mapato yake ndio yanagawiwa karibu asilimi 49% kwa 51% baina ya mashirika yetu ya bandari. Lakini ukiangalia yale mapato mengi ambayo ndio makubwa zaidi hayatekelezwi kimuungano, ndio maana mimi nikasema bado kuna umuhimu wa hii kamati yetu ya Fedha iitwe kamati ya uchumi ili kuangalia maeneo mengine ambayo tunaweza kukusanya fedha nyingi kwa ajili ya kuendesha uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie ili nisije nikakosa la kusema wakati wa Bajeti masuala ya mapato ya gesi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya shindikizo la Baraza la Wawakilishi tulisema kwamba suala la mafuta liondoshwe kabisa katika katiba ya muungano, yaani lisiwe suala la muungano. Suala hili mpaka sasa hivi najua mnalionea haya lakini sisi bado tunaendelea kusema kwa sababu serikali bado iko kimya, zile jitihada ambazo tulikuwa tunaziona kama miezi minane iliyopita kabla ya serikali ya awamu ya saba inaonyesha jitihada zile sasa hivi zimekwisha na hakuna mtu yeyote ambaye limo ndani ya akili yake kuweza kulishughulikia suala hili. *(Makofi)*

Lakini wakati huu tukiendelea kudai kwamba suala la mafuta liondoke katika masuala ya muungano bado suala la gesi kwa kuwa inakusanywa na mpaka sasa hivi ni suala la muungano, Mhe. Naibu Spika, mapato yetu ya gesi yaliyokusanywa kwa ndani ya miaka minane kule Bara tunahitaji mapato yale tuyapate. Mhe. Waziri wa Fedha utakapokuja kwenye bajeti tunatoa indhari mapema aje atuambie kwamba ni kiasi gani ya mapato yamekusanywa ya gesi kwa miaka minane iliyochimbwa kule Tanzania Bara, na Zanzibar mpaka sasa hivi haki yetu iko kiasi gani. Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, shughuli itakuja kuwa nzito kwa waziri wa fedha *(Makofi)*

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, nasema haya kwa uchungu kwa sababu bado mimi kama mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuna haki zangu za kimsingi ambazo nahitaji nizipate lakini naambiwa serikali haina fedha, wakati nikiangalia kwa haya niliyoyasema fedha naziona na naamini Serikali ikiweza kusimamia vizuri fedha hizi zitaweza kupatikana na wananchi wetu waishi katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi yake nzuri, naunga mkono ripoti ya kamati. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nataka niipongeze kamati, ukweli kamati imefanya kazi nzuri chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Salmini Awadh Salmin ma wajumbe wake wote. Ripoti ya kamati nimeisikiliza kwa makini sana na nimejaribu kuwasikiliza kwa makini sana Waheshimiwa wawakilishi.

Naomba na mimi nitoe ufafanuzi katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo: Kwanza labda nianze na jila la kamati nataka niwaambie tu waheshimiwa serikali sio iliyoweka jina la kamati, jina la kamati limewekwa na baraza lenyewe na liko kwenye kanuni sisi serikali hatuna matatizo yoyote kama mtabadili jina alimradi mkatuambia tu kazi za kamati hiyo ni zipi na zipi kama

mnavyotuambia kwa kamati ambazo zipo sasa hivi. Kwa upande wetu sisi serikali hatuna matatizo.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimeelekezwa na kamati na nyengine waheshimiwa wawakilishi, nianze na hoja ya kwanza ambayo kamati imeiona walichozungumzia ni mapungufu ya mapato katika kipindi ambacho kuanzia Julay/Novemba nataka nianze na hoja hiyo.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema tukaweka wazi ili kila mmoja aweze kufahamu kuanzia mwezi wa Julai, mpaka Novemba, 2010 taasisi yetu ya Mapato *Zanzibar Revenue Board* imekusanya bilioni 40.4 sawa na asilimi 93.3% imekusanya chini ya kiwango cha bilioni 2.9. Taasisi yetu ya TRA *Tanzania Revenue Authority* imekusanya bilioni 28.3 ni sawa na asilimia 104% imekusanya ziada ya bilioni 1.2 ya makisio. Hii ndio hali halisi ya makusanyo kwa taasisi zetu mbili hizo ZRB chini ya kiwango cha 2.9 bilioni na TRA zaidi ya kiwango cha 1.2 bilioni nini kilichosababisha chini ya kiwango ndio hapo ambapo waheshimiwa waligusia baadhi ya maeneo.

Kwanza mapato ya Mawizara makusanyo yanayokusanywa na Mawizara, lakini vile vile wamezungumzia mapato yaliyoshuka kutokana na uvuvi. Mhe. Naibu Spika, nataka nieleze ni kweli Mawizara yamekusanya chini ya kiwango lakini kwa sasa tumeshaanza kuzishajihisha Wizara ili waweze kukusanya zaidi, vile vile kuwa karibu na Wizara ili ziweze kukusanya zaidi.

Kwa upande wa mapato ya uvuvi na hususan yale ya bahari kuu. Mhe. Naibu Spika, utakumbuka kwamba huko nyuma ilikuwa hatukuwa na *authority* Zanzibar inasajili meli mapato yake yanaingia kwenye mfuko wa Zanzibar, lakini baada ya makubaliano tumekubali kuunda *authority* asilimia hamsini ya mapato yanayosajiliwa Bara na Zanzibar yanakwenda kwenye *authority* kwa matumizi yao na fedha zilizobakia tunagawana SMZ na SMT. Sasa ni dhahiri kwa mtiririko huu utaona kwamba kile ambacho kinakuja moja kwa moja kwetu kitapungua kwa sababu kuna na *authority* ambayo tumeiunga ya Muungano au ya pamoja inachukua sehemu yetu na sehemu za wenzetu zinakwenda pale.

Lakini hata hivyo Mhe. Naibu Spika, kuna hoja vile vile ambayo imeulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu juu ya suala zima la Shirika la umeme kupungua mapato yake, kwa sababu serikali ilikuwa ikiwapa fedha kufidia deni la matumizi ya umeme ndani ya taasisi zetu lakini serikali imesitisha fedha hizo, nataka nilitolee ufafanuzi kidogo hili suala ili tukiondoka hapa waheshimiwa wawakilishi sote tuwe na kauli moja na mtazamo mmoja. Serikali ilianza kulipa shirika la umeme kuanzia bilioni 300 mpaka ikaendelea ikakaribia hata bilioni

600 kila mwezi , lakini tuliwapa kwa sababu mbili kubwa hili nataka liwe *very clear* kila mmoja alifahamu.

Kwanza tuliwapa kusaidia *IDO* kwa upande wa Pemba, tulisema kwamba kwa sababu ndugu zetu kutoka Pemba umeme wanatumia wa majanareta tulilazimika serikali kusaidia mafuta yale ya *IDO* kupitia fedha hizo . Lakini la pili tulisema kwamba tunapunguza deni ambalo Shirika la Umeme ilikuwa inalidai serikali, sasa uamuzi baada ya kupatikana kwa umeme wa uhakika kutoka Pemba serikali imesitisha fedha hizo na tukasema sasa pamoja baina ya Shirika la Umeme na Serikali tuone tunadaiana nini tupate hesabu za uhakika ili tuweze kulipana, nathubutu kusema Shirika la Umeme na Wizara yangu wameanza kufanya kazi hiyo.

Lakini vile vile na nataka nitoe kauli hii Mhe. Naibu Spika, ndani ya Baraza lako tukufu tumetoa kauli na tumewambia shirika la umeme taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano zilizopo Zanzibar waziwekee tukuza, hii itapunguza kudaiana unachukua unaweka tunamaliza, hakuna ile kwamba unadai aliyekuwa haweki umeme katika taasisi yake atajikuta yuko kwenye giza. Kwa hivyo hii itasadia Shirika la Umeme kupunguza malalamiko na narudia tena waweke mita na taasisi yoyote inayokataa kuweka mita basi waje tuone taasisi hazipashwi kukataa kuweka mita za umeme ziwekwe zitapunguza hilo tatizo la Shirika la Umeme.

Mhe. Naibu. Spika, kuna suala jengine ambalo limekuja misahama. Kamati ilisema kwamba misamaha ni mikubwa na hasa misamaha inayopitia kwenye miradi, nataka nithubutu kusema kwamba ni kweli. Lakini nia yetu kama ni serikali tunataka kupunguza misongamano hiyo na nataka niihakikishie kamati yako tukufu na Baraza lako tukufu mwazi wa Januari, ilikuwa ni 2.4 bilioni, lakini katika mwezi wa February misamaha ilikuwa 0.78 bilioni. *(Makofi)* na tutaendelea kuishusha misamaha hiyo. Naomba sana mawaziri wenzangu tushirikiane kwa sababu misamaha mingine inapitishwa ndani ya Wizara zao bila ya wao kushirikishwa. Nawaomba sana tushirikiane katika hili ili tuweze kufanikisha hili suala.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine alililokuja kuzungumziwa ni suala la kuwa na taasisi mbili za kukusanya mapato zinatoka TRA na ZRB sasa nataka niseme tu Mhe. Naibu Spika, mimi kwa mtazamo wangu zinatupa *affections*. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, ZRB inakusanya sasa hivi bilioni 10 na zaidi na TRA inakusanya 6.7 bilioni kwa mwezi, lakini TRA inazozikusanya zile zote zinakuja SMZ tunatumia sisi, SMZ haina mamlaka ya kuwalipa mishahara wale ukiziunganisha hizi taasisi ukafanya moja sehemu ya pesa zile utatoa ili kuwahudumia mishahara ya wale wafanyakazi waliopo pale. Kwangu mimi kama ni msimamizi wa fedha nasema tuendelee na kuwa na taasisi mbili ili

fedha nyingi zaidi tuzipate kutoka TRA, vyenginevyo tutalazimika kuwalipia mishahara wale na hii itatupunguzia upeo wetu wa matumizi.

Kwa hivyo kwa upande wangu mimi nasema bado naridhika kuwe na taasisi hizo mbili mpaka hapo uamuzi utakapokuja mwengineo.

Mhe. Naibu Spika, kulikuja suala la kuitumia taasisi yetu ya ZSSF kuwekeza katika miradi mikubwa, nataka nithubutu kusema huo ndio mwelekeo wetu mkubwa, ZSSF iende katika kuwekeza miradi mikubwa lakini katika kipindi kama hiki bado ZSSF haijawa na uwezo huo ZSSF ina wanachama 59,000 karibu wanachama elfu sitini na tunataka tuipeleke mpaka iwe na wanachama laki moja. Juzi nilikuwa nasikiliza taarifa ya KBC Kenya wao sasa hivi wameingia kwenye utaratibu wa kuzalisha umeme wa upepo 100. MW thamani yake ni 60 bilioni Kenya shillings. Kwa hesabu za haraka haraka unazungumzia 8 tirion Tanzania shillings. Sasa hizo ni pesa nyingi ukiwaambia ZSSF wawekeze kwenye mradi mkubwa kama huo hawana fedha hizo, lakini ukweli ni kwamba tunataka ZSSF nayo iende kuwekeza katika miradi mikubwa mikuba.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala kwa nini vifurushi visije moja kwa moja Zanzibar badala ya kutua Dar es Salaam mimi ningependa ikafanyika hivyo, kwa sababu hicho kifurushi kinabebwa ndani ya ndege ningependa sana ndege ikaja moja kwa moja Zanzibar kwa sababu ningepata kupata. Lakini ukweli ni kwamba virushi vyenyewe na wakala wenyewe huwa wanaangalia ndege gani wana mikataba nazo katika kusafirisha vifurushi vyo ndege nyengine zinakuja Dar es Salaam, la msingi ni kwamba wale wenzetu wanaohudumia hivyo vifurushi wawe makini katika kuleta kifurushi hicho kwa muda mfupi tu.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala jengine ambalo lilizungumziwa kuhusu habari ya serikali ina mipango gani katika kuinua pato la taifa , nataka niseme tu Mhe. Naibu Spika, tumeangalia *contribution* za sekta zote kwenye pato la taifa, tumegundua kuna baadhi za sekta *contribution* zake n indigo lakini tukizipa msukumo zinaweza kufanya vizuri. Moja nataka kusema ni sekta ya viwanda *contribution* yake ni chini ya 8% kwenye pato la taifa.

Pili ni sekta ya uvuvi *contribution* yake kwenye pato la taifa ni chini ya asilimia tano sekta hizi tumesema tukizipa msukumo zinaweza kuongeza sana pato letu la taifa, hali kadhalika tukibadilisha kilimo chetu sasa hivi kilimo chetu sehemu kubwa ni sehemu ya kutegemea mvua lakini hivi sasa tunataka tuende kwenye kilimo cha *irrigation*. Mhe. Waziri yupo tunahangaika pamoja kutafuta fedha kwa ajili ya kuweka miundo mbinu ya umwagiliaji, tukifanikiwa basi tutabadilisha pato la taifa na litaongezeka. Bahati mbaya Waziri wa Uwezeshaji ametoka kidogo lakini tumepewa kazi mimi Waziri wa Uwezeshaji na Waziri

wa Uvuvi, kuangalia jinsi gani tutakavyoweza kuwawezesha wananchi moja kwa moja sio ule utaratibu wa kuwapa pesa, utaratibu wa kuwapa pesa mtu anapokuwa na shida zile pesa anatumia, tunataka tuwawezeshe wananchi moja kwa moja.

Kama tunaona mwananchi huyu ana uwezo mzuri wa kufuga, basi ni mifugo ya aina gani inaweza ikastawi hapa. Pelaka mifugo, wawekee mabanda waanze kazi moja kwa moja, tunaangalia hilo. Tukianza huko kuwawezesha wananchi naamini pato letu nalo litaanza kukua vizuri sana na mapato ya wananchi yataweza kukua. Mhe. Mwenyekiti, mipango iko mizuri na mingi tu. Tunataka kuifanya, sio kuifanya kwenye karatasi. Tunataka kwenda *field* kuifanya ili tuweze kufanikisha mambo yetu.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti ambalo nimeliweka kwa sababu wengi walilizungumza, majengo. Nataka nithubutu kusema majengo mengi ya serikali, wizara zetu zinakaa katika majengo makongwe au majengo ya zamani. Baraza la Mawaziri limeunda Kamati ndogo, mwenyekiti wake nikiwa mimi, mjumbe Mhe. Waziri wa Ardhi, Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mhe. Waziri wa Katiba. Hao ni wajumbe.

Kuyaangalia majengo haya yote yanahitaji matengenezo kiasi gani na kuweka utaratibu kama kuuzwa yauzwe kwa taratibu upi. Ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya kujenga majengo mengine kwa ajili ya matumizi yetu. Hii kwa ajili ya Unguja na Pemba. Tayari Wizara ya Utumishi na Utawala Bora, tumeshawapa kibali. Watafute kiwanja waanze kujenga jengo la Wizara Pemba. Hatua hizo tunakwenda nazo. Suala la majengo la Wizara sasa hivi tunalifanyia kazi na tunataka liweze kuwa katika Bajeti yetu inayokuja.

Suala la jengo la Afisi ya Rais. Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba. Nataka niseme kwa masikitiko makubwa. Hata na mimi nilipoliona lile jengo nimesikitika sana. Jengo hili serikali imetumia zaidi ya milioni mia saba kwa ajili ya jengo hili. Kama mambo yangekwenda vizuri jengo hili lilitarajiwa kumalizika mwaka jana. Sasa hivi ingelikuwa ni historia kwa Wizara ya Fedha kuwa na jengo zuri na wamekuwa wameshaanza kulitumia. Kwa bahati mbaya Mkandarasi hakuzingatia ushauri wa muelekezi. Hili jengo limekatika na tumelifelisha kuliendeleza.

Sisi wizara tulichokifanya ni kukaa kitako na Mkandarasi. Tumesema tunataka ku-*settle* naye nje ya Mahakama na ku-*settle* kwetu ni rahisi, aturejeshee mtaji wetu, achukue jengo lake. Mazungumzo yetu yapo mbali sasa hivi na tutakuja kuleta taarifa rasmi tumemalizane naye vipi.

Ushauri wa wajumbe tumeupokea lakini na sisi wizara husika hatuwezi tukaziwacha fedha za wananchi zikapotea kama vile. Mkandarasi tumemwambia aturejeshee hela yetu yote tuliyompa ili tuweze kufanya mambo mengine. Tayari Mhe. Naibu Spika, tumesha-*indentify* eneo jengine kwa ajili ya kujenga Wizara ya Fedha na sehemu fedha hizo tutazitumia kuweza kujengea jengo jengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nadhani nimeweza kujibu baadhi ya hoja nyingi. Kulikuwa kuna suala la *Join Finance Commission*. Mhe. Rashid Seif aliliulizia. Nataka nimwambie tayari tumepokea. Ile ripoti ya mwanzo imepitiwa na Baraza la Mawaziri la Zanzibar na ikapitiwa na Baraza la Mawaziri la Muungano. Ikagundulikana kwamba ina takwimu za zamani. Ilikuwa ina takwimu za mwaka 2004/2005 na leo tunazungumzia mwaka 2010/2011.

Kwa hivyo *Join Finance Commission* wameambiwa wa *up date* zile *statistic* zao. Kwa bahati nzuri wiki mbili zilizopita nimepokea ripoti mpya ambayo wame *up date* zile takwimu na sasa hivi wizara yangu tunaandaa waraka kuiwasilisha ripoti ile kwenye *cabinet* tena. Tukishapata kibali nadhani utekelezaji wa ile ripoti utaanza mara moja. Mhe. Naibu Spika, sina haja ya kulitolea ufafanuzi OIC kwa sababu halimo humu katika ripoti hii. Nadhani hilo ataliuliza tena wakati wa Bajeti, na mimi naliwacha kama lilivyo.

Suala la Mhe. Hamza nadhani asiwe na wasiwasi na mimi, tupata majibu mazuri ya kuweza kusaidiana katika suala zima la matumizi ya gesi. Tutaweza kutafuta taarifa hizo na wakati ukifika tutaweza kumsaidia, kimepatikana nini na kimetumika vipi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nakupongeza leo upo *very, very smart* (Vicheko na Makofi). Naomba nichukue fursa hii nimpongeze Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa jinsi alivyokuwa mzoefu na alivyoiwasilisha ripoti yake vizuri na yenye kufahamika. Nampongeza yeye pamoja na wajumbe wake wote kwa juhudi yao waliyochukua kutayarisha ripoti hii nzuri.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, kujibu au kuyaweka sawa yale masuala ambayo baadhi ya wajumbe walikuwa wana wasi wasi nayo. Kwanza ni suala la biashara huria ambayo mwakilishi amesema imekuwa biashara holela. Huu ni mfumo wa biashara ya leo. Kwa hivyo biashara ziende kwa mujibu wa nguvu za soko na sio nguvu za amri.

Hata hivyo sheria zetu tulizonazo katika biashara zimepitwa na wakati kidogo. Wizara yetu imo mbioni kuzifanyia kazi sheria hizo ili kuzirekebisha. Vile vile

kutunga baadhi ya kanuni ambazo zitaweza kusaidia katika suala hili la kuweka biashara hii isiwe holela kama vile inavyofikiriwa.

Juhudi zimeshaanzwa kufanywa baina ya Wizara yetu ya Biashara na wafanyabiashara. Tumekaa pamoja na kuzungumza namna gani ya kuweza kuona kabla ya kukaa kitako wenyewe kufahamishana na kupanga bei zao, wafanye mashauri na Wizara ya Biashara ili kuona bei zao wanazozitoa zinalingana na hali halisi ya bei za dunia na hali halisi ya maisha ya wananchi wetu. Bila ya ukaidi wafanyabiashara hao kwa moyo mmoja wamekubali kushirikiana na serikali yao kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili kuona tunakaa pamoja kuangalia bei ya bidhaa, tangu anaponunua mzigo, wakaupakia katika meli, hadi kufikia bandari ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika mazungumzo hayo tumewashirikisha wenzetu wa TRA, ZRB, Shirika la Bandari na wengineo. Kuona namna gani serikali nayo itaweza kupunguza baadhi ya gharama ambazo si muhimu. Vile vile na wafanyabiashara kupunguza faida zao ili kuwawekea bei nzuri wananchi wapate kufaidika na bidhaa muhimu ambazo tunahisi zitaweza kuwasaidia katika maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwahakikishie wawakilishi wote wa Baraza tukufu kwamba Serikali yetu Zanzibar, kupitia Wizara yake ya Biashara, suala hili tunaliona na tunalifanyia kazi. Hivi karibuni tu wataona hatua tutakazozichukua.

Kuhusu suala la ZSTC vile vile ripoti imeeleza na wachangiaji wengi wameeleza kwamba magendo ya karafuu ni makubwa na Shirika lipo katika hali ya kuyumba yumba.

Ni kweli na serikali kupitia Wizara ya Biashara imeshapitia suala hili la ZSTC na kwa sasa hivi tumo kufanya mabadiliko makubwa ya ZSTC. Naamini katika kipindi kifupi kijacho mtaona mabadiliko makubwa katika Shirika la ZSTC ambalo litakuwa na mamlaka ya kuweza kuuza karafuu zao bila ya kutumia mawakala. Vile vile kuzingatia suala la mikarafuu kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Yupo mwanasheria mmoja alisema zao la karafuu limekuwa kama mtoto wa nje ya ndoa. Kwa sababu anasema zao hili Wizara ya Kilimo kazi yao kupanda mkarafuu, ZSTC ni kununua na kuuza. Kwa hivyo hakuna mtu anayeangalia. Imekuwa kama mtoto wa nje ya ndoa, mtoto akizaliwa hashuhulikiwi isipokuwa siku ya mwisho anatafutwa kadhi akatoe idhini. Hajui kalelewa wapi, kasomeshwa wapi na wala katoka wapi. Masuala haya sasa hivi itakuwa

mikarafuu inaanza kushuhulikiwa tangu inapoanza kupandwa miche, hadi kufikia uzalishaji. Naamini kwamba njia hiyo itaweza kusaidia sana.

Lakini vile vile suala la kuangalia bei za karafuu ili kuwapa wakulima bei nzuri ambazo kwamba zitapunguza kwa kiasi kikubwa kushajihisha suala la magendo ya karafuu nje ya nchi. Pia ushirikiano baina ya wananchi na serikali yao pamoja na viongozi wao wote wakiwemo sisi hapa Wawakilishi kwenye Baraza hili Tukufu. Naamini kwamba linaweza kuzuia wimbi kubwa la magenzo hasa linatoka katika sehemu ya Kaskazini Pemba.

Baada ya hapo kulikuwa kuna suala la, habari ya kiwanda cha Mahonda, ambalo nimeshalieleza asubuhi. Lakini nataka niwatoe wasi wasi tena, ndugu zangu Wawakilishi. Serikali hili tumeliona na tunalifanyia kazi. Katika kipindi kifupi tutakupeni taarifa ya serikali, namna gani tutaweza kukaa pamoja na huyu muwekezaji, kuona kama tunaweza ku *review* mkataba au tunaweza kuangalia masuala mengine.

Naomba kusisitiza kwamba hiki ni kiwanda muhimu sana. Kilitarajiwa kuajiri watu wengi sana na kuzalisha kiwango cha sukari ambacho kingiweza kuhifadhi gharama za pesa za kigeni kununua sukari kutoka nchi za nje. Kwa hivyo ningeomba tuwe na subira kidogo, katika kipindi kifupi tu tutapata *result* zake. Lakini haya tumeyazingatia, tunayachukua na tutayafanyia kazi.

Suala la viwanda ni kweli viwanda vingi nchini vimekufa na vyengine vinajikongoja, vipo taabani. Kuna mambo mengi sana yanatukabili, lakini moja wapo ni kwamba gharama za uzalishaji pamoja na upatikanaji wa malighafi nchini. Katika masuala ya uzalishaji ni kweli kwamba umeme unachangia kwa kiwango kikubwa sana. Umeme wetu ni ghali masoko yetu ni mamoja kwa hivyo tutashindwa kuwa na ushindani katika masoko ikiwa suala la umeme halikushughulikiwa.

Kwa sasa hivi suala serikali imechukua jitihada kwamba suala la malipo ya umeme yametiwa katika orodha ya kero au changamoto za Muungano. Limeshaanza kuzungumzwa na tunalishughulikia kuona kwamba agizo la Mhe. Rais wa Tanzania Mhe. Jakaya Kikwete kwamba bei ya umeme Tanzania Bara na Tanzania Visiwani iwe moja. Tutafanya jitihada kuona kwamba ile kauli ya Mhe. Rais inatekelezwa kwa vitendo. Hasa kwa vile ile *infrastructure* yenyewe ya umeme kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar ni mali ya Zanzibar. Suala hili tunalifanyia kazi naamini kwamba likitatuka basi viwanda vyetu vitapata nafasi nzuri sana ya kufanya kazi nzuri sana.

Pia Wizara yetu ya Viwanda inashirikiana na Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Uvuvi na Mifugo, kuona kwamba tunashirikiana kwa pamoja kupata

rasilimali ambayo itatusaidia sisi kuweza kuwa na viwanda ambavyo vinapata rasilimali hapa hapa nchini. Kwa mfano viwanda vya usindikaji samaki na viwanda vya matunda na kadhalika. Hili wizara inalifanyia kazi na wala halikufumbia macho. *Inshallah* kwa kipindi kifupi mtaona mabadiliko katika sekta ya viwanda.

Tukija katika uzalishaji wetu. Mwakilishi kasikitika sana, basi hata chumvi hapa Zanzibar hatuwezi kuzalisha, wakati chumvi imetuzunguka kila upande wa visiwa vyetu. Hilo suala ni kweli chumvi inazalishwa katika visiwa vyetu. Ingawa utaalamu bado haujafika katika kiwango kizuri. Hilo vile vile wizara yetu imelichukulia hatua madhubuti. Hivi karibuni tulikuwa na mkutano na wenzetu wa *UNIDO* kuona namna gani wataweza kutusaidia. Sasa hivi kiwanda cha chumvi kipo pale Wawi Pemba na wana umoja wa wazalishaji chumvi wamejiunga. Kiwanda kile ni chao wao, wanachokosa ni mashine moja ya kukaushia chumvi ili kukausha chumvi ile iweze kukaa kwa muda mrefu.

Pale wanao mtambo wa kutia *iodine* ambao unakuwa *supported the UNICEF* ambayo ndio hasa utaweza kusaidia madini haya kupunguza maradhi ambayo yamekusudiwa kwa watoto na hata watu wazima. Kwa hivyo *UNIDO* wametuahidi kwamba mashine ile wataifatuta na watatusaidia ili kiwanda kile kiweze kuzalisha chumvi ambayo itakuwa na madini joto na ambayo itakuwa imeshakaushwa. Sio chumvi tu viwanda vingi malighafi zitaimarishwa katika kipindi hichi. Naomba tuwe na subira na tuombe dua mambo yetu yaende kama tulivyoyapanga.

Kuhusu bidhaa za vyakula. Ni kweli bidhaa zote zinazotoka nchi za nje zinapokuja Dar-es-Salaam *container* bei inakuwa ni ndogo kwa sababu wanapoondoka wanaondoka na mali katika ma-*container.* Kinyume na Zanzibar. Zanzibar kidogo bei ni kubwa kwa sababu *container* likija hapa linaondoka tupu. Hii inatokana na kwamba uwezo wetu wa uzalishaji ni mdogo. Naamini kabisa tukiweza kuimarisha viwanda, tukaweza kuimarisha kilimo basi naamini tutaweza kusafirisha bidhaa zaidi.

Vile vile juhudi ya Wizara ya Miundombinu ya kuweka mkakati mzuri wa kuweza kujenga Bandari kubwa zaidi ambayo itatusaidia katika masuala ya *transit trade,* haya nayo yatatusaidia sana katika masuala ya kupunguza bei za ma–*container* kuja Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mpaka hapo nimeweza kujibu zile hoja muhimu ambazo zimezungumzwa na Wajumbe mbali mbali. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa hii kutoa ufafanuzi kama upo unaohitajika unaohusiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Kwanza nianze na kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin. Hoja nyingi za Waheshimiwa Wajumbe zililenga Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo zikifuatiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mbali ya Mhe. Rashid Seif na Mhe. Mwenyekiti, hakuwa na hoja inayolenga Wizara yangu. Hoja zaidi zilikuwa katika kuielekeza wizara yangu. Kwa hivyo niseme tu nakubaliana nao na Wizara itayachukua, ushauri na maoni yao tutayafanyia kazi inavyopaswa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo (Mhe. Salmin Awadh Salmin): Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufanya majumuisho mafupi.

Mhe. Naibu Spika, ripoti yetu imepata kuchangiwa na Waheshimiwa Wajumbe watano (5) nao ni kama hivi ifuatavyo:-

(1) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
(2) Mhe. Hija Hassan Hija
(3) Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
(4) Mhe. Rashid Seif Suleiman
(5) Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Naibu Spika, masuala yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe, tayari waheshimiwa mawaziri wahusika tayari wameshayapatia ufumbuzi, wameweza kuyajibu vizuri. Naamini Waheshimiwa Wajumbe wameridhika nayo. Kwa wale waheshimiwa waliotoa ushauri naamini ushauri wao Waheshimiwa Mawaziri wameuchukua na wataendelea kuufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri watatu (3) waliotoa ufafanuzi.

Mhe. Omar Yusuf Mzee (Waziri wa Fedha, Uchumi na Maendeleo)
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui (Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko)
Mhe. Mansoor Yussuf Himid (Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili)

Kwa majibu yao na ufafanuzi wao mzuri. Naamini majibu haya yatakuwa yamewaridhisha waheshimiwa Wajumbe. Kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, nichukue nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia ripoti

yetu na wale waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia, wanaweza kuchangia katika ripoti za siku zijazo.

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. Naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

Mhe. Naibu Spika: Ndugu wajumbe ilikuwa tuna kamati tatu (3) tuzipitishe leo, lakini hii moja zimebakia dakika kumi. Inaonesha hata Mwenyekiti wetu wa pili hatuwezi kumwita akasoma. Kwa hiyo tunaomba tuje jioni mepema tumalize Kamati mbili zilizobakia. Sasa naahirisha kikao mpaka saa 11 za jioni.

(Saa 6.45 Baraza limeakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

RIPOTI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA USTAWI WA JAMII

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii (Mhe. Amina Iddi Mabrouk): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kabla sijaanza kutoa hotuba yangu naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa na kwa furaha kubwa kukupongeza wewe Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kwa mara ya kwanza kukalia kiti hicho ukiwa kama Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema ya kuweza kukutana hapa leo hii, kwa lengo la kujadili masuala mbali mbali yenye maslahi na nchi yetu pamoja na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, tunapenda kumshukurani Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuzifanya na hatimae kuzikamilisha kazi zetu za kamati kwa mafanikio. Hali hii imetokana na kupata mashirikiano makubwa kutoka katika wizara zote na watendaji wake zilizo chini ya kamati yetu kwa kuziwezesha kutekeleza majukumu yake ya ufuatiliaji wa kazi za kamati kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi-Zanzibar.

Mhe.Mwenyekiti, aidha napenda niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa ushirikiano wao mkubwa uliokuwepo muda wote ambao Kamati ilifanya kazi zake za ufuatiliaji, kuihoji Serikali na hatimae kutoa maoni ili kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu ina wajumbe wanane na makatibu wawili. Naomba niwatambulishe wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
4. Mhe. Asha Abdu Haji	-	Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
6. Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Mjumbe
7. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Mjumbe
8. Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Mjumbe
9. Ndugu Talib Enzi Talib	-	Katibu
10. Ndugu Shemsa Maabad Mohamed	-	Katibu

Mhe.Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niwasilishe mbele ya Baraza lako tukufu Muhtasari wa taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii juu ya utekelezaji wa shughuli za wizara tatu za serikali ambazo zipo chini ya usimamizi wa Kamati yetu.

Mhe, Mwenyekiti, Kamati yetu imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha kanuni cha 104(d) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Majukumu na kazi za kamati hii yameelezwa katika kanuni ya 110 ya kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati hii katika mwaka uliopita.
b) Kufutilia utekelezaji wa sera na mipango ya wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.
c) Kufuatilia Mapato na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya wananchi iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imepewa uwezo wa kusimamia wizara tatu za Serikali ambazo ni:-

i. Wizara ya Afya.

ii. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

iii. Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Kamati ilifanya kazi zake katika awamu mbili kwa kipindi cha wiki nne. Awamu ya kwanza ilifanya kazi kwa muda wa wiki mbili Pemba ambapo kwa awamu ya pili ilikuwa kwa upande wa Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhishwa na utendaji wa wizara hizo. Ingawa bado kuna maeneo yana mapungufu katika baadhi ya wizara ambayo yanahitaji ufuatiliaji wa msingi ili kupatiwa ufumbuzi na kukuza ufanisi. Kigezo cha uchumi duni tulionao kisiwe ni sababu pamoja na mambo mengine inayopelekea kukwama katika utekelezaji wa baadhi ya mambo ambayo yapo chini ya uwezo wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu umuhimu wa Sekta ya Afya kwa maisha ya mwanadamu. Ni vyema basi kuendelea kumpongeza Rais wa kwanza wa Zanzibar Marehemu Abeid Aman Karume kuzingatia umuhimu huo na kuanzisha utaratibu wa kuwa na matibabu bure mnamo mwaka 1964. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko na hali ya uchumi wa Zanzibar hivi sasa, wananchi hulazimika kuchangia kiasi kidogo ili kuipa uwezo zaidi wizara kutoa huduma muhimu za afya kwa ubora na ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati katika ziara yake katika Wizara ya Afya ilipata nafasi ya kutembelea taasisi zake mbali mbali Unguja na Pemba. Mbali ya kuwepo kwa baadhi ya mafanikio ambayo Kamati yangu yameyaeleza katika ripoti kuu katika uimarishaji wa sekta ya afya, lakini bado kuna maeneo yanahitaji kuimarishwa na kuchukuliwa hatua za haraka ili kuhakikisha kuwa wananchi wanafikishiwa huduma hiyo kwa ufanisi.

Kwa mfano, huko Pemba Kamati yetu iliweza kutembelea Hospitali ya Wete, Mkoani na Chake Chake. Kamati imesikitishwa sana na hali iliyoikuta Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani, kwa kweli hospitali hiyo ni chafu na hairidhishi kwa ajili ya kuhifadhiwa wagonjwa wa aina zote. Kamati imeitaka wizara kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa hospitali hiyo inarejea katika mazingira bora ya usafi. Imebaini kuwa hali hiyo imetokana na kutokuwepo kwa uwajibikaji ipasavyo.Aidha, katika Hospitali ya Wete kuna tatizo la kukosekana kwa vyumba vya kuhifadhia maiti. Jambo hili Kamati imeona ni muhimu na kwamba ipo haja kwa serikali kuhakikisha kuwa sehemu hizo zinaanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti, aidha Kamati yetu inaishauri Wizara ya afya kuweka mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa chumba cha *I.C.U* katika Hospitali ya

Mnazi Mmoja kinafanyiwa ukarabati wa kiutaalamu na kuwekewa vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya wagojwa mahatuti. Kutokana na Kamati kubaini kuwepo kwa muuguzi mmoja tu, hitilafu ya vifaa muhimu na udogo katika kitengo hicho cha wagonjwa mahututi, imeiagiza wizara kuhakikisha kuwa kitengo hicho kinaongezwa,kinapatiwa wauguzi wa kutosha na vifaa vyote vilivyokosekana kulingana na mahitaji kabla ya Kikao cha Bajeti 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inasisitiza umuhimu wa kuwaenzi wataalam wa Wizara ya Afya ili wapate moyo wa kuwatumikia Wazanzibari ikiwa ni pamoja na kuwapatia maposho yao kwa wakati, usafiri na mahitaji mengine muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la upungufu wa wafanyakazi katika sekta za afya limejitokeza sana kwa upande wa Pemba na Unguja kiasi cha kupunguza ufanisi katika wizara hiyo. Hivyo, Kamati imeitaka Serikali pamoja na kuwa ina mpango maalumu wa kupunguza Wafanyakazi, kuona umuhimu wa kuendelea kuajiri wafanyakazi katika kada zote za afya.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilipata nafasi ya kutembelea Kituo cha Uuguzi Pemba na Unguja kilicho chini ya *Zanzibar Commercial Institute*. Kutokana na mazingira ya kituo hicho, Kamati imekubaliana na hoja zote za Wizara ya Afya na Elimu kuhusu kuendelea kuwepo kwa kituo hicho kwamba hakijatimiza masharti ya usajili. Hivyo, kamati inashauri uongozi wa kituo hicho, Wizara ya Elimu na Afya kukaa pamoja kulitafutia ufumbuzi suala hilo. Chuo ni lazima kifuate masharti ya usajili ili kiweze kutoa mafunzo ya uuguzi kwa sifa zinazotakikana.

Mhe. Mwenyekiti, Miradi ya Ukimwi ni miongoni mwa miradi ya afya inayobahatika kupata ufadhili mkubwa, lakini wasi wasi wa Kamati yetu ni kuwa Je, kuna udhibiti upi juu ya matumizi ya fedha hizo? Hivyo, Kamati inashauri kuwa fedha zinazopatikana kupitia miradi ya Ukimwi zioneshwe katika Bajeti ya Serikali ili Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali aweze kuzikagua.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeona kuwa bado kuna ufinyu wa bajeti unaoikabili sekta hii muhimu ya afya hivyo inaishauri Serikali kuzingatia suala hili ili kunusuru kupungua kwa ufanisi katika sekta ya afya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Elimu ni muhimu katika maendeleo la taifa lolote. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuwekeza kwa kuhakikisha kuwa inakuwa na wataalamu wa kada tofauti kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar ya baadae.

Mhe.Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaipongeza Serikali kwa kuona haja ya kuanzisha Mradi wa Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) huko Tunguu. Ingawa kuna hitilafu ndogo ndogo lakini kimsingi inapongeza hatua za ujenzi wa chuo hicho. Chuo kinatarajia kuongeza Kitivo Kipya cha Uhandisi mara baada ya kukamilika. Aidha, serikali inakusudia umalizike haraka ujenzi huo ili ukifika muhula ujao wa masomo majengo yaweze kutumika. Tunamshauri mjenzi kuongeza bidii ili aweze kumaliza ujenzi huo na kukabidhi kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imevutiwa na hatua nzuri ya maendeleo ya Chuo cha Amali Mkokotoni.Kwakweli Chuo hiki kimejitahidi kuhakikisha kuwa kinawapatia vijana waliokosa kuendelea na masomo kwa sababu tofauti elimu bora ya mafunzo ya amali. Kamati yetu imethibitisha kuwepo kwa vitendea kazi ambavyo vinaweza kukidhi haja iliyopo. Hali hii itasaidia vijana kuweza kujiajiri wenyewe na kupunguza tatizo la ajira nchini. Sambamba na Chuo hiki, Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji kimekuwa kikijitahidi kufikia lengo kama hilo.

Hata hivyo, Kamati imeishauri serikali kuhakikisha kuwa inakipatia vitendea kazi vya kutosha vikiwemo walimu wa fani maalum na baadhi ya vifaa ili nacho kiweze kukidhi haja inayokusudiwa. Suala la kuweka uzio katika vyuo vyote hivi pia ni muhimu ili kudhibiti utulivu kwa wanafunzi na hata kunusuru uvamizi wa maeneo yake.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Kamati kubaini kuwa kuna uhaba mkubwa wa walimu katika skuli takriban zote Pemba hasa kwa masomo ya sayansi, imeishauri wizara kulichukulia hatua tatizo hili kwa namna maalum itakayofaa ili vijana na taifa kwa ujumla liweze kukidhi haja ya fani hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ina umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kuwa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yanafikiwa. Jambo la kusikitisha ni kwamba bado uimarishaji wa taasisi hii hauridhishi. Kamati inaishauri serikali kuanzisha miradi zaidi kwa lengo la kuimarisha taaasisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kwa muda mrefu sasa Taasisi ya Karume imekosa kuwa na hatimiliki jambo ambalo Kamati imepata hofu ya kuwepo kwa uwezekano wa kuendelea kuvamiwa baadhi ya maeneo yake. Hivyo basi, Kamati imeiagiza wizara kuhakikisha kuwa inasimamia upatikanaji wa hatimiliki ili kudhibiti maeneo hayo kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imeanzishwa kwa lengo la kuinua na kuimarisha hali za Wanawake, Vijana, Watoto na Watu walio katika makundi maalum ya wazee wasiojiweza, mayatima na wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Katika ufuatiliaji wa wizara hii, Kamati imeweza kufahamu juhudi mbali mbali ambazo wizara imekuwa ikiendelea kuchukua katika utekelezaji wa majukumu yake hayo. Hata hivyo, wizara imeonekana kuwa na changamoto kuu tatu.

Kwanza, uhaba mkubwa wa nafasi katika jengo la wizara linalotumika hivi sasa. Jengo halitoshelezi hali ambayo imepelekea baadhi ya taasisi zake kutawanyika na kufanyakazi katika mazingira magumu katika ofisi tofauti mfano, Idara ya Ustawi wa Jamii inaendelea kutumia ofisi zake za zamani zilizopo karibu na majengo ya Mahkama. Hali hii kwa kiasi fulani Kamati imeona inaleta ugumu wa kiutendaji katika wizara hii muhimu inayosimamia ustawi wa watu. Hivyo, kuna haja kwa serikali kuzingatia kutafuta jengo litakalotosheleza kwa ofisi.

Pili, ufinyu wa bajeti ambao unasababisha wizara kutoweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi pia ni tatizo la msingi. Kamati imeitaka wizara ihakikishe kuwa inasimamia ipasavyo maelekezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohd Shein juu ya haja ya kuwa na bajeti ya kutosha katika wizara hii ili kuiongezea ufanisi.

Tatu, kuna haja ya kuajiri wafanyakazi wenye taaluma zinahitajika ili kuondokana mara moja na tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni wazazi na tunaelewa ugumu wa suala hilo kwa watoto na hata kwa wazee wetu ambao nao wanafikia hali ya kurudi katika utoto kutokana na umri na sababu nyengine za maradhi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza maslahi ya walezi katika Kituo cha Watoto Mazizini na vituo vyengine vinavyowahudumia wazee ili angalau yalingane na kazi za walezi hao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza wizara kuanzisha kituo cha *'ONE STOP CENTER'* kinachosimamia ukusanyaji wa taarifa mbali mbali za udhalilishaji wa watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kituo hicho ni muhimu kwa kweli kitasaidia kuondokana na tatizo sugu lililopo la kukosekana kwa ushahidi katika kesi nyingi za udhalilishaji watoto. Hata hivyo, inaihimiza wizara iharakishe kufungua kituo kama hicho Pemba ili kiweze kuwasaidia wananchi katika kupambana na kesi za udhalilishaji watoto.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nina imani kuwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu katika kuijadili ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii watakuwa na mengi ya kuchangia kutokana na umuhimu wa sekta hii ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya watu wa Zanzibar yanafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya awali ili na mimi niweze kutoa mchango wangu juu ya Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kabla ya kuanza kutoa mchango wangu naitumia nafasi hii kukupongeza sana kuteuliwa kuwa Mwenyekiti na leo umeanza kazi na ni matumaini yetu kwamba utatuongoza vizuri katika muda wako huu wote wa Uenyekiti wa Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii (Mhe. Amina Iddi Mabrouk) pamoja na Wajumbe wake wote wa Kamati na Makatibu wao wa Kamati kwa kuweza kufanya kazi za kamati kwa muda wa wiki nne kama walivyoeleza Unguja na Pemba, na hatimae leo wameweza kuwasilisha ripoti yao hapa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizi za kamati ni muhimu na ni moja kati ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza kuangalia utekelezaji wa shughuli za kila siku za serikali. Kwa hivyo, kupitia kamati Waheshimiwa Wajumbe wanapata nafasi ya kupitia katika wizara mbali mbali na taasisi zake ili kuona utekelezaji wake na hatimae leo kuwasilisha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizi za kamati ni muhimu sana kwa wenzetu wa serikali, kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wanapata nafasi ya kwenda moja kwa moja kwa walengwa. Mhe. Mwenyekiti, utaona kwamba ripoti hizi zinajadiliwa na hatimae zinapitishwa. Lakini ripoti hizi zitaweza kuwasaidia sana Waheshimiwa Mawaziri hasa wakati wa vikao vya bajeti, na kwa sababu wakati huo tena hakuna hoja za kupitisha kirahisi kama leo tunavyopitisha kamati.

Kwa hivyo, niiombe serikali sana kuwa makini na kuziangalia hizi taarifa za kamati kwa sababu utekelezaji wake utaweza kutusaidia sana wakati wa vikao vya bajeti. Ndio maana Mhe. Mwenyekiti, siku za mwanzo ilikuwa ripoti hizi za kamati zilikuwa zinabakia hapa katika Baraza, lakini kwa kuona umuhimu wa ripoti hizi ndipo Waheshimiwa Wajumbe wakapendekeza kwa Baraza

kwamba ripoti hizi ziwasilishwe katika wizara mbali mbali ili kuona namna ya taarifa za kamati na juu ya utekelezaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii imeeleza mambo mengi kupitia wizara zake, wizara tatu ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupitia ripoti hii kuna mambo mengi, ripoti hii imesheheni mambo mengi sana kuna changamoto, kuna mafanikio, kuna ushauri na mambo mengine ambayo wenzetu wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wameyaona. Lakini mimi nimechukua tu baadhi ya maeneo na kwa sababu ningeweza kuanza kuchukua maeneo yote tungeweza kufika mpaka asubuhi hapa, lakini nimechukua baadhi ya maeneo ambayo yamenigusa ili niweze kutoa mchango wangu naamini na wajumbe wenzangu nao watayaona yale yaliyowagusa na hatimae tutakamilisha ripoti yetu kamili. Kwa hivyo, kwa kuanzia nianze na Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini uhaba wa wafanyakazi katika Kitengo cha *I.C.U* na wametueleza katika ripoti yao kwamba chumba cha *I.C.U* hakina mitungi ya *oxygen* ya kutosha na badala yake kuna mtungi mmoja ambao unatembezwa katika vitanda vyote, imekuwa kama vile vikao vya wanywaji wa pombe mtungi wa pombe unawekwa kati kati kwa hivyo bakuli linapitishwa kwa kila mtu. Kwa hivyo, imekuwa kama hicho kitengo chetu mtungi mmoja umekuwa ukitembezwa katika kila kitanda.

Mhe. Mwenyekiti, jengine wametueleza kwamba kuna kitu hapa wamekiita *monitoring system*, sisi hatuelewi sio wataalamu wa afya. Lakini kitu hiki ambacho kina wapimia wagonjwa waliokuwa mahatuti mapigo yao ya moyo lakini chombo hiki hakifanyi kazi, hiyo ni hatari.

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha *I.C.U* hata hili jina lake ukilisikia wewe mwenyewe unashtuka kwamba ni pahala ambapo pana shughulikia uhai wa mwisho wa binadamu na pale hapelekwi mtu wa ovyo ovyo tu kwenye wodi, anapelekwa mtu ambaye hali yake ni mbaya anahitaji kupata msaada wa mwisho. Mhe. Mwenyekiti, leo inasikitisha wenzetu wa Wizara ya Afya kwamba kitengo hiki hawajakipa umuhimu unaotosheleza, pengine kutakuja ile dhana kwamba tunaukosefu wa fedha na kwa sababu ndicho kichaka chetu tunachojifichia mara zote. Mhe. Mwenyekiti, tukishakuwa na matatizo yetu kichaka chetu cha kujifichia ni ukosefu wa fedha, lakini wakati mwengine kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati mambo mengine hayahitaji ukosefu wa fedha, ni mambo ambayo yanaonesha uwajibikaji mbovu katika shughuli zetu za utekelezaji wa kila siku.

Kwa hivyo, kitengo hiki ni muhimu na nimuombe sana Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha aweke miundombinu hii ambayo wagonjwa ambao wanakuwa na hali mbaya wanahitaji kupata matibabu ya dharura pale, basi waweze kupata mahitaji yote yanayostahiki. Mhe. Mwenyekiti, sisi wakubwa tunapougua huwa tunakimbizwa pengine Muhimbili, pengine Ulaya huko lakini wananchi wetu waliokuwa hawana uwezo kwa kwenda katika maeneo hayo pale ndio Ulaya yao. Kwa hivyo, kitengo kile kitengenezwe vizuri na nimuombe sana Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha kama kuna tatizo la fedha, basi tuwape wenzetu hawa ili wakamilishe hizi taratibu kwa sababu hapa ndipo penye uhai wa wananchi wetu na serikali hii lazima tukumbuke kuwa ni ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi viongozi tupo lakini kwa niaba ya wananchi kuanzia Mhe. Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote tupo kwa niaba ya wananchi na kwa mujibu wa katiba yetu inavyotuelekeza. Kwa hivyo, hili jambo sio la kulidharau, kitengo hiki ni muhimu kinahitaji kiwe kinakwenda na wakati na kisiwe na mapungufu juu ya vifaa vyake. Kama tutakuwa katika hali hii basi tunaweza tukapoteza maisha ya wananchi wetu hivi hivi bila ya taratibu ambazo zinahitajika. Kwa hivyo, hilo ni kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii imezungumzia kuhusu fedha zinazotolewa kwa wazee waishio nyumba za wazee Sebleni ambapo kwa mwezi wazee wetu ambao tumewaweka pale tunawalipa sh. 25,000/= kwa mwezi. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hebu tuziangalie sh. 25,000/= kwa mwezi unampa mtu mzima uliyemuweka pale umemuahidi kumuhifadhi pale, hana baba, hana mama kwa mwezi unamlipa pesa hizo nilizozitaja hivyo atazitumia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tujiangalie sisi halafu tuwaangalie na wao, wale ni watu ambao wanachukuliwa na serikali, hawawezi kulima, hawawezi kupata rizki yao pahali pengine popote hivyo wanategemea fedha zile ambazo wanapewa na serikali sh. 25,000/= na wakati huu mgumu kwa kweli kiwango hiki wanachopewa wazee wetu wale tena wako 65 tu, wala sio wengi wanaoishi katika Nyumba za Wazee Sebleni hakitoshi kinahitaji kuongezwa, tena kiongozwe zaidi ya asilimia mia moja, pengine ingekuwa ni vyema na wao serikali ikawapa kima cha chini cha mshahara. Kwa sababu huku sisi tukilalamikia kima cha chini cha mshahara cha shilingi laki moja Waheshimiwa Wajumbe wenzetu wazee tuliowaweka pale hawana uwezo wanapata shilingi 25 elfu kwa mwezi, hawana baba, mama, ndugu, baba yao serikali, mama yao

serikali, tumewapa mpaka nyumba. Kwa hivyo, wale ni wazee wetu ambao tumewaweka pale.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kuona wazee wale sasa wamekuwa omba omba, wanapita katika maduka wanaomba, wakimkuta mtu wanamuomba na kwa sababu inalazima hivyo kutokana na kiwango hiki kidogo cha fedha wanachopewa. Sasa nimuombe Mhe. Waziri katika bajeti hii inayokuja kama nilivyotangulia mwanzo uje na kauli nzuri hapa ilibajeti yako ije ipite kwa urahisi. Nimuombe sana na Mhe. Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo amuongezee fedha Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ili wazee wale 65 tu wala sio wengi waweze kupata fedha angalau kupata ule mlo mmoja kwa siku waweze kuishi kwa raha mustarehe kama tunavyoishi sisi wajumbe wako Mhe. Mwenyekiti.

Katika taarifa ambayo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ametueleza hapa, anaeleza kwamba kuna mradi wa udhibiti wa wazee ambapo kuna ukarabati wa paa la nyumba la wazee lililoanguka Sebleni. Mimi ninaipongeza sana wizara na serikali kwa kuanzisha mradi huu ambapo sasa hivi *Alhamdulillah* jengo lile ambalo limeungua moto kiasi cha miezi miwili iliyopita limeweza kufanyiwa ukarabati. Naipongeza sana serikali, nimpongeze Mhe. Waziri, nimpongeze pia Mhe. Waziri wa Fedha kwa kukubali kutoa pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jengo lile.

Lakini mbali na kufanya ukarabati, ripoti imeeleza kwamba, wizara mwaka huu wa fedha 2011/2012 imekadiria jumla ya shilingi 640 milioni kwa ajili ya ukarabati wa majengo na kuzungusha ukuta wa Nyumba za Wazee Sebleni. Hizi ni taarifa njema Mhe. Mwenyekiti, na kama kutakuwa na jambo hili kweli basi litakuwa ni ukombozi wa wazee wale wasiojiweza ambao tumewaweka katika nyumba zile. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nyumba zile ziko katika hali mbaya hilo wala halina ubishi, ni nyumba zilizojengwa muda mrefu, ni nyumba ambazo zina matatizo, baadhi yake zinavuja, masilingi yananing'inia, waya za umeme zinaning'inia, uhifadhi wao umekuwa mgumu, wezi wanaingia kwa sababu hakuna ukuta, wengine wamezifanya ndio kona za kumalizia mambo yao. Kwa hivyo, nyumba zile zimekuwa ni eneo ambalo lipo lipo tu katika lugha ya kileo.

Ukienda pale Mhe. Mwenyekiti, mifugo ya ng'ombe au mbuzi imezagaa ovyo katika nyumba zile. Kwa hivyo, ile dhana ya uhifadhi wa wazee imekuwa haipo. Sasa naamini sana, kwa kuwa lengo la wizara ni kutenga kiwango hiki cha fedha, ingawaje hakiwezi kutosha kwa wakati mmoja lakini tutapata pa kuanzia. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha akubali fungu hili litumike kwa ajili ya kufanya haya ambayo wenzetu wa Wizara ya Ustawi wa Jamii wameyakusudia. Kwa sababu wazee wale kama nilivyosema mwanzo

tumewaweka sisi wenyewe kwa hivyo ni wajibu wetu kuwashughulikia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nisichukue muda wako mwingi nije sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kumalizia. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na wao wana changamoto nyingi, changamoto moja ni ukosefu wa walimu wa sayansi. Lakini katika ripoti hii imetueleza kwamba, tayari wana mipango mbali mbali kabambe juu ya kuhakikisha kwamba walimu hao wanapatikana kwa wingi.

Mimi niwapongeze, Mhe. Mwenyekiti, skuli yangu ya sekondari ya Nyerere haina walimu wa sayansi na ni skuli ya sekondari. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Elimu mipango hii aliyoikusudia aitimize ili tuone kwamba tunapata walimu wa sayansi na hesabati wa kutosha kwa ajili ya watoto wetu.

Lakini pia kuna ukosefu wa vifaa vya maabara. Leo inasikitisha kuona kwamba skuli ya sekondari haina vifaa vya maabara ambavyo vitawawezesha watoto kufanya mafunzo yao kwa vitendo, na vijana hawa tunawategemea sana katika masuala mbali mbali kama mtihani na mambo mengineyo.

Skuli yangu ya sekondari ya Nyerere haina hata ile *test tube* moja ambayo watoto unaweza kuwauliza hiki kitu gani akakwambia. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, tunajua azma ya kutekeleza haya anayo lakini ajitahidi ili kuona kwamba skuli zetu za sekondari zinakamilika na zinakuwa na vifaa vya kisasa ili kuona kwamba watoto wetu wanasoma katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi naikubali ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naiunga mkono pamoja na changamoto nyuingi, lakini kwa kweli inahitaji kufuatiliwa ripoti hii, serikali inahitaji kuifuatilia kwa makini ili tuone mabadiliko katika kipindi kijacho. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuumba na kutuweka hai wakati huu tukawa tunapata ile pumzi ya kupumua kwa dakika. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kutoa taarifa zake nzuri zenye mwelekeo na zimekwenda kwa wakati ambao sasa hivi ndio wakati tunaoutaka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kuchangia katika Wizara ya Afya. Wizara hii nina historia nayo nzuri sana hivi nikikaa hapa naliona lile jengo lilivyo. Mara nyingi sana mimi Waziri wa Afya nakuwa sipendi kumlalamikia hata kidogo, kwa sababu hana uwezo, hana nyezo, waziri naamini na hasa huyu wa sasa hivi aliyekuwepo kama laiti angelikuwa ana nyenzo basi naamini wizara hii ingekuwa na lile jina la rufa basi lingekamilika, kwa ile hamu aliyokuwanayo.

Lakini waziri hana kitu, atafanya nini waziri?hali halisi ilivyo wagonjwa wanazidi kurundikana, leo lakusikitisha Mhe. Mwenyekiti, zaidi kuwa hata wale ma-*expert* hatunao kabisa wanatukimbia, na yeye sifikirii kama anawafukuza, hawafukuzi lakini hana cha kuwapa, atakaanao vikao vingi zaidi ya 50 atayozungumza ni yale yale. Lakini angekuwa anawezeshwa Mhe. Waziri basi naamini wataalamu wote wangekuwa wameshakuja hivi sasa. tumepiga kelele sana jamani tuwawezeshe hawa madaktari wetu ili waweze kukaa, leo Bara wanalipwa fedha nzuri tu, 1.5 asikimbie hapa, leo ukiambiwa *expert* analipwa shilingi laki tatu kama nitakosea waziri samahani utanirekebisha kweli atakaa hapa?

Lakini mimi nimefurahi kwa kuwa Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye ni kijana maridadi kabisa ni mtu ambaye amekaa kule ameona mazingira ya wenzetu kule Bara naamini ana-*quote* na sasa hivi *Alhamdulillah* tumeona jinsi gani waziri anavyoanza kuleta neema zake na naamini wizara hii sasa ataisaidia, nina asilimia kubwa.

Juzi nimekwenda nimekuta mlango mzuri tu *lift* ambapo *lift* siku zote naisema hii, *lift* ni muokozi wa wagonjwa. Waziri hivi sasa anafanya vitu vyake, leo *lift* ya upande wa pili inafungwa vizuri na hivyo ndivyo neema tunavyoitaka. Kwa sababu leo mtu mzito kwa mfano, Mwenyezi Mungu anistiri hivi hivi nisiumwe lakini mimi nina kilo 110 nani ataweza kuninyanyua? Sasa hili ni moja ambalo nimelipigia zogo mpaka leo *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu atujalie sasa *lift* ipo.

Nimezungumza suala la chumba cha mahututi utasema kama mimi nalala mle nakijua juu chini. Mhe. Mwenyekiti, chumba cha mahututi leo anawekewa mtu feni la juu, tunamuuguza tunammaliza? Hebu tutizame ndani humu sasa hivi, ubaridi mwepesi kabisa inajenga rutuba, leo yule anawekewa pangaboi tupu linabeba hewa chafu inampelekea yule mgonjwa badala ya ule umahatuti aliokuwanao unamuelekeza kuwa aendelee kufa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu ambavyo kidogo nimevisahau leo sikuvaa miwani, lakini kuna vitu ambavyo yule anayekaa pale kwenye chumba kile kuna mashine za kuangalia jinsi gani mwenendo wa yule mgonjwa unaoendeshwa na kujua, leo hakuna. Kuna kitu kidogo pale karibu na yule mgonjwa kila mara

ende akachungulie pale na utakuta mhudumu ndani ya chumba kile ni watu wawili tu, pengine kuna siku nyengine kuna zaidi ya wagonjwa watano na wagonjwa wale wanatakiwa kila mara waangaliwe *condition* yake ikoje, hakuna vitu hivyo. Leo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri ana mzigo mzito sana kwa hospitali kila siku tutamlaumu, kumbe si pahala pake pa kulaumiwa.

Tukija kwenye *CT Scan* leo utakuta ina wafanyakazi wawili tu, mmoja keshakwenda kusoma sasa hivi na huyo rabi rabi nafsi mguu majanini mguu njiani pesa ziko wapi? Mhe. Waziri wa Fedha msaidie Waziri wa Afya, huyo kijana bwana kwa vyovyote itakavyokuwa asirudi kwa ajili ya fedha. Mimi nakujua wewe *paly boy* lazima utamsaidia huyo, hali ngumu ule ukweli tuuseme jamani, hali ngumu sana ya *CT*. Kwa sababu *CT* ni moja katika kujiangalia katika *frame* yako ya mwili tatizo lako. Zamani tulikuwa tunaifuata Bara shilingi laki mbili, leo Zanzibar shilingi laki moja tu, tena inategemea kama kuna ongezeko la dawa nyengine inakuwa shilingi lako moja na nusu ni *very cheaper* kabisa.

Sasa hii kwa kweli ni suala ambalo nampa pongezi Mheshimiwa wangu babu, lakini hapo hapo nampa pole kabisa. Kwa sababu ni kitu ambacho wizara hii ni ngumu sana.

Tukija kwenye wodi kuanzia ghorofa ya kwanza, ya pili mpaka ya tatu. Leo mimi nilikuweko huko huko utasema ndio waziri wa afya mwenyewe. Wodi nambari moja kwa kweli kuna wafanyakazi kidogo sana, hatukuwa na ile *International Nursing*, hatukuingia kabisa tunafanya mambo yetu ya Kiswahili tu. Kwa sababu utakuta *nurse* mmoja na *ordarly* mmoja niambie wodi ile ina wagonjwa wangapi? Nalo hili jamani tuongezeni ajira, tukiweka ajira vizuri pale basi nafikiria babu yangu Juma atakuwa katika hali nzuri sana na mshahara ukawa juu zaidi, sio tuongeze ajira halafu mshahara wenyewe ukawa chini aa, nawatetea *nursing*, *ordarly* pamoja na madaktari mshahara bado haukidhi haja.

Tunaingia katika Hospitali ya Mapinduzi Mpya. Mhe. Mwenyekiti, Mapinduzi Mpya haina hadhi, siku moja mimi nilimpigia Mhe. Waziri nikamwambia niko mimi hapa sasa hivi Mapinduzi Mpya lakini uso wangu umezama juu naona mpaka mbingu naziona na nimo ndani ya chumba, ile kangriti inabanduka, haioneshi hadhi ya Mapinduzi kusema kuwa anawekwa waziri. Mhe. Waziri wa Fedha zuia mawaziri wasiende kujitibu nje wajitibu hapa, hilo nasema zuia, watapokuwa wakilala pale Mapinduzi Mpya itakuwa na *standard* yake. Lakini leo ukucha tu, Dar es Salaam au Ulaya, zuia fungu hilo wape wanyonge, wakwenda Ulaya wanyonge kwa sababu hawana uwezo, mnyonge leo atajitibu

wapi *pressure* ana uwezo wa kwenda pahala? Sasa mnyonge ndio apelekwe kule.

Kwa kumalizia wizara hii kwa kweli nasema kuwa Mwenyezi Mungu ambariki sana Mhe. Waziri wa Afya na *Inshaallah* ataiweza kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Jengine katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Na yeye nimshukuru sana Mhe. Waziri amefuata nyayo zile zile alizokuwa akipita waziri aliyeondoka ni vile vile, mpaka sasa hivi hakuna tofauti yoyote, si mbishi na ndivyo inavyotakiwa. Lakini zaidi tunachokitizama sasa hivi walimu wa sayansi na hili siku zote linasemwa. Tunamuomba suala hili aliendeleze kulichukulia kipaumbele cha hali ya juu kabisa.

Mwenzangu amesema suala la maabara. Mhe. Waziri ninavyokujua kwa jitihada zako na hasa mwenyewe ulivyokuwa mtu wa elimu toka asubuhi ulikuwa ukiitwa maalim, basi nafikiri vitu hivi unaweza kuvikamilisha kwa kupitia bajeti yako ikiwa kubwa atakusaidia Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo nimesahau, sikutaka kurejea lakini nimesahau kwenye kitengo cha macho. Katika kitengo hiki juzi nilipeleka wagonjwa kufanyiwa operesheni ni aibu, kitengo kidogo kile hakifai sasa hivi, wanakopa au wanakwenda kuazima katika wodi nyengine kwa kuwafanyia watu operesheni wawangojee kule halafu wawachukue inakuwa ni aibu. Mgonjwa unamtoa meli moja unampeleka meli tano kwenda kumlaza. Kwa kweli hii ni *affect* kubwa sana, naomba waziri muhusika awapatie kiwanja hawa watu wa kitengo cha macho ili waweze kupata mfadhili kuwajengea sehemu yao ya kfuanya operesheni vizuri na wawe na jengo la kisasa.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza nimsifu Mhe. Waziri kwa jitihada zako na leong la kutaka kufikisha pale ulipokusudia. Lakini Mheshimiwa matatizo yamekuwa mengi katika maeneo yetu, unajua kwenye ripoti mambo mengine yanakuwa hayamo, mengine inabidi tusaidie kama hivi tunavyosaidia.

Mhe. Waziri juzi hapa tulizungumzia suala la watoto kupotea, hili kwa kweli tunaomba ulitilie mkazo mkubwa sana, kwa sababu kupotea kwao wao ndio sehemu moja ya kubakwa. Watoto wanapotea vibaya sana, wengine wanapotea kwa mazingara ya Kiswahili lakini wengine wanapotea kwa mtu kufanya ufisadi tu, amchukue mtoto wa kike tena ndio moja kwa moja. Zamani ilikuwa watoto wa kike lakini sasa hivi mpaka wanaume wanapotezwa.

Mhe. Waziri mimi ushauri wangu kuwa ujenge sasa hivi na hawa watu wa sheha kuwe na maafisa ambao wanaweza kupitia kwa masheha ili kuweza kupata *data* za uhakika na nini uweze kufanya ili kupunguza hii hali. Kwa mfano, hivi sasa wenzetu polisi wameamua kufanya polisi jamii, kwa kweli hili ni jambo zuri sana Mheshimiwa, sasa na wewe ungeweka mtindo kama huu, rai kama hii, basi naamini kwenye shehia zetu lingeweza kuondoka.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba niwashukuru mawaziri wote pamoja na mwenyekiti wa kamati hii kwa utaalamu mzuri na kuleta ripoti kama tulivyosema kuwa kamati zina umuhimu wake kwa mawazidi na kwa kanuni. Kwa hvyo machache naunga mkono kwa asilimia 99 ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuichangia Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Mimi kwanza nianze kwa kukupongeza Mhe. Mwenyekiti kwa kukikalia kiti chako leo na naamini utatuendesha vizuri kama wanavyofanya wengine, Naibu Spika, Mwenyekiti mwenzako ambaye tayari amekikalia kiti hicho.

Pili nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati wa ripoti hii na wajumbe wake wote kwa ripoti yao nzuri ya kina ambayo wameitoa hapa. Kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin mambo yako mengi kwa hivyo kila mmoja nadhani atapata nafasi ya kusema yale machache ili wajumbe wengi waweze kupata nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na haya yafuatayo: Kwanza katika Wizara ya Afya. Naomba nianze na mimi kwa kuupongeza sana uongozi mpya wa Wizara ya Afya kuanzia waziri na naibu waziri wake kwa kazi nzuri ambayo wanaonekana wameifanya na wanaivalia njuga kuona kwamba wanayapatia ufumbuzi matatizo ambayo yamekuwa yakikabiliwa na hii wizara kwa muda mrefu sana. ushahidi wa hata ni ziara ambazo waziri na naibu waziri wamezifanya katika hospitali na vituo vya afya takriban vyote Unguja na Pemba katika kipindi kifupi tu hiki tangu wameteuliwa. Hiyo ni kuonesha *commitment* yao ambayo wanayo katika kuona kuwa wanayatambua matatizo ili wapate kuyatatua.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mbali ya pongezi za jumla niwapongeze pia kwa kazi nzuri hususan Mhe. Waziri aliyoifanya iliyopelekea hatimaye kuhakikisha Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ambayo imo ndani ya Jimbo la Mji Mkongwe inapata huduma ya maji sasa kwa ubunifu wao wenyewe. Kukosekana kwa maji katika hospitali hii kwa muda mrefu kulikuwa kunaathiri huduma nyingi sana pale. Kwa hivyo, kwanza hilo nataka niwapongeze.

Lakini baada ya pongezi hizo na mimi niendelee kutilia mkazo suala la umuhimu wa kuimarisha huduma katika chumba cha *ICU* au chumba cha wagonjwa mahututi pale katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mweneykiti, mimi nimebahatika karibuni kama mara mbili kwenda pale kwa sababu kulikuwa na wagonjwa ambao walilazwa na unaiona hali yake ilivyokuwa mbaya, kuanzia hiyo ya mitungi ya *oxygen*, lakini pia kama nilivyosema *monitoring system* pale ambayo katika chumba cha *ICU* ni kitu muhimu mno. Kwa sababu ndicho kinacho-*monitor* ile hali ya mgonjwa anavyoendelea. Kwa hivyo, kinahitaji kuimarishwa.

Lakini pia hata idadi ya wauguzi ambao wana mafunzo maalum ya kuhudumia katika chumba kile, unaweza kuingia pale ukakuta kuna mhudumu mmoja au wawili, lakini wanapaswa kuwahudumia wagonjwa wote waliokuwemo mle ndani ambao ni wengi. Kwa hivyo, nasema kuna haja sana ya kukiangalia chumba hicho cha *ICU* ili kuimarisha huduma zake.

Pili Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine hili kamati imepongeza hatua zinazochukuliwa toka huko mwanzo za kutangaza huduma za matibabu kuwa ni bure. Lakini ikasema kutokana na hali ya uchumi inavyoendelea katika nchi yetu inapelekea kulazimika kuwataka wananchi wachangie huduma hizi.

Sasa bila shaka wananchi wetu wanachangia lakini wengine uwezo wao kama inavyosemwa ni mdogo. Moja katika malalamiko ya wananchi wetu wengi sana Mhe. Mwenyekiti, ni suala zima la gharama katika kupata huduma ya *CT Scan* ambapo wanatozwa shilingi laki moja. Inawezekana shilingi laki moja kwa baadhi yetu tukawa tunaimiliki, lakini tukizingatia kwamba katika nchi yetu shilingi laki moja ndio kima cha chini cha mshahara, maana yake unamwambia mwananchi yule wa hali ya chini asiweze kuimudu huduma hii.

Sasa hivi imesogezwa hapa Zanzibar, lakini zamani ilikuwa haipatikani kwa sababu ilikuwa ni ghali na vigumu kuifuata Dar es Salaam. Hivi sasa ipo hapa, lakini bado wananchi wanashindwa kuitumia na utakuta mtu akiambiwa mgonjwa wake anahitaji huduma hii anaanza kutanga tanga mitaani kwenda kuzitafuta shilingi laki moja ili mgonjwa wake aweze kuhudumiwa. Najua kumewekwa utaratibu wa kusema kuwa, kuna baadhi ya watu kutokana na hali zao wanaweza kufikiriwa wakapewa huduma hii bila ya malipo, lakini inaonekana kutokana na utendaji ulivyo pale hii huduma kupatiwa bila ya malipo imekuwa ni kazi kubwa kweli kweli. Naomba hilo Mhe. Waziri alitizame.

Mhe. Mwenyekiti, pia kumekuwa na malalamiko kwa wananchi sina hakika kama yana ukweli, lakini baadhi ya wananchi wanalalamika kwamba mara nyengine pia hakutolewi stakabadhi unapokwenda kufuata huduma hii

kutokana na malipo hayo. Sasa fedha hizi zinaishia wapi kama madai hayo ni ya kweli? Inapaswa pia uongozi wa wizara ulitizame kwa umakini suala hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara ya Afya ni suala zima la wagonjwa ambao wanahitaji kupelekwa nje ya nchi wale ambao maradhi yao hayawezi kutibiwa hapa Zanzibar au pengine hata Bara. Wagonjwa wale wanaoelekezwa na madaktari kwamba wanahitaji kupelekwa nje ya nchi na mara nyingi wanapelekwa India, lakini hivi sasa tunaambiwa kuna orodha ndefu ya watu ambao wanatakiwa kupelekwa huko inashindikana kutokana na ukosefu wa fedha. Taarifa nilizonazo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara ya Afya inadaiwa takriban dola laki mbili, elfu nne mia sita na sitini na tisa katika Hospitali ya Miot, India ambako ndiko kunatolewa huduma hizo. Sasa hii inapelekea kushindwa kupokea wagonjwa wengine kutoka kwetu na kuwahudumia.

Kwa hivyo, nilikuwa nadhani kwanza wizara hii ya rafiki yangu mpenzi Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo (Mhe. Omar Yussu Mzee) asaidie kulisafisha hili deni ili tuweze kupeleka wagonjwa wengine. Kwa sababu wanatokea wengine ambao bado wanahitaji huduma hizi na sisi kama nilivyosema hapa hatuna uwezo wa kuzitoa, hivyo ikifikia hali hiyo waweze kupelekwa. Kwa hivyo, nadhani kuna haja ya wizara kusaidiwa ikalilipa deni lile ili tuweze kuendelea kuwapatia huduma wananchi wetu.

Sambamba na hilo hizi huduma za kupata madaktari mabingwa kutoka nje wanaokuja hapa tuziimarishe, pengine kuna haja ya kuendelea kutafuta utaratibu wa kuzichukua hospitali zetu hapa na kuzitafutia hospitali rafiki za nje zikawa zinabadilishana uzoefu wa madaktari, vifaa na misaada kama hii ili kuziongezea nguvu angalau mambo kama haya madogo madogo yaweze kufanyika hapa hapa na kupunguza mzigo wa kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Lakini wakati haya Mhe. Mwenyekiti, yanaweza kuonekana kwamba ni mambo labda makubwa, kuna moja ambalo tunaliona ukifika hospitali pamoja na hii Hospitali Kubwa ya Mnazi Mmoja, ambalo ni *basic* tu na uongozi wa wizara nadhani unapaswa kulifanyia kazi. Nalo ni taratibu mzima wa kuanzia kupokelewa mgonjwa mpaka kupatiwa matibabu. Unapopeleka mgonjwa na karibuni mimi mwenyewe nilishiriki kama mara mbili kupeleka wagonjwa mahatuti pale mtu alipata ajali, lakini inaonekana kuanzia mapokezi mpaka wauguzi hata zile taratibu si nzuri. Tunajua kuna uhaba wa wauguzi, mnaambiwa pengine nyinyi wenyewe mnaouguliwa msaidie pale, lakini unaweza ukaambiwa umpeleke chumba cha *X-ray*, akisha pigwa *X-ray* mnaambwia mpelekeni juu, mnampeleka juu mnaambiwa kuna nini sijui mrudisheni tena *X-ray*, *yaani* ni kama vile hakuna taratibu zinazoeleweka.

Ukimpeleka huko *X-ray* unaambiwa mimi sipigi mpaka nipate *instruction* ya daktari fulani. Sasa *instruction* mimi nitaijuaje? Ilikuwa huyo aliyenambia nimlete hapa ndio anipe hiyo, kama kuna maelekezo au maandishi, hakuna taratibu, unaambiwa huyu kutokana na hali yake mrejesheni juu lakini moja kwa moja mpelekeni *theatre*, unamchukua unampeleka unaambiwa subiri kwanza.

Kwa hivyo, inaonekana kama vile hakuna taratibu zinazoeleweka za mgonjwa akifika katika hali gani, anapokelewa vipi, anakwenda hatua ipi mpaka kufikishwa. Kwa mfano, kama anahitaji upasuaji kufikishwa katika chumba cha upasuaji hatimaye amalizikie katika wodi ni kama vile kila mmoja anafanya kazi kwa kubahatisha. Inawezekana kutokana na mazingira magumu wanayofanyia kazi wanachoka na ndio maana hizi taratibu zinakuwa hazieleweki. Lakini nadhani hili ni suala la msingi sana kwa hospitali kwamba inajua taratibu, sisi wengine tukisafiri tunakagua marafiki zetu hospitali za nje tunaona, ukifika unajua hupati tabu kwamba hatua ya kwanza ni hii, ya pili ni hii, mpaka unafika mwisho, hapa kwetu utakuta kuna *confusion* kubwa sana. Kwa hivyo, naomba na hili pia ifatiliwe.

Kwa wizara hii la mwisho niseme ambalo limesemwa na baadhi ya wajumbe hapa hili suala la mafao au stahiki za wafanyakazi katika sekta hii, kuanzia madaktari, wauguzi mpaka odali. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha katika eneo ambalo anapaswa alipe umuhimu mkubwa katika bajeti yake itakayokuja baadae mwaka huu, basi alitazame hili kwa umuhimu mkubwa sana.

Dunia nzima inafanya kila juhudi kuwavutia madaktari na wauguzi kwenda katika nchi zao, kupata ajira katika ulimwengu wa Magharibi ni shida sana, lakini ukiwa daktari, ukiwa muuguzi kwenye sehemu zinazotakiwa hupati tabu kupata kazi. Tunawaona vijana wetu wengi wanaokwenda kule wanakuwa wanapembejewa wabakie pale, kwa sababu kila nchi inawahitaji hawa, sasa sisi tumewasomesha lakini kutokana na mafao, stahili, mishahara midogo wanaondoka. Sasa nadhani hili pia tulitazame, huu utaratibu kwa madaktari bingwa tunamlipa shilingi laki tatu kwa mwezi hawezi kubaki daktari wataendelea kutukimbia kila siku. Kwa hivyo, nadhani hili pia lipewe umuhimu wake mkubwa sana, badala ya kuelekeza nguvu kwa wanasiasa tu, pia tutizame sasa haja ya kuongezea mafao yanayostahili kwa wafanyakazi wetu hasa hawa profession wanaofanya kazi katika maeneo kama haya.

Nikimalizia hilo Mhe. Mwenyekiti, niingie kwa ufupi katika wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Katika wizara hii kwanza nadhani suala moja kubwa sana la kutizamwa hapa, pametajwa matatizo mengi lakini nmoja ambalo naliona mimi ni kwamba tumejitahidi sana kuongeza *structure* katika Wizara

ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama vile madarasa, kujenga skuli mpya. Nadhani sasa wakati umefika kwamba hapa kwanza labda tungefanya kazi ya kuongeza *quality* sasa badala ya *quantity* kabla ya kuongezea skuli nyengine na vyuo vyengine.

Kwa sababu tunakuta tunaongeza majengo, lakini uwezo wa kuhudumia hatuna na matokeo yake ndio maana *performance* ya skuli za Zanzibar ukilinganisha na skuli za Bara katika mitihani ya taifa kila siku inakuwa hairidhishi. Kwa hivyo, nadhani kuna haja ya kutoa msukumo maalum katika suala la *quality*.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka kuzungumzia suala la walimu. Ripoti ya kamati imezungumzia hususan upungufu wa walimu wa sayansi na katika hili imesemwa kwamba Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kinaanzisha kozi ya stashahada kwa ajili ya walimu wa sayansi. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hilo peke yake halitoshi, unaweza ukaanzisha kozi hiyo ya kutoa stashahada lakini utawapata wanafunzi wachache sana wenye uwezo watakaotaka kujiunga na fani hii ya ualimu kwa sababu ile ile kama niliyozungumza katika sekta ya afya ya maslahi madogo unapofanya kazi katika sekta hii.

Kama unataka kuipa umuhimu mkubwa sekta ya elimu basi pia ni lazima tuangalie maslahi wanayoyapata wafanyakazi hasa walimu katika sekta hii ya elimu, ili kuwavutia watu kwenda kusomea huo ualimu katika fani ya sayansi na baadae kuja kubakia kufanya kazi katika sekta hii.

Kwa hivyo, nadhani tusizungumzie tu kwamba chuo kikuu kinaanzisha kozi hii lakini kipi kitawavuta wanafunzi wetu wenye uwezo mzuri. Badala ya kwamba sasa kila mwanafunzi ambaye kakosa fani nyengine zote ndio tena anachukua ualimu, iwe kwamba chaguo lake la mwanzo linakuwa ni katika fani ya ualimu, ili kunyanyua elimu tukitambua kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi yoyote duniani.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili pia kuna *concern* nadhani ni muhimu kuizungumzia hapa kwamba Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)* namna kilivyoanza sivyo kilivyo leo. Hata watu waliokuwa mwanzo wamevutiwa kuja kufanya kazi pale wakiwemo wahadhiri sasa wanaanza kupunguza *interest* kwa sababu ya hali halisi ya uendeshaji na mahitaji yake. Pengine tungefanya uamuzi wa kisiasa wa kuona vyuo vikuu kikiwemo cha taifa lakini baadae tunashindwa kufanya maamuzi hivi sasa yakinifu ya kuki-*support* na kukiendeleza Chuo Kikuu cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, chuo kikuu pahala popote huwezi ukakiendesha kama unavyoendesha skuli ya sekondari au chuo cha kawaida kwa maana ya *college*,

unahitaji mahitajio yake, wahadhiri wake malipo yao yanatakiwa tofauti na wafanyakazi wa kada nyengine. Nadhani kuna haja ya kuliangalia hili kwa makini ili isije ikawa ni aibu mwisho kwamba tumeanzisha chuo kikuu kwa kishindo lakini baadae kikawa kimeanguka hadhi yake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine linalohusiana na elimu ya juu ni suala la wale wanafunzi ambao wanalipiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika vyuo vya elimu ya juu vya hapa nchini. Moja katika tatizo sugu hapa ni kwamba wanafunzi wetu wanapelekwa huko lakini hawaingiziwi fedha ambazo wameahidiwa matokeo yake wanasoma katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nimelizungumza mara nyingi humu katika kipindi cha maswali na katika michango mingine, hata tulipokuwa tukichangia Mswada wa Kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Nadhani wakati tunasubiri sheria ile ifanye kazi kwa kipindi hichi bado wizara ilitazame hili kwa umakini mkubwa. Ule utaratibu wa kupeleka barua tu kwa wanafunzi wetu waruhusiwe kufanya mitihani wakati wizara inashughulikia lakini huduma nyengine hawazipati haiwatoshelezi wanafunzi wetu kufanya vizuri. Kwa sababu haiwezekani mwanafunzi anakosa yale mahitaji yake ya msingi tukategemea kwamba barua ya kumruhusu kufanya mitihani ikamuwezesha kufanya mitihani vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nilikuwa nataka kupendekeza kitu. Sisi mfumo wetu wa uendeshaji mambo katika nyanja nyingi tumeurithi kutoka katika mfumo wa Kiingereza kutokana na wakoloni walipokuwa wakitawala hapa. Moja katika jambo zuri lililokuwepo Uingereza hadi hii leo ni nafasi inayopewa kwa mtu anayeitwa *Chief Inspector of School* yaani Mkaguzi Mkuu wa Skuli. Humu katika ripoti ya kamati limetajwa hili, lakini tofauti ninayoiona mimi ni kwamba ripoti hii haichukuliwi uzito wake unaostahiki kwa sababu inaishia katika nyanja za utendaji serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kwa wenzetu Uingereza *Chief Inspector of School* anafanya kazi yake kwa kuzikagua skuli takriban zote zilizokuwa katika nchi ile na kila mwaka anatoa ripoti yake.

Kwanza anaiwasilisha hadharani badala ya kuipa wizara lakini baadae inachukua mjadala wa kitaifa, inawasilishwa hadi katika Bunge la Uingereza na inafanyiwa maamuzi kuanzia ripoti ya mkaguzi kama ilivyo ya mkaguzi mkuu kama ilivyokuwa na nyengine muhimu katika nchi. Inajadiliwa na kamati na baadae inajadiliwa katika Bunge kwa hivyo inapata kujua hasa matatizo ya msingi yaliyokuwemo katika sekta ya elimu ambayo kama nilivyosema ndio roho ya maendeleo ya nchi, ni yepi ili yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa nataka kupendekeza pengine si vibaya na sisi hapa Zanzibar tukaweka utaratibu kama huu kwamba *Chief Inspector of School* akawa anatayarisha ripoti yake na ripoti ile inatolewa hadharani inajadiliwa katika nchi. Inaletwa katika chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi ili wawakilishi kwa ujumla wao waweze kuitolea maoni na kuona ni maeneo yepi yanahitaji kupewa msukumo, ili kunyanyua sekta ya elimu katika nchi yetu na kwa hivyo kuweka msingi mzuri wa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya kamati na nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji miongoni mwa wajumbe wa kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mchango mfupi sana kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama wawakilishi tunapokwenda kuangalia katika taasisi za serikali tunajifunza mengi. Jambo moja ambalo tumejifunza kwa wizara zile tatu ni mashirikiano baina ya mawaziri na manaibu mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya yamekuwa makubwa ya hali ya juu. Sisi kama kamati tumejifunza kwamba mawaziri hawa na manaibu mawaziri wao wamekuwa na mashirikiano ya kutosha na kwa kweli wamejenga hadhi mbele yetu na mbele ya taifa hili la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama mjumbe wa kamati hii naomba kutoa wito kwamba wale mawaziri ambao wana manaibu mawaziri wao basi waige mfano wa Mhe. Ramadhan Abdallla Shaaban na Mhe. Juma Duni Haji jinsi wanavyowashirikisha manaibu mawaziri wao katika utendaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo tumejifunza ni kwamba tumeangalia *budget performance* ya wizara hizi tatu kwa ujumla haziridhishi. Upatikanaji wa fedha kwa wizara hizi tatu muhimu ni mdogo na haupendezi katika mtazamo wa dunia ya leo. Kwa hivyo, wito wangu kwa Wizara ya Fedha kwamba duniani kote nchi hizi zinawekeza kwenye elimu na afya. Lakini bado Zanzibar fedha katika wizara hizi muhimu zinakuwa mtindo huo sana, *budget performance* yake inakuwa ni ndogo sana. Kwa hivyo, ushauri wangu kwa serikali kwa jumla waongeze pato hili la wizara hizi kwa ajili ya kuwekeza katika masuala ya elimu na masuala ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mtazamo huo wa kijumla wa wizara tatu sasa niende kwenye wizara moja moja na nianze na Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, jambo moja ambalo kamati tumeliona ni makusanyo ya fedha pale

Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo yanatokana na huduma za matibabu na maegesho ya vyombo.

Mhe. Mwenyekiti, pale Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka jana iliagiza kwamba mapato yale yaliyotokana na huduma na maegesho ya vyombo yaingizwe katika mchakato wa kibajeti, ili *CAG* na *PAC* wapate kuyakagua kama fedha halali za mapato ya serikali. Kwa bahati mbaya wizara hadi hii leo haijatekeleza agizo lile.

Sisi kama kamati pia tumefuatilia halijatekelezwa na tumeagiza tena kwamba agizo hili litekelezwe katika mchakato wa kibajeti ili *PAC* wapate kukagua kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar. Sisi kama kamati tunaomba Mhe. Waziri wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto hili alifanyie kazi litolewe kwenye bajeti ili tuone uhalali wa makusanyo yale na matumizi yake.

Mhe. Mwenyekiti, hoja kubwa ni kwamba Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hawajapeleka washika fedha, hawajapeleka risiti, lakini fedha zinakusanywa hawasubiri risiti wala washika fedha. Kwa hivyo, tunachoomba utaratibu uandaliwe kuingiza fedha hizi katika mapato ya serikali kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo tumeliona Wizara ya Afya ni suala zima la fedha za wahisani. Bado kuna mawazo kwamba fedha za wahisani za miradi ya ukimwi pengine malaria na chanjo si fedha za umma. Baadhi ya wataalam wanaona kwamba hizo fedha ni fedha za wahisani wanaendelea na miradi kwa hivyo hazihusu kuangaliwa na Baraza la wawakilishi. Nadhani ni mawazo finyu kidogo, fedha yoyote ambayo inaingia hapa ni fedha ya umma, iwe ya mfadhili, iwe ya serikali.

Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba serikali hapa wajiangalie mapato yale yaliyokuwemo kwenye miradi ya ukimwi pengine na chanjo tuyaone katika bajeti ya serikali kwamba ni makisio na mapato ya serikali, ni *public money* kama ilivyo sheria.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala zima la *ICU*, hili naomba uturuhusu turejee tena kwa sababu ni suala muhimu. Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanaposikia *ICU* wanafahamu kwamba ni hatua ya mwisho ya kumuokoa mgonjwa. Sisi tumekwenda katika kamati na tumeona kwamba kile chumba hakifai kuwa *ICU*, tumeona kuna vitanda sita kwa wagonjwa sita na muuguzi mmoja, mtungi wa hewa ya *oxygen* ni mmoja, *monitory system* hamna. Kwa hivyo, chumba cha *ICU* hakina sifa. Maana yake ukitaka kumuangalia mgonjwa kwamba yuko

hai unampelekea mkono puani je, yuko hai au amefariki, hiyo si *ICU*. Sasa hakuna tofauti ya mgonjwa aliyekuwepo *ICU* na yule aliyekuwepo nyumbani.

Sisi kama kamati tumemwambia Katibu Mkuu kwamba amwambie Waziri kabla ya bajeti hii tuone mabadiliko kwenye chumba hichi. Sisi kama kamati tunadhani hatuna haja ya kupitia bajeti bila ya kuona chumba hichi kimerekebishwa. Hatuwezi kusubiri wagonjwa wanafariki pale kwa sababu ndogo ndogo kama hizi halafu tujikaze kwamba tupitishe bajeti ya serikali. Tumeagiza kwamba hili lifanyiwe marekebisho haraka kabla ya bajeti hii ya 2011/2012 ili tuone kama kweli maagizo ya kamati yanafuatwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri alifanyie suala hili ili tuone uwajibikaji wa serikali. Hatuamini kwamba hewa ya *oxygen* ina gharama kiasi hicho ya kuwa haipatikani kwenye chumba kile. Hatuamini kwamba hakuna uwezekano wa kupata wauguzi sita kwa kila kitanda na muuguzi wake. Hatuamini kwamba serikali inashindwa kuwaweka wauguzi angalau watatu kuongeza nguvu katika chumba kile. Kwa hivyo, wito wetu kama kamati jukumu hili lirekebishwe kabla ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, pia tumeona kwamba kwenye kamati juu ya wizara hii hatua ya mwanzo kwenda kuangalia maelekezo ya kamati kwenye chumba hichi cha *ICU*. Je, kamati imetekelezewa wajibu wao na serikali au tumedharauliwa, pale tumedharauliwa na sisi tuna haja ya kuidharau serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo tumeliona ni suala zima la Chuo cha Sayansi ya Afya Mbweni hapa nataka nitoe pongezi. Kuna Mzanzibari ambaye alikuwa anaishi Malaysia lakini kutokana na wito wa Rais wa kuunda Kitengo cha *DIASPORA* ameamua kurudi Zanzibar kuja kufanya kazi hapa Zanzibar. Ni mtaalam ambaye alikuwa ameajiriwa Malaysia lakini ameacha kazi kule na familia yake amerudi Zanzibar kuja kufanya kazi.

Ushauri wangu kwa serikali mtaalam huyu tumuenzi ili uamuzi wake wa kuja Zanzibar usije ukaleta mawazo mengine. Ni mawazo ya busara mtaalam huyu ameona arudi kwao aje afanye kazi Zanzibar kusaidia nchi yake na ndugu zake. Mhe. Mwenyekiti, wito wangu kwa serikali ni kwamba tumsaidie mtaalam huyu ili aweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika Chuo cha Afya Mbweni kuna uvamizi wa maeneo. Tumekuwa tukisema mara nyingi kwamba lazima maeneo ya taasisi za serikali tuapatie hakimiliki. Hadi hii leo Chuo cha Sayansi ya Afya Mbweni hakina hakimiliki watu wanavamia na eneo limebakia dogo sana. Ushauri wetu kama kamati basi serikali ishirikiane na chuo kile waweze kupatiwa hakimiliki ili maeneo yaliyobakia yasiweze kumalizika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Wizara ya Afya nadhani nifikie hapo na nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba maagizo ya kamati hii ni Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wala sio Kamati ya Wanawake. Kwa hivyo, hatuna masihara katika hili, *ICU* irekebishwe iangaliwe haraka sana vyenginevyo huko mbele hatuelewani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nadhani niwape pongezi kwamba licha ya matatizo waliyonayo ya uhaba wa walimu lakini wanaendelea kusimamia vizuri katika majengo ya maskuli yetu Unguja na Pemba. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, nadhani Wizara ya Elimu inastahiki sifa kwamba wanaendelea kusimamia ujenzi wa skuli zile 10 katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Changamoto ambayo inawakabili ni ukosefu wa walimu wa sayansi lakini suala hili Mhe. Waziri na viongozi wenzake yuko mbioni kulifanyia kazi kwa ajili ya kutatua tatizo hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jengine katika hapa ni ombi langu tu kwamba vituo vya *TCU* Zanzibar vinachukua jitihada kubwa sana katika kuwasomesha walimu wetu. Ushauri wangu kwa serikali wawapatie fungu maalum la bajeti ili waweze kutoa huduma nzuri zaidi kwa kusomesha walimu wetu katika vituo vya *TCU* za walimu Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa katika wizara ya mama yangu niseme tu kwamba hapa vile vile hapakuwa na matatizo makubwa ila tatizo lao ni kwamba ofisi yao ni finyu. Nitoe wito kwa serikali wapatiwe jengo la maana ili waweze kujitawanya na kufanya kazi vizuri. Lakini mliobakia mote mwengine kwa kweli wizara hii ambayo waziri wake ni mwanamke wanajitahidi kufanya majukumu yao kama ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia sitaacha kupongeza maamuzi ya Mama Shadya Karume ya kujenga nyumba ile ya Mazizini ambayo ni maamuzi sahihi, halali na yanapaswa kupigiwa mfano. Katika hili nadhani niseme kwamba *First Lady* lazima auige mfano wa Mama Shadya kwa maana ya kuleta maendeleo katika nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii tukaweza kukutana hapa. Mhe. Mwenyekiti, pili nikupongeze wewe binafsi kwa mara ya kwanza kukikalia kiti hicho adhimu. Namuomba Mwenyezi Mungu ajaalie akubakishe katika kiti hicho na akupe kiti cha juu zaidi baada ya hapo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya

kuzikagua wizara hizo na hatimaye wakaweza kutuletea ripoti hii ambayo kwa kweli imegusa katika kila eneo na inaonesha kwamba wamefanya kazi ya ziada katika kufanya wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, pili niseme kwamba ripoti hizi zina umuhimu mkubwa sana kwa sababu moja kati ya kazi za Baraza letu ni kuisimamia serikali. Hilo ni jukumu la kikatiba. Watu tunaoisimamia serikali basi utakuta Baraza la Wawakilishi katika kuisimamia serikali ni kupitia utendaji wa kamati zetu. Kupitia utendaji wa kamati zetu ndio tunapoweza kutekeleza jukumu la Baraza la Wawakilishi katika kuisimamia serikali.

Kwa msingi huo basi, hii ina maana kwamba utendaji wa kamati zetu ni sawa na kuangalia utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka mmoja. Katika kila mwaka huwa tunakutana na kupitisha bajeti za wizara kadhaa, kwa msingi huo upitaji wa kamati katika wizara maana yake ni kamati kwenda kuangalia utekelezaji wa bajeti katika kipindi kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, naliomba Baraza ripoti hizi kwa kweli zipewe muda mwingi katika kujadili kwa sababu katika ripoti hizi ndipo tunakuta utendaji wa serikali, tunakuta usimamizi wa Baraza kwa serikali. Kwa hiyo, haiwezekani kwamba ripoti hizi kuzipa muda mchache sana katika kujadili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kuomba muda zaidi katika kujadili ripoti naomba kwamba ripoti hizi zichukuliwe na zipelekwe kwa watendaji, chochote kinachoonekana hapa kama ni kosa yawezekana kwamba wanaofanya makosa sio mawaziri, watendaji ndio wanaofanya makosa. Kwa hiyo, kama kuna chochote ambacho kinatakiwa kifike katika wizara basi ni muhimu kwa watendaji kukabidhiwa ripoti hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kesi hii ilipita katika mawizara na bahati mbaya sana watendaji hawakuwa na ripoti. Sasa si kitu kizuri kwamba tunachokijadili hapa ingawa ningelitaka kuona watendaji hapa katika wizara zetu tatu wakiwepo kwa sababu ndio wanafikia moja kwa moja maelezo yatokanayo na ripoti hii. Kwa hivyo, mbali ya kuwepo kwao hapa lakini napendekeza ripoti hizi zisiishie kwa wawakilishi bali ripoti hizi zikabidhiwe kwa Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wengine wa wizara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa Wizara ya Afya na hapa nitakuwa na mambo mawili matatu. Kwanza niunge mkono umuhimu wa kuwa na *ICU* katika kisiwa cha Pemba. Maana yake hii iliyopo Mnazi Mmoja hatujaweza kuikamilisha leo tunajadili kuanzisha *ICU* Pemba kidogo ni kitu ambacho hakijakaa vizuri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuacha kulijadili hilo kwa umuhimu wake. Ni muhimu iliyopo Mnazi Mmoja ikamilishwe kama Hospitali ya Rufaa, lakini kwa mazingira ya visiwa vyetu Unguja na Pemba kuna umuhimu mkubwa sana na kisiwa cha Pemba kuwa na *ICU*. Pemba huwa kuna wagonjwa wengi katika hali ya mahututi, haiwezekani mgonjwa mahututi ukamchukua ukampandisha kwenye Serengeti kumleta Unguja nafikiri atakufia mikononi.

Haiwezekani mtu mnyonge ana mgonjwa mahututi ukamwambia akodi ndege kwa sababu serikali haina ndege ya kusafirisha wagonjwa. Kwa hivyo, kuna kila haja na kuna kila umuhimu wa kisiwa cha Pemba kuwa na huduma hii ya *ICU*.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ingawa niliuliza swali katika Baraza la Wawakilishi na swali langu bado halijajibiwa lakini kwa umuhimu wake naomba niliweke hapa. Serikali imeanzisha utaratibu wa kuchangia gharama kwa wananchi tunakwenda nalo, lakini tatizo hili kwa kweli suala la watu kuchangia gharama hasa za matibabu limekuwa ni tatizo kubwa sana. Hatufiki pahala kwa kweli tukajua hasa ni maeneo gani ambayo serikali inaruhusu kuchangia gharama na ni maeneo gani ambayo serikali inapinga kuchangiwa kwa gharama. Sasa hivi inakuwa ni vurugu mechi katika hospitali zetu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Waziri wa Afya afanye kazi kubwa sana ya kulitazama hili. Hospitali yetu ya Chake Chake kwa kweli nasema hivyo kwa sababu ndio mara nyingi ninapokuwepo kuna tatizo kubwa la wagonjwa kuchangishwa kila aina ya huduma. Mzazi akenda anataka kujifungua apeleke mipira, *gloves* na kila kitu, lakini hata kitanda anachokitumia hutakiwa akichangie. Hili ni jambo la kusikitisha sana, wenzangu wananambia si Chake Chake tu, lakini mimi nasema Chake Chake kwa sababu ndio mara nyingi ninakuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kilio kikubwa cha wananchi juu ya suala zima la kuchangishwa gharama, kila kitu unachokifanya hospitali ni gharama. Kwa hiyo, namuomba sana Waziri wa Afya asimamie suala hili. Anapokwenda yeye kama Mhe. Juma Duni Haji kwa kweli watu siku hiyo wanaweza wakawa *standby* lakini mara tu akiondoka msimamo pale pale. Sasa suala hili laitani tukipewa sisi wawakilishi tulifanyie kazi au wakimwaga askari wa usalama na askari mbali mbali nadhani itakuwa ndio dawa. Kuna haja kubwa sana, kuna kilio kikubwa sana ambacho kinatakiwa kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo napenda nilisemee ni tatizo la usafi. Mhe. Mwenyekiti, tunatazamia kwamba hospitali pawe ni pahala makimbilio ya usafi. Ni kitu cha kusikitisha sana kwamba hospitali zetu kwa kweli ni chafu sana, utakuta wodi moja choo kinachotumika ni kimoja. Katika hali kama ya

hospitali utawezaje kuweka choo kimoja, huyu ana tumbo la kuharisha, huyu ana kipindupindu choo ni hicho hicho kimoja na ni kichafu.

Mhe. Mwenyekiti, leo katika gazeti la Zanzibar Leo Hospitali ya Chake Chake inakosa maji. Sasa huwezi kuwa na hospitali ambayo haina maji, suala la maji na suala la usafi ni vitu muhimu sana vinavyohitajika katika hospitali zetu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Waziri wa Afya, msaidizi wake wasimamie kwa nguvu kubwa sana katika suala la kuona usafi unaimarishwa katika mahospitali yetu. Mgonjwa hukimbilia hospitali kwa ajili ya kwenda kupata matibabu, inawezekana kwamba mle mle hospitali akapata maradhi mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala la elimu tunaipongeza serikali kwa kuanzisha Kamati za Skuli. Mhe. Mwenyekiti, kamati hizi za skuli pamoja na kazi nzuri wanayofanya ya kuimarisha maskuli yetu lakini mamlaka yao wakati mwengine yanakuwa ni makubwa.

Hebu tupate muongozo wa waziri, hizi kamati za skuli zina mamlaka gani, maana yake leo ikiwa mwanafunzi hakwenda na mchango kamati za skuli ndio zinazotoa adhabu kwamba mwanafunzi huyu mfukuze. Wakati mwengine huwa zinakwenda kinyume kabisa kabisa na msimamo wa serikali. Unaweza ukasema kwamba serikali haijaruhusu wanafunzi waliokuwa hawachangii wafukuzwe lakini kamati wao hujipiga kifua wakakwambia sisi kama kamati tunawafukuza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aliangalie hili na ikiwezekana atupe uhalisia wa suala hili ukoje. Mamlaka iliyonazo hizi kamati za skuli kwa kutekeleza mambo mbali mbali yanayohusiana na masuala ya maendeleo ya wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nigusie Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana wizara kwa kazi wanayofanya hususan kupitia vikundi vya ushirika. Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari sasa hivi wameshajihishwa sana katika kujikusanya kwa nia ya kujiletea maendeleo. Hivi sasa popote utakapokwenda utakuta vikundi vya ushirika, hii maana yake ni kwamba watu sasa wako tayari katika kujiletea maendeleo yao, tatizo lao kubwa ni namna ya kupata uwezo wa kujiletea hayo maendeleo yanayokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ikishirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ziunge nguvu za pamoja ili ziwasaidie mbinu na uwezo vikundi hivi ambavyo viko tayari kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao. Si kitu cha kufurahisha hata kidogo kwamba watu wameshajikusanya

lakini wakakosa tu wakati serikali yao ipo. Kwa hivyo, tunaiomba serikali ifanye kadri kila juhudi inayowezekana kuvisaidia vikundi hivi kwa kuvipa nyenzo, utaalam na kila namna ambayo inaweza ikavisaidia kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho naomba kwa kamati yenyewe ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kamati hii kwa kweli nimeshawahi kuifanyia kazi, naifahamu mazingira yake ya kazi. Takriban ni tofauti na Kamati ya PAC. Kamati ya PAC mara nyingi inaonana na malodi, inaonana na makatibu wakuu na wahasibu. Lakini kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inakutana na watu wenye matatizo. Wazee, wenye ukimwi, wenye ulemavu, watu ambao wameshajikusanya wanataka kusaidiwa, wazazi na inakutana na kila aina ya makundi kamati hii.

Sio vyema na haipendezi Mhe. Mwenyekiti, kwa kamati yako kwenda pahala ambapo pana watu wenye matatizo na kuanza kuvutana vichochoroni pembeni kwa ajili ya kupigishana donesheni. Watu wanapoona kamati hii basi hupata faraja kwamba leo viongozi wetu wanakuja kwa ajili ya kuja kutuona. Kwa vyovyote vile katika akili zao huwa wanategemea kitu fulani na katika hatua nyengine kweli unalazimika lazima utowe chochote. Sasa wakati mwengine unayo wakati mwengine huna inabidi kamati ya Baraza iseme uongo, tutakuja kesho kumbe ndio gia ya kutokea hiyo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naliomba Baraza la Wawakilishi wajaribu kutenga fungu maalum kwa kamati hii, pale inapokwenda kuwatembelea watu wenye matatizo mbali mbali, kwa heshima ya Baraza la Wawakilishi, inakuwa ni vizuri na kamati kutoa chochote. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba fupi kwenye kamati hii kama ifutavyo. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na michango mikubwa niseme tu kuwa taarifa hii imeandikika vizuri na tumeifahamu na natoa pongezi kwa kazi kubwa kamati iliyofanya na kuyaona waliyoyaona pamoja na mapendekezo yao.

Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, nyongeza haigombi. Kwanza naomba nizungumzie katika suala zima la elimu. Mhe. Mwenyekiti, elimu ndio ufunguo wa maisha na hakuna taifa lolote linalokwenda ikiwa watu wake hawana elimu ya kutosha. Wakati unabadilika na sisi lazima tubadilike.

Mhe. Mwenyekiti, kwa makusudi kabisa serikali yetu iliamua kukuza kiwango cha elimu ya sekondari kwa kueneza madarasa ya sekondari takriban kila shehia. Kinyume na ilivyokuwa hapo zamani wakati Pemba nzima katika

wakati wetu kulikuwa kuna shule moja tu ya sekondari. Sasa hivi zimeenea ni hatua nzuri na leo ilikuwa ni kuwakuza watoto wetu kielimu

Mhe. Mwenyekiti, unapounda kitu basi kuna mambo yake ni lazima yatangulie. Unapoweka shule ya sekondari inahitaji kuwepo walimu wa kutosha, tena wenye sifa za kutosha za kusomesha hiyo sekondari. Kwa masomo ya sayansi unahitaji kuwe na vifaa vya sayansi ambavyo wanafunzi watatumia katika masomo yao pamoja na walimu ili kuweza kukijua wanachokifanya na kuweza kukabili mitihani ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira katika zile sehemu ambazo shule hizi ziko basi bahati mbaya kimazingira ni lazima kuwe na nyumba ya mwalimu. Kwa hivyo, ilikuwa ni lazima hizo nyumba ziwepo ili kila mahala elimu itolewe katika hali inayofaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali ilivyo hivi sasa tuna shule za sekondari zimeenea, kwa hivyo ni neema kwetu na kila inapotolewa matangazo muda wa siku mbili wanatangazwa watoto wanaopasi tu, hivyo ile ni neema kubwa. Linalosikitisha Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba wanapofanya mtihani wa kidato cha nne matokeo yanakuwa mabaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika matokeo ya juzi yaani yale ya hivi karibuni kwa wale waliomaliza kidato cha nne, nilifanya utafiti angalau kwa shule zangu tatu katika jimbo langu zilizokuwa zina shule za sekondari, basi niliona mambo ambayo mimi mwenyewe naona aibu hata kuyataja.

Kwanza katika kutafuta basi niliangalia kwenye masomo yote, ukichukua matokeo ya jumla kwa kila somo katika kila skuli kwenye skuli zangu tatu za Mkongeni, Kiki na Uwondwe, GPA yao ni 4.7 na kuendelea mbele. Nikisema GPA maana yake ni kuwa kama watoto wastani wa darasani wamepata A basi huwa ni 1, B ni 2, C ni 3, D ni 4 na F ndio 5. kwa hivyo *average* ni 4.7 na kuendelea ni kama kuwa katika masomo hayo waliyofanya mitihani yao kwa skuli hizi tatu wote wamefeli. Katika hizo skuli tatu ni mwanafunzi mmoja tu ndio kapata *division* 3, wengine wote waliobakia ambao ni wachache wamepata *division* 4.

Mhe. Mwenyekiti, Jimbo la Mtambwe ni moja katika majimbo 18 yalioko Pemba na 50 yalioko Unguja. Naamini sio Mtambwe tu, huo ndio wastani wa mambo ulivyo isipokuwa skuli chache sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwenye ripoti kuwa kuna ukaguzi mkubwa tu, walimu wakuu wanafanya ukaguzi na kupeleka taarifa wizarani, wizara inafanya ukaguzi mkuu katika skuli chache. Lakini sisi siku zote tunaangalia

matokeo, ikiwa matokeo mabaya tunasema kila kitu ni kibaya, hapa sio kwa masomo ya sayansi tu pia kwa masomo ya *Art*.

Kwa hivyo, ushauri wangu kwa serikali ni kwamba kwa sababu bila ya elimu hatuwezi kufanya lolote. Hivyo ni vizuri tuendelee na mpango huu mzuri wa kuelimisha watoto wetu kwa wingi, lakini tuone kuwa watoto wanapata elimu inayostahiki na walimu wanamudu kusomesha hayo masomo. Sio kutangaza majina kisha watoto wakawa wanafeli ovyo, wakishafeli hawana nguvu au uwezo wa kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, ili patokee mafanikio, basi kuna mambo ambayo yanahitajika. Kwanza ni ukaguzi uliothabiti na wa kweli. Kwa vile mwalimu mkuu anataka adumu pale alipo basi atawakagua walimu wenzake na kupeleka ripoti ambayo yeye mwenyewe itakuwa hairidhishi kwa wale walimu wake. Kwa hivyo, mimi binafsi ukaguzi wa walimu wakuu naupinga moja kwa moja, kwa sababu hauelezi hali halisi ilivyo na ingelikuwa ndivyo basi tungeona matokeo. Tungesikia leo skuli fulani mwalimu mkuu kaleta ripoti kuwa walimu wake ni wabaya sana. Lakini kila siku tunasikia kimya na matokeo ni mazuri, lakini mwisho wa siku watoto wetu wanaangukia kufeli.

Mhe. Mwenyekiti, skuli inahitaji mashirikiano makubwa sana baina ya walimu, wanafunzi na wazee kwa kupitia kamati yao ya skuli. Mimi nililogundua katika utafiti wangu ni kinyume na wizara kwa makusudi ilipoweka kamati ya skuli kwa maslahi ya skuli. Badala yake katibu wa kamati ya skuli ambaye ni mwali mkuu huwa anatoa miongozo na taarifa tu kwa kamati, kamati hawafanyi kazi zao vilivyo. Kwa hivyo, kuweka watu kupokea taarifa ni kinyume na kuweka watu kuwa ndio wenye uwezo wa kujua ile hali halisi ilivyo. Nashukuru kamati ilivyoeleza kuwa ipo haja kwa huyu Mwenyekiti, atafutwe mtu mwenye uwezo anayeweza kuiendesha hii kamati.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana kwa kuongeza ujenzi wa skuli hizo 15, lakini tujuwe kuwa tulikuwa na mpango huko nyuma kwamba wazee wasaidie kujenga majengo ya skuli. Sasa hivi kuna majengo mengi sana Unguja na Pemba ambayo bado hayajaezekwa, kuna majengo mengi ambayo yanatakiwa kufanyiwa matengenezo na kuna shule mpya ambazo zinajengwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nieleweshwe kwamba kwa haya majengo ambayo sijayaona maelezo yake ya kuridhisha humu, isipokuwa kamati inahimiza tu yamalizwe kuezekwa. Haya majengo ambayo sheria ya kuwa yajengwe mpaka kufikia kiwango cha kuezekwa imekamilika na yanahitaji kuezekwa ili watoto wapate kusoma. Je, kwa vile ni mengi sana wizara imefanya mpango gani wa makusudi ili kuona haya majengo yameezekwa na

yanatumika kwa kuwasomeshea wanafunzi ili kuondoa ule msongamano wa wanafunzi ambao pia unapunguza wakati wa masomo.

Mhe. Mwenyekiti, sitowacha kulalamika kwa sababu ni wajibu wangu, niende kwenye Wizara ya Afya ambayo ni muhimu ambayo sote tunahitajia na tunashukuru Wizara ya Afya kwa kufuata dira ya serikali, imejitahidi kuongeza vituo vya afya. Wizara imesema kila penye masafa ya kilomita 5 basi Kituo cha Afya kipo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna vituo vyengine kwa bahati mbaya havina madaktari, kwa maana ya daktari ni yule mtu ambaye anatibu na ni mkubwa katika kile kituo, sio kwa *qualification*.

Kwanza kabla sijaendelea nashukuru safari hii Waheshimiwa Mawaziri mbali mbali walikuwa wakifuatilia malalamiko yetu. Mhe. Mwenyekiti, katika kituo changu cha Uwondwe ambacho ni kikubwa sana chenye watu wasiopungua vijiji 12, wanaotumia kituo kile, lakini hakina daktari, daktari aliyeko ni mmoja tu ambaye anafanyakazi Makongeni na Uwondwe, ambapo kuna umbali ambao haupungui kilomita 10. kwa bahati mbaya kwa siku za mvua haiwezekani kwenda Makoongeni na ukaja ukafanyakazi Uwondwe. Hata ikitokea kesi kubwa ya namna gani kwa siku za mvua huwezi ukamchukua mgonjwa ukampeleka Wete. Kwa hivyo, kuna kila ulazima wa kituo cha Makoongeni na kituo cha Uwondwe kila mmoja kuwa na daktari wake. Kwa bahati nzuri tunao vijana wetu waliomaliza elimu ya afya diploma na hawajaajiriwa na bado shida tunaipata ya daktari.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa hili, ifanye haja ya dharura ili tupate daktari pale katika kituo cha afya Uwondwe atakayesaidia matibabu, kwa sababu tunahangaika sana. Mhe. Naibu Waziri kwa sababu kaenda, basi nafikiri atanipa ushauri mzuri kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda umepita sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika moja. Suala la mwisho lililobakia ni kwamba kwa bahati mbaya wazazi wengine hutokewa na uzazi wa ghafla, na wazazi wale huwa wanahitaji uangalifu maalum katika kupelekwa kwenye vituo kwa matibabu pale inapotokezea matatizo. Mhe. Mwenyekiti, tuna tabu sana kupata haya magari ya kubebea wagonjwa, kwa hivyo hulazimika kutumia gari zetu kuchukulia wagonjwa kama hao ambao kiafya hasa haturuhusiki.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara ifanye mpango na kututupia macho, muje hospitali za mashamba angalau mutafute njia ya kuweza kupatikana gari inapotokezea hii dharura. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii fupi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii iliyosomwa hivi punde.

Pia nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, kwa siku ya leo ya kwanza kukalia katika kiti hicho na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akujaalie kazi yako iwe na baraka na ufunguzi mwema.

Mhe. Mwenyekiti, nakukumbusha jambo moja tu kwamba unapomtaja mjumbe wa kwanza basi na wa pili mtayarishe ili ajuwe vipi ajitayarishe *Inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia hotuba hii kwanza kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, elimu ni ufunguo wa maisha, huu ni usemi ambao wameusema wazee na una maana pana sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mhe. Mwenyekiti wa kamati alizungumza kwamba kuna upungufu mkubwa wa walimu kisiwani Pemba. Mimi naamini sio kisiwani Pemba tu hata kisiwani Unguja kuna upungufu huo wa walimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi kwamba kuna walimu mbali mbali ambao wamesomea ambao mpaka leo hawajaajiriwa, nahisi kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ingejipanga vyema kuwaajiri walimu hao ili kupunguza upungufu huu wa walimu.

Halikadhalika, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alizungumzia kuhusiana na upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi. Kwa kweli visiwa vyetu vya Unguja na Pemba tatizo hili lipo kwa muda mrefu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiwa mwakilishi nashangazwa na kitu kimoja tu katika wizara hii, nafikiri waziri hapa yupo. Tumeanzisha skuli za michipuo kwa muda mrefu sana ambazo zinatoa wanafunzi wenye vipaji vikubwa vya akili, kuna skuli mbali mbali ambazo wanakwenda wanafunzi hawa na wanafunzi hawa wanatoka maskulini kwao wakiwa ni wa mwanzo katika skuli zao. Sasa wanafunzi hawa tunawaandaa vipi, hata ikawa Zanzibar mpaka leo ikawa na upungufu wa walimu wa sayansi kila siku upungufu wa walimu wa sayansi.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa makini sana na aweke mikakaati maalum ya wanafunzi hao wa michipuo ili rasilimali hii ya ubingwa na uhodari walionao uendelee ili taifa letu la Zanzibar lipate wataalamu wa hali ya juu kwa kupitia hawa wanafunzi wa sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo mimi nitalizungumzia kuhusu habari ya elimu, kwa kweli ni masikitiko makubwa ya mishahara duni ya walimu wa

Serikali ya Zanzibar. Kwa kweli walimu wana kazi ngumu, kila mmoja anaelewa kwamba mwalimu kazi yake sio kusomesha tu. Mwalimu ana kazi ya ujaji, anakazi ya ukarani na ana kazi ya kila kazi unayoijua wewe hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikasema walimu wana kazi ya ujaji, ni kwamba wanafunzi wote wenye matatizo yao kwao kwa wao wanakwenda kwa walimu. Mwalimu mwanafunzi fulani kanifanya hivi na hivi, kisha mwalimu ana hukumu, mwalimu yule kanifanya hivi na hivi mwalimu anaamua. Kwa hivyo, walimu hatukuwapa nafasi ya kusomesha tu, bali wana kazi ya kuwalea wanafunzi katika mazingira tofauti tofauti. Kwa maana hiyo walimu wanapaswa kuangaliwa maslahi yao, pamoja na kuangaliwa maslahi ya wafanyakazi wote wa Zanzibar, lakini walimu wapewe nafasi ya kwanza kutokana na umuhimu na unyeti wa kazi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja hapa kuhusiana na kazi ngumu ya walimu. Mara moja katika skuli yangu pale, ilipita gari na wanafunzi ulikuwa umeshafika wakati wa mwisho wa kuondoka skuli na kwa sababu ile gari ilisimama, basi walikwenda kuvamia wanafunzi ili wapate msaada wa kufikia kwao, lakini dereva wa gari alikuwa hataki kuwasaidia wale wanafunzi ili kuokoa hata usalama wao, kwa sababu ilikuwa ni gari ya wazi na wale watoto walikuwa ni wadogo wadogo. Basi alitoka dereva pamoja na mfanyakazi mmoja katika gari ile kwenda kuwazuia wanafunzi wale, lakini walishindwa kuzuilika ikawa wanaivamia gari. Katoka mwalimu mmoja tu mwanamke tena mdogo, akenda kusimama na kuwaambia hebu nyinyi njooni huku, basi wale wanafunzi waliteremka kwenye ile gari tena kwa upole kabisa.

Kwa hivyo, walimu wana kazi ngumu, wana kazi ya kitaalamu na wana kazi ya ufundi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naiomba wizara yako ijipange sawa sawa pamoja na kushirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ili iwaangalie walimu katika maslahi yao na maposho yao.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hili, hivi sasa inasikitisha kwamba kuna walimu wamesahihisha mitihani katika kipindi kilichopita hicho basi mpaka leo hawajalipwa posho lao la mitihani, inasikitisha sana. Kwa hivyo, walimu wanapaswa wazingatiwe sana kwa sababu ya kazi ngumu ambayo wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nategemea kwamba baada ya kikao hiki, basi walimu hawa watajisikia vizuri sana na kwa sababu ya Serikali yao ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, basi wanategemea wananchi wote na wafanyakazi wote wafaidike ndani ya maslahi yao katika uongozi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha hapo basi niende kidogo tu kuhusu habari ya huduma ya likizo za walimu. Huduma hii haina mpango, walimu wanapewa

huduma bila kuzingatia. Kwa sababu kuna walimu wanatimiza miaka 20, lakini hata mara moja hawajapewa huduma hii ya likizo. Kuna walimu kila baada ya miaka miwili au miaka mitatu basi wanapewa huduma ya likizo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri suala hili ulipange vizuri ili kila baada ya kipindi fulani mwalimu awe anajisikia kupata hii huduma ya likizo, kwa sababu hili nalo ni motisha kwao. Mhe. Mwenyekiti, huduma hii ya likizo ya Shs.30,000/= kwa kweli hii imepitwa na wakati kwa mujibu wa wakati tulionao sasa.

Halafu jengine ambalo napenda kulichangia mimi kuhusu hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, kuna ukosefu mkubwa wa vitabu vya skuli za msingi hasa darasa la kwanza mpaka la tatu. Darasa la kwanza mpaka la tatu wamepelekewa *syllabus* walimu ya kufundishia, lakini hawajapelekewa kitabu hata kimoja. Kwa maana hiyo wizara inapaswa kujipanga na kuwapelekea walimu vitabu ili na wao wajitanafasi katika kazi yao ya ufundishaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita nilitembelea skuli mbali mbali, kwa masikitiko sana nilipita TAC pale Mzingani nakazungumza na walimu wa elimu masafa pale, kuna kitu kimoja walinielezea walimu wa skuli ya Kiwani msingi, kitu hicho ni cha masikitiko sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba unisikilize vizuri kuhusu kitu hicho, kisha ukifanyie kazi vizuri.

Walimu hao wanasema kwamba jamani wizara itutambue tukiwa wazima, tukiwa wagonjwa na tukifa. Nikawauliza kulikoni. Wakaniambia kuna mwalimu wetu anaitwa Ali Khamis, mwalimu huyu kafariki, lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, haikuleta hata mjumbe mmoja kuja hata kuihani ile familia iliyopata msiba. Kwa hivyo, hiki ni kipigo kikubwa sana ambacho tumepata mshangao je, wizara ina nini inatutaka tukiwa wazima tu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa kweli linavunja moyo kwa kiasi fulani, kwamba walimu wanapokuwa wazima wanatumika, lakini wanapofikwa na msiba kama huu hawajaliwi, kwa kweli wanahuzunika. Mimi labda niwaambie walimu wa skuli wa Kiwani msingi na walimu wote kwa jumla wastahamili na niseme hilo lilikuwa ni bahati mbaya kama lilitokea haikuwa ni makosa ya wizara, lakini tunalizungumza hivi ili wajuwe kwamba ujumbe wao umefika.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo niende kwenye Wizara ya Afya kidogo tu. Mhe. Mwenyekiti, mimi katika wizara hii kwa sababu wenzangu wamechangia sana, basi sitaki hata niichangie sana. Isipokuwa naona kuwa ni kitendo cha aibu sana kwamba hospitali zetu zinatajwa na Mhe. Mwenyekiti wa kamati kwamba ni chafu. Jamani sehemu ya afya ni pahala muhimu sana, kwa sababu hospitali hata kama iko safi basi ile harufu yake ukenda basi inachosha, seuze

panakuwa pachafu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Afya, nafikiri suala la usafi ni kuwapanga vyema wafanyakazi tu, kwa sababu wafanyakazi wanaofanya kazi za usafi wapo na hili halihitaji gharama kubwa, ni kuwapanga vyema tu ili mazingira yetu haya yakawa ni mazuri na yakawa yanapendeza kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba ni juzi tu tulikuwa tukipitisha mswada wa haki za watoto. Mhe. Omar Ali Shehe alizungumza hapa kwamba Hospitali ya Chake Chake na kuna baadhi ya wajumbe wakasema hapana sio Chake Chake tu, kuwa hizi huduma za kulipia afya zimekuwa ni nyingi mno. Kwa hivyo, mimi ningekuomba Mhe. Waziri, kwa kuwa tumepitisha mswada juzi tu wa kutunza watoto, basi mama wajawazito na watoto wadogo wasitozwe huduma yoyote ya afya, kwa sababu ndio miongoni mwa kuwatunza. Lakini leo tunakwenda kumtoza huduma ya afya mama mjamzito, ambaye keshokutwa anazaa, au tunamtoza huduma mtoto wa miaka miwili au mwaka mmoja na nusu, sasa itakuwa tunamtunza vipi. Kwa hivyo, suala hili naomba tuliangalie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niungane na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya PAC, Mhe. Omar Ali Shehe, kuhusiana na hii Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuwa inapita kwenye makundi tofauti. Kwa maana hiyo inapaswa kabisa kutengewa fedha maalum, kwa ajili ya kutembea katika mazingira yale ambayo wanapita, kwa sababu mazingira wanayopita ni magumu na ni aibu kwa Waheshimiwa Wawakilishi kwenda kuzungumza na watu wenye ulemavu, wakaombwa msaada na wakashindwa kutoa msaada. Inastahiki sana Baraza la Wawakilishi wapangiwe bajeti maalum, kwa ajili ya kamati hii kwa kutembea katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache, nashukuru na mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani, ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kunifikisha hapa na kuweza kuzungumza katika Baraza hili na kuweza kuchangia hotuba hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Kwanza napenda kusema kwamba nataka nichangie zaidi kuhusu wazee wetu ambao tunaweka katika hali ya kuwachangia fedha.

Mhe. Mwenyekiti sisi tunachangia fedha, yaani serikali inawachangia wazee fedha, lakini utakuta wazee wanachiwa fedha kiasi cha shilingi 5,000/- tu

katika mikoa au vijijini. Kwa kweli ni tofauti unavyoona wazee wa hapa mjini utasikia wamechangiwa shilingi 25,000/- kwa mwezi.

Lakini ukweli ni kwamba wazee wetu wa vijijini hivi sasa wamepewa shilingi 5,000/- kwa mwezi, fedha hizi zinaweza kufika hata miezi mitatu mzee yule bado hajapata huduma hiyo. Kwa hivyo, kuna haja ya kuwajali sana wazee katika mikoa au vijijini na wao waweze kupata huduma kulingana na wenzao wa hapa mijini kama tulivyosikia hapo mwanzo kwamba wanaweza kupata shilingi 25,000/- kwa mwezi na wala hiyo haitoshi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema kuchangia hasa angalau kuweza kufikia mshahara wa watu wa chini shilingi 100,000/- kwa mwezi. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu suala la kuwachangia wazee katika makaazi. Kwa mfano, mjini kuna maakazi ya Amani pamoja na Welezo yote yako mjini, lakini wazee wetu wa vijijini sijasikia hata mkoa mmoja kuwa ipo sehemu ya kukaa wazee angalau kukusanywa kwa pamoja na kuweza kupatiwa huduma nzuri.

Kwa kweli mikoa yote ya Unguja na Pemba wazee wako mbali mbali na wala hawana huduma ya kawaida kuchangiwa na kujulikana kama pale wapo wazee na kuna haja ya kwenda kwa ajili ya kutoa huduma, kwa ajili ya kuwajali wazee. Kwa mfano, hivi sasa wazee wa mashamba au katika mikoa wameshazoea kumsumburi Mwakilishi au Mbunge ndio aweze kutoa huduma zao, serikali imejiondoa kabisa badala ya ile shilingi 5,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, tukifikiria shilingi 5,000/- kwa mwezi tunaweza kusema kwamba shilingi 5,000/- kwa siku haitoshi je, fedha hizi kwa mwezi na hawa wazee wetu tumewaweka katika hali gani ambao wako vijijini. Kwa hivyo, ni vizuri serikali ikaanza upya kupanga maendeleo ya wazee wa vijijini na wao wakalingana na wenzao wa mjini.

Kwa maana hiyo, utawakuta wazee wa vijijini wako njiani kila siku, kwa ajili ya kuja mjini na wanakuwa omba omba na halafu jioni anarudi tena kijijini kwa makaazi. Vile vile hivi sasa tunaambiwa kuna wazee 65 tu katika Nyumba zetu za Wazee za Amani, yaani hao wazee wa Amani 65 sio kama wazee wote kama wazee wengine, kwa sababu ukifuatilia sana wazee hao ni waheshimiwa au watu wenye vipato ndio wanaokwenda kuwekwa pale.

Kwa hivyo, kuna haja serikali ama kamati kufika vijijini, kwa ajili ya kujionea hali halisi ya wazee na kwamba kuna haja ya kuwahudumia ipasavyo.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu Wizara ya Elimu. Kwa kweli hivi sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

tunayo mabanda mengi ya kusomea wanafunzi. Lakini katika skuli zetu nyingi hazina vikalio vya wanafunzi na wanafunzi wengi wa vijijini au mikoa wanakwenda skuli wakiwa na sare zao mbovu kutokana na kukosa vikalio, yaani wanakaa chini.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ijitahidi sana kuweza kupata vikalio kwa kila skuli angalau wapate yale madeski ya kuchonga na wala sio viti kwa ajili ya kukaa. Vile vile wanafunzi hao wanasoma lakini walimu wao ni kidogo.

Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ijitahidi sana kuangalia skuli zote hasa wa mikoani au vijijini ziwe na walimu wakutosha. Kutokana na hali hiyo, pia naiomba wizara ya Elimu iajiri walimu kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi kwa lengo la kupatikana ufanisi katika kuwafundisha watoto wetu pamoja na kumaliza tatizo hilo la walimu kwenye skuli zetu.

Vile vile napenda kuchangia kuhusu Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto katika Sheria yao ngumu ambayo wanaomba ipitishwe, ili ipatiwe adhabu nzuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zingatia muda.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwa mfano, hivi sasa wapo wabakaji, lakini wabakaji hao husiki kesi zao kama wamefungwa muda gani na wala amefungwa wapi. Kwa kweli utasikia mbakaji na baada ya siku mbili, tatu husikii tena habari ya mbakaji. Kwa hivyo, ni vyema sheria hii ipangiwe hasa kwamba sheria iseme wazi, kwamba adhabu ya mbakaji ni kifungo cha maisha na isiwe adhabu hii haikupangiwa muda na hapo ndipo tutapoweza kuondoa suala la ubakaji hapa nchini.

Pamoja na hayo, kwa upande wa akinamama wanaofanya matendo mabaya kwa wanawake wenzao hasa watoto, wao waekewe adhabu hiyo ya kifungo cha maisha pale anapogundulika na tabia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii adhim leo ya kupata muda wa kuchangia Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

Vile vile sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya, pia kwa kutuwezesha kuwa na hali ya utulivu na amani katika nchi yetu na kuweza kuyajadili mambo yetu katika hali ya usalama.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila endapo kwamba ripoti ya kamati hii nisipoichangia hata kidogo. Kwa kuanzia mchango wangu niende moja kwa moja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na ndio ilikuwa wizara yangu.

Kwa kweli suala la kuiboresha elimu ni jambo lenye kuhitaji nguvu kubwa sana. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, kila tunaposimama hapa na wakati tunapokuwepo mitaani tunazungumzia kuhusu suala la maslahi ya walimu.

Kwa hivyo, hivi sasa tunamuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti angalie kwa jicho la huruma zaidi masuala ya maslahi kwa walimu wetu, kwa sababu tatizo kubwa kila mjumbe ambaye anasimama hapa anazungumzia maslahi ya walimu. Kwa maana hiyo, kwa wakati huu tunamuomba suala hili aliangalie vizuri, ili tatizo hili liondoke kabisa.

Kwa mfano, mishahara hii midogo haitowawezesha walimu wetu kufanyakazi kwa bidii na kuhakikisha kuwa elimu bora inapatikana.

Sambamba na hilo kuhusu posho la likizo. Mhe. Mwenyekiti, ni kiwa mwalimu nimeshuhudia mwaka mzima mwalimu hajapewa posho yake. Kwa mfano, mwalimu anakwenda likizo mwaka huu kipindi cha Ramadhan, lakini mapaka likizo ya mwaka mwengine ndipo anapokuja kupata futari kwa zile shilingi 30,000/- ambazo analipwa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri tunakuomba sana kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa awamu hii uangalie sana suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika elimu ninashauri serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali aingalie ujenzi wa uzio katika skuli zetu hasa zile skuli ambazo ziko mashamba, kwa sababu za mjini nyingi tunashukuru kwamba wizara imejitahidi kuzijengea uzio.

Kwa kweli migogoro mikubwa hivi sasa inajitokeza katika suala la ardhi skuli, kwamba baada ya kujengwa hata kama palikuwa panakichaka, basi baadaye wananchi wanaanza taratibu kufuata maeneo ya skuli na kuyachukua, jambo ambalo linapelekea migogoro baina ya skuli pamoja na wananchi wetu.

Kwa hivyo, ninashauri sana kama vile Chuo chetu cha Amali cha Mkokotoni kizuri kimemaliza juzi tu na tayari kimeshaanza kazi, lakini bado hakijajengewa uzio. Vile vile kuna tatizo katika Skuli ya Mkwajuni kila siku

kuna migogoro ya ardhi baina ya wananchi pamoja na skuli zetu, pia Skuli ya Gamba na Chaani.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la uhaba wa walimu. Waheshimiwa Wajumbe wengi wanaosimama wanasema kwamba walimu wa *Science* ni kidogo, lakini hata hao wa *Art* wanahitajika. Kwa hivyo, kama wapo kuna skuli yenye walimu wengi, basi nilitewe katika Jimbo langu la Chaani kwa skuli zangu nne za *Secondary*.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Baraza lako tukufu hili tunaiomba serikali kupitia Wizara yake ya Elimu na Mafunzo ya Amali iajiri walimu ambao wamesoma kwa muda mrefu sasa na hawajaajiriwa. Kwa kweli sisi tunawahitaji hata kama watakuwa wa *Art*, basi niletewe mimi tu au waajiriwe kwa upande wangu mimi, nitawachukua watu hao na nitawatumia katika skuli zangu kwenye Jimbo la Chaani.

Kwa kweli tunashukuru sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali awamu iliyopita kwa ujenzi wa skuli nyingi sana. Kwa mfano, katika jimbo langu takriban shehia zote zina skuli. Sasa kwa awamu hii tunamuomba sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, majengo tunayo lakini tunahitaji walimu bora tena wakutosha.

Nikiendelea na mchango wangu kwa haraka nizungumzie Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza sina budi nimpongeze mama yangu Mhe. Waziri kwa mswada wake mzuri ambao umepitishwa juzi tu katika Baraza hili tukufu. Kwa kweli mswada ule tumeuchangia vizuri pamoja na kumshauri na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukubalia mawazo yetu na hatimaye mswada ule umepita kwa salama. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijazungumza mengi katika hili naiomba sana Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti iangalie kwa jicho la pekee wizara hii, kwa sababu ni wizara kubwa, yenye mambo mengi tena ni muhimu sana. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika bajeti ya mwaka huu utatusaidia sana katika wizara hii ambayo ina idara nyingi pamoja na mambo muhimu sana.

Vile vile katika hili nasisitiza sana katika mswada tulioupitisha juzi ni mzuri, lakini naiomba serikali kupitia Wizara hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuangalia upya, yaani kuhakiki watoto wenye matatizo ya ulemavu suala la unyanyapaa bado lipo, watoto hawa wanafungiwa majumbani na wanakosa haki za msingi kama binadamu au watoto wengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kupitia ripoti hii ambayo ipo mbele yetu, basi naiomba izingatie suala la watoto wenye ulemavu na tuwajue hasa yaani tupate *data* rasmi, ili tuweze kuwasaidia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Wizara ya Afya. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi waliopita wamelichangia sana na wala sina haja ya kurejea, isipokuwa nataka nizungumzie suala la uhaba wa madaktari na wala sitozungumzia kwenye Hospitali ya Mnazimmoja na nitaelezea kwa Kaskazini Unguja.

Nadhani madaktari wapo, lakini hawatoshi. Kwa mfano, juzi mimi mwenyewe binafasi nilikwenda Hospitali ya Kivunge na mgonjwa, basi nilipofika pale daktari wa zamu hayupo alikuwa amepata dharura ya kwenda mjini na nilipouliza wale wengine walisema hapa sisi tunakuwa na daktari mmoja tu wa zamu, kwa nini iwe hivyo, walinielezwa kuwa madaktari ni kidogo hapa na inapotokezea dharura kama hii inakuwa shida. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Afya kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, tuangalie hii hospitali mmoja ambayo ni muhimu sana kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Vile vile nizungumzie kwa haraka suala la wahudumu wa mama wajawazito na watoto nalo pia ni tatizo kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwa mfano, kwenye Kituo cha Afya cha Gamba hivi karibuni nimeshuhudia karibu mwezi mmoja na nusu huduma hizi hazipatikani na sababu kubwa ilikuwa kuna mtu aliambiwa jamani tuchangie huduma fulani hapa.

Kutokana na hali hiyo, nadhani ni vyema leo Mhe. Mwenyekiti atueleze Mhe. Waziri wa Afya hapa kama kweli au vipi, kwamba watu hawaruhusiwi kuchangia huduma za mama wajawazito, kwa hiyo zile huduma zikasitishwa kabisa kutokana na kwamba hapakuwa na vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tulisema kwamba hivi sasa ni wakati wa Mawaziri, lakini Mhe. Abdalla Juma Abdalla ameomba na tunampa dakika mbili.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya upendeleo maalum na mimi nataka nitumie dakika mbili tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza kamati kwa kufanyakazi nzuri sana ambayo ni ngumu, mambo waliyoyabaini ni ya kweli kabisa. Kwa hivyo, wenzangu wengi wamechangia Wizara ya Afya hasa kuhusu masuala ya *CT-Scan* na *ICU* na wala mimi sisemi kitu, isipokuwa nasisitiza tu kuwa hayo waliyosema wenzangu nayaunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niko kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambapo ninayo mambo matatu nataka niyazungumze tena kwa ufupi sana.

Kwa kweli mapungufu makubwa ya Wizara ya Elimu kuhusu ule Mfuko wa Elimu ya Juu, kwa sababu mfuko ule ni mdogo na wala hautoshi kuwasomesha wanafunzi walioko nje ya nchi na wizara ikimaliza nusu mwaka tu huwa inahangaika sana namna ya kuendesha wale wanafunzi.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, suala hili alitilie maanani sana, kwa sababu nyenginevyo tutakuwa tumepoteza fedha za watu bure. Kwa mfano, mtu anafika nusu ya safari yake anashindwa kwa sababu ya maslahi na hili ni jambo la kusikitisha sana.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu taasisi za serikali kama vile Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hasa skuli wameliweka nyuma sana kuhusu suala la kutafuta Hati Miliki ya maeneo yao ya skuli.

Kwa kweli hali hii imesababisha mambo mengi, kwa sababu ya kutokuwa na Hati Miliki wananchi wamejenga mpaka karibu zile skuli zenye, kiasi ambacho skuli kama inataka kujenga mabanda mengine zaidi inakuwa haina nafasi na mtu anadai ni shamba la mzee wangu. Kwa hivyo, suala hili naomba wizara ilitilie mkazo sana kwa zile skuli ambazo hazijakuwa na Hati Miliki, basi wajitahidi kutafuta Hati Miliki.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika Wizara ya Afya kuna baadhi ya Vituo vyetu vya Afya ambavyo havina Hati Miliki. Kwa hiyo, ni jambo la msingi sana kuharakisha, ili kuyalinda maeneo hayo.

Jambo jengine la mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna kilio kikubwa cha walimu, kwa sababu walimu ni kiwanda cha kutengenezea wataalamu maslahi yao ni madogo. Pamoja na maslahi hayo, kinachosikitisha Mhe. Mwenyekiti ni michango mingi kwa Wizara ya Elimu kwa mshahara ule wa walimu. *(Makofi)*

Kwa mfano, unamkuta mwalimu hicho kijimshahara chake kidogo anachopata, lakini kuna michango ambayo haipungui mitano au sita na ukijakuangalia huo

mshahara nusu nzima umeshakwenda kwenye michango na yeye haumtoshi hata kwa wiki moja.

Kwa hivyo, naiomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ilione suala hili na iwapunguzie sana walimu michango. Kwa mfano, kuna michango ya Mwenge, Tamasha la Elimu pamoja na mingine mbali mbali kiasi ambacho kila mwalimu hana furaha na hali hii inasikitisha sana. Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, suala hili alizingatie na nitaendelea kupiga kelele kila nitakapopata nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa ni zamu ya Mawaziri wale wanaohusika na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Lakini kabla ya kutoa nafasi hiyo napenda kumpa nafasi Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ili aweze kutoa maelezo machache ndani ya dakika mbili.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, napenda nikushukuru. Lakini kabla sijatoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo mawili matatu ambayo nilikuwa nikiguswa guswa na mimi naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza sana kamati inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Amina Iddi Mabrouk. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninayo maeneo mawili matatu tu ambayo nataka niyatolee maelezo kidogo, ili tutakapoondoka hapa Waheshimiwa Wajumbe wawe wamepata ufafanuzi kidogo.

Kwanza limezungumzwa kuhusu suala la posho la wazee, nataka niseme kwamba sisi sote tunaguswa hawa wazee ni wetu na wala hakuna anaowakataa. Kwa kweli suala hili lipo katika wizara yangu na tunalifanyiakazi. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wavute subira kidogo tunakamilisha taratibu na watatusikia tunaangalia posho la wazee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka niseme tu, mimi kama Mzanzibari ningelipenda zaidi kuona kwamba wazee tunawalea wenyewe katika nyumba zetu. Kwa kweli hawa ni wale wazee kwa sehemu kubwa hawana watu wa kuwahudumia, kwa maana hiyo ndio serikali ikawa inao. Lakini ni vizuri tena vizuri zaidi badala ya kukimbilia kutengeneza posho pamoja na Nyumba za Wazee, basi ni bora wazee hawa tukawalea ndani ya nyumba zetu kwa heshima za wazee wetu. *(Makofi)*

Vile vile suala jengine ambalo nataka nilitolee maelezo kidogo kuhusu *statements* za Waheshimiwa Wawakilishi kuhusu vifaa vya *ICU* na kujenga *ICU* kule Pemba na hasa nikatakiwa Waziri wa Fedha tutengeneze utaratibu wa kusaidia eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu nataka niwahakikishie kwamba lengo kubwa la Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba ambayo inaongozwa na Mfumo wa Umoja wa Kitaifa Sekta ya Afya kuipa kipaumbele. Kwa kweli sekta hii tumepanga kuipa kipaumbele katika maeneo muhimu kama vile upatikanaji wa vifaa na madawa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti wanaomba Waheshimiwa Wajumbe wavute busira, kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba ripoti hizi zinatusaidia sisi katika kuandaa bajeti. Kwa maana hiyo, nataka niwahakikishie kuwa hilo nalo tumeliona na tunalifanyiakazi.

Suala la mwisho ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi wameligusa ni kuhusu suala la maslahi kwa wataalamu. Kwa mfano, tukiangalia madaktari, walimu pamoja na wataalamu wengine. Kwa kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wawakilishi, ili wataalamu wetu wasitukimbie, basi nidhahiri kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuwatengenezea maslahi bora. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wavute subira wakati Waziri wa Utumishi anaandaa Bango Kitita lake. Kwa kweli Bango Kitita litaonesha kila mtaalamu na sifa yake pamoja na mshahara wake. Kwa hiyo, tumpe nafasi Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora amalize kuandaa Bango Kitita lake, halafu anipe mimi changamoto ya kutafuta fedha, ili aweze kugawa kwa mujibu wa Bango Kitita lake. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema kwamba elimu. Kwa kweli bila ya kuwa na elimu bora umasikini tulionao bado utaendelea kuwa chini, nidhahiri kwamba elimu ina umuhimu mkubwa sana katika taifa letu pamoja na dunia kwa ujumla. Kwa hivyo, tutaendelea kuimarisha Sekta ya Elimu na tutaendelea kuisaidia Sekta ya Elimu.

Vile vile bila ya kuwa na afya bora hatutaweza kujituma na kufanyakazi kwa faida ya nchi yetu pamoja na wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, kupungua kwa malaria tumeona isha moja nzuri, ambayo serikali yetu imeifanya na wananchi wetu hivi sasa wanajituma na wanapata muda mwingi wa kufanyakazi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, serikali tutahakikisha sekta hizi mbili pamoja na nyengine tutazipatia fedha za kutosha, ili ziweze kufanyakazi kwa uzuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mimi nianze kwa utamaduni wa kumpongeza Mwenyekiti na kwa sababu ni kikao chako cha kwanza tumekuona unaweza, kwa kweli waliokuchagua hawakufanya makosa. *(Makofi)*

Vile vile naomba nitoe shukurani zangu nyingi kwa Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii), kwa kazi nzuri aliyofanya pamoja na wenzake na kueleza kinaga ubaga udhaifu na matatizo tuliyonayo katika Sekta zetu hizi tatu za Afya, Elimu na Wanawake na Watoto. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sitochukua muda wa kujibu kila hoja maana waliochangia kwa mujibu wa *record* yangu ni wajumbe kumi na moja na kila mmoja ameeleza mambo mengi, lakini mengine yamejirudia.

Kwa kweli namshukuru Mhe. Mwenyekiti, alipompa nafasi Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa sababu yale aliyokuwa akiambiwa si mazuri, basi mwisho wakimwambia yeye kwamba mpe fedha babu Duni, yaani Mhe. Waziri wa Afya. Kwa hivyo, nahakika mara hii Mwenyezi Mungu akitujaalia mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Lakini kwa jumla masuala yaliyozungumzwa ya jumla ni suala la ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Afya, ambayo sina haja ya kuzungumzia zaidi na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameshalizungumzia. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano tu, jinsi hali inavyokuwa ngumu na pale tunapolaumiwa watu wajue.

Hospitali ya Mnazimmoja, ili uweze kuiendesha basi kila mwezi unahitaji shilingi milioni 50 iweze kwenda vizuri na hizo maana yake ni shilingi milioni 600 kwa mwaka. Kwa kweli huo ufinyu wa bajeti wenyewe basi zinazotengwa kwa mujibu wa hali ilivyo huwa hazifiki shilingi milioni 200 na kama zinafika basi hazizidi. Sasa pale unaposikia wanabinywa raia kwamba wachangie ni katika kujaribu kufanya mambo yasogee.

Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa suala la upungufu wa wafanyakazi. Sasa nadhani kifurushi cha Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa sababu wengi ya wale tunaowasomesha wengine wanaondoka si kwa sababu wanataka, lakini wanaona mambo yamewashinda wanakwenda kutafuta kwenye majani kijani. Kwa mfano, akiingia Dar-es-

Salaam *Nurse* hata yule aliyesomea Chuo chetu cha Mbweni analipwa shilingi 700,000/- mpaka 800,000/-.

Vile vile kuhusu suala la nusu kaputi tumewapeleka Moshi sita wamerudi wawili, wengine wamebaki Muhimbili kwa kufuata maslahi. Sasa mambo haya yanategemea na mtu mwenyewe, kuna kupenda kufanyakazi kwa sababu ni kwetu na pia maslahi ya maisha.

Kwa hivyo, vitu hivi vikivutana inategemea hali ya mtu. Mhe. Mwenyekiti, kifurushi cha Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambacho kinapigiwa kelele sana na katika ziara zote nilizotembelea kwenye kila kituo basi pamoja na mengine nitaambiwa hakuna dawa, vifaa lakini Mhe. Waziri maslahi, yaani hilo ndilo linalomaliziwa.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba hilo umelisikia na Waheshimiwa Wajumbe pia wamelieleza.

Pamoja na hayo kuna suala la uchafu limetajwa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe si vizuri kusema, lakini usafi ni tabia. Wakati mwengine hata mtu umpe kila kitu kama tabia yake mchafu basi ni mchafu. Lakini hata hivyo, mara nyengine huwa kuna upungufu wa vifaa.

Katika kujaribu kutekeleza matatizo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, yaani kujifunza, niliwaita viongozi wanaohusika nikawaambia kwamba hivi kwa mwezi ile hospitali iwe safi inahitaji milioni ngapi. Wakaniletea hesabu kwa jumla ni milioni kumi, kwa vifaa kama vile ditol, na mambo mengine yote. Tukafanya tulivyoweza tukawanunulia vifaa vya mwezi mzima tukasema hebu tuone. Bado malalamiko yapo lakini sio makubwa, zaidi malalamiko ya Mnazi Mmoja yalikuwa yamechanganyika na upungufu wa maji, lakini Mwenyezi Mungu amejaalia tumejitahidi tumetatua tatizo la maji.

Sasa mara nyengine inawezekana vile vile kwamba mtu hataki kujilazimisha kufanya kazi kwa sababu ya kwamba maslahi yake madogo, sasa vitu kama hivi vinahitaji usimamizi, lakini hata tukitaka kusimamia kama na zile haki za yule mfanyakazi hatumpi inakuwa huna sababu ya kumlazimisha anakwamba sawa lakini nipe haki zangu.

Waheshimiwa Wajumbe hesabu niliyoletewa mimi ya malipo ya madaktari kuitwa usiku nyumbani au kufanya kazi zaidi ni 28 millioni hazijalipwa hawa ni haki yao, kuna wafanyakazi wanakaa masaa 48 muda wote huo, sasa nilikwenda sehemu moja sijui kwa Mhe. Hija Hassan au wapi kule wakanambia Mhe. Babu sisi hatukatai kukaa masaa 48 lakini yale ya serikali yale tutakaa

yale yaliyokuwa ya ziada hatukatai lakini angalau tugaie japo nusu shilingi ili tukifika kule nyumbani tuache kile kihogo. Sasa anapokwambia hivyo huyu maana yake ni kwamba yuko tayari kufanya kazi lakini na wewe una wajibu vile vile, kwa hivyo katika wajibu kuna haki.

Kwa hivyo kubaki wafanyakazi na kuwaongeza wakawepo kutategemea vile vile ni haki na wajibu tutakaowatekelezea tunategemea tuvute subira kama tulivyoambiwa, hatutoweza kuwapa mbingu maana hatuna lakini angalau maji ya kunawa mikono inshaalla baada ya miezi mitatu au minne tutayajua. Suala kubwa ambalo nalo la *intrest* lililozungumzwa hapa ni masuala ya kuchangisha, sababu ya kuchangisha nimeieleza kwamba ni upungufu wa kipato ni kweli lazima nikubali kwamba imekuwa ikifanywa bila ya mpango maalum, lakini wizara yangu ilishaandika sera kamili ya mfumo mzima wa uchangiaji uweje, moja katika kutatua tatizo hili ni ile inayoitwa bima ya wafanyakazi inaweza kusaidia sana kupunguza suala la uchangiaji.

Kuna njia nyingi za kulitatua tatizo hili lakini suala la msingi ambalo limeshauriwa na wataalam wangu ni kwamba kama tunataka wananchi wachangie basi wakishachangia tena wapate huduma, kama anaambiwa lipa shilingi ishirini basi aipate huduma ya shiringi ishirini, hatari iliyokuwepo kwamba anatoa shilingi ishirini na huduma hapati, au anaambiwa atoe zaidi vichochoroni. Sasa hili tutakapomalizia utaratibu wake tutaliweka wazi na kila mwananchi atajua kipi anastahiki kuchangia, ukweli tunahimizwa hasa kinamama wao kuna zile *minimum* namba nne na tano ambazo zinasema mama mjamzito asichangishwe chochote hayo ni malengo ya dunia, na sisi kama ni sehemu ya dunia tulikuwa tunastahiki tuyafuate lakini hii yote itategemea utaratibu mzima abao tutaushughulikia wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, nisingependa nichukue muda zaidi suala la ICU amenisaidia Mhe. Omar kulieleza tulipopita katika ziara mimi na mwenzangu tuliliona na pale hapahitaji lile silinda, kwa kweli lile silinda pale kunajengwa *system* ile gesi inakuwa inatembea inakwenda mpaka kwenye kitanda cha mgonjwa, na kuna na ile *monitoring unit* ile inatakiwa kila kitanda iwepo ili ule moyo ukipiga kuwe kuna mtu anasoma pale kuona hali ya mgonjwa, lakini hali hiyo ilikuwa ni ngumu sana kuna mbili au tatu nyengine ni mbovu na kituo chenyewe eneo dogo. Lakini naomba nieleze kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja ina mpango wa muda mrefu wa kutengenezwa ili ipate hazi iliyotakiwa na serikali ya kwamba iwe ya rufaa, hivi sasa kuna wafadhili wadachi ufadhili usiopungua dola milioni saba, ambao utatengeneza yale majengo yaliyokuwa kiwanda cha madawa kule yatatengenezwa yaonekane ni majengo ya hospitali na lile zogo na ghasia nyingi zilizopo hapa Mnazi Mmoja hasa ile sehemu ya *out pation* itaondoshwa na itapelekwa kule ili hii hapa ipatikane nafasi ya kuweka mambo vizuri na ijulikane kwamba ni hospitali ya rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Mbweni sina haja ya kulieleza pale ilikuwa inashikiliwa tu kwamba yule jamaa tumtunze na tumemtuna na sasa ndio daktari mkuu wa pale Mbweni, na ndio Mwalim Mkuu wa kile Chuo.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi kweli ni wachache hasa manasi hivi sasa tunamalizana na wakubwa kule Mhe. Haji na Mhe. Omar nadhani kesho tutamfikirishia wale vijana wote waliokuwa wamemaliza Mbweni labda baada ya wiki moja au mbili wataajiriwa, lakini tumeamua kwamba katika hao wanaoajiriwa nisikilizeni vizuri, hao watakaoajiriwa sitini wanakwenda Pemba. Hiyo yote ni kutia umuhimu wa hali ilivyo kule Pemba lakini ndugu zangu naomba mambo mawili kuna wale vinana wanaotoka Pemba tunahakikisha tunawapeleka Pemba *(Makofi)* Sasa wakubwa sio nyie, lakini wakubwa wana tabia za kuwaoa itabidi sasa mume amfuate mke Pemba. *(Makofi)* Halafu pamoja na hayo kutakuwa na wengine ambao watakuwa ni vijana kutoka Unguja na wao tutawapeleka Pemba, lakini tunaomba msaada wenu moja katika tatizo watakalolipata ni ukosefu wa makazi.

Mhe. Muwakilishi na Mbunge unanambia kituo chako hakina mtendaji nakuletea mtendaji umpe nyumba wala usimlipishe, umwachie vile visenti vyake kidogo ambavyo havijaongezwa angalau apate ugali na nyengine amwachie mzee wake Zanzibar, tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia Wizara ya Afya na tumesaidia vituo vilivyokuwa havina watu kama mtatizama hapa Mhe. Naibu wangu hayupo hapa anakamilisha kazi hiyo kuhakikisha kwamba utaratibu huo tuliokubaliana na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba tunaumaliza katika siku tatu nne zijazo katika kukabili upungufu huo.

Waheshimiwa yale mengine yaliyobakia tunawashukuru kwa michango yenu na ushuri wenu na tumeuchukua, tunaufanyia kazi na ripoti hii nimeshaisoma na wakubwa wangu wanaonisaidia au wataalam nategemea wakati wa bajeti tutakuja na maelezo mazuri zaidi nawashukuru sana. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nakupongeza wewe kwa kukalia hicho kiti kwa mara ya kwanza, halafu namshukuru Mwenyekiti wa kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na kamati yake kwa jumla kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata mengi mie katika mijada iliyokuwepo hapa kwenye ripoti ya kamati hii, nikiri mbele yako kwamba itanisaidia sana katika kufanya elimu kuwa bora zaidi hapa Unguja na Pemba, kwa hivyo mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti haya hayataki majibu yanataka kutekelezwa kwa hivyo nadhani ni vizuri kuyachukua kwa ajili ya kuyatekeleza kuliko kuyatafutia majibu hapa wakati kazi ipo pale pale, lakini kuna mambo matatu

mpaka manne haya nataka niyaeleze kidogo kwa sababu ni yetu pamoja mimi pamoja na sisi tuliokuwemo humu kwenye Baraza la Wawakilishi.

Kwanza suala la hatimiliki katika maskuli yetu. Mhe. Mwenyekiti huko katika maskuli yetu sisi huwa tunawahamasisha watu kuanzisha maskuli na maeneo ya kujengie hiyo skuli huwa tunatafuta sisi waheshimiwa wawakilishi, tukishapata yale maeneo tunaanzisha kujenga skuli Wizara ya Elimu inakuja kutia mkono wake pale skuli tayari inaanza. Kwa hivyo nataka tuengeze kidogo jitihada yetu katika hili kwamba tukishapata pale pahala tukianza kujenga skuli basi waheshimiwa wawakilishi na wabunge wajitahidi kusaidia kupatikana suala la hatimiliki pela mahala kwa sababu skuli ni nyingi na lazima tuhakikishe kwamba sisi Waheshimiwa tunahakikisha katika kutafuta hatimiliki katika suala lile inapatikana Skuli zetu za zamani zote zina hati miliki tumerithi kwa wakoloni na ramani zipo.

Mhe. Mwenyekiti, wala muwakilishi asije akadanganyika akakuta watu wana *site plan* akafikiri ndio hatimiliki tofauti *site plan* na hatimiliki ni mambo mawili tofauti kabisa, sisi kwenye Baraza la Mapinduzi tumeshaamua kabisa kwamba suala hili tulifanyie kazi lakini naomba msaada wa waheshimiwa wawakilishi na wabunge wenye maskuli yaliyopo katika maeneo yetu.

Pili kuna suala la kamati ya wazee, kamati ya wazee imewekwa pale kwa ajili ya kusaidia na walimu na kusema kweli kamati ya wazee ni mabalozi kwa ajili ya wazee wenzao waliomo kwenye maeneo ili kuondoa ile kutokufahamiana baina ya walimu na wazee walioko kwenye yale maeneo ambayo ndio walioletwa wale watoto kusoma. Kwa hivyo ile kamati ya wezee inatakiwa iwe inasaidia kule, sasa kamati za wazee hazitakiwi kufanya kazi pale skuli inatakiwa kufanya kazi kwa upande wa wazee huko, sasa kama wamekubaliana kuna suala la michango basi wazee wawashawishi wazee wenzao huko katika suala la michango, sio kwenda kuwaambia wanafunzi wasije skuli kwa sababu hawajatoa mchango, hilo sio halali kabisa kumzuia mwanafunzi ukasema asiende skuli kwa sababu hajatoa mchango tunaikanusha sana kwenye Wizara ya Elimu hiyo, na atunawataka walimu wetu wasifanye hata mara moja kumrejesha mtoto kwa sababu hajatoa mchango hilo nimeona nilizungumze.

Lakini la tatu suala la masomo. Haya masomo yetu haya *performance* ikawa inakuwa mbaya ni suala ambalo kusema kweli pamoja na matatizo yote tuliyokuwa nayo lakini nafikiri mashirikiano ya wazee na vijana waliosoma katika yale maeneo wakawasaidia wale vijana wao wanaendelea kusoma ili linafanyika katika maeneo mengi sasa hivi hapa Unguja. Ndio maana *performance* mwaka huu ya Unguja ya mtihani wa *Form IV* ni 82 *percent*, *percormance* ya Pemba ni 55 *percent* ni kwa sababu hawasaidii vijana. Badala

yake wanaiachia Wizara peke yake ishughulikie masuala hayo, safari hii matokeo yamekuwa mabaya sababu moja ni hiyo.

Lakini la pili ni lile alilosema Mhe. Waziri wa Afya hapa kufanya kazi Pemba hili tatizo tunalo unaweza kupata walimu wazuri wanawake ukawapeleka Pemba wakafanye kazi wanaolewa wote, si vibaya kuolewa lakini moja katika sababu ya kuhama kutoka Pemba kuha hapa Unguja sasa na walimu hapa ni wengi wameshapita kile kiwango kinachohitajika, lakini Pemba kuna tatizo la walimu na unapeleka baada ya kumaliza unawapeleka katika skuli mbali mbali baada ya muda kama alivyosema mwenzangu tunaombana ebwana wewe nisaidie aje zake Unguja, sasa haya ndio matatizo tunayowkenda nayo kwa hivyo tusaidiane katika hili maana ni letu pamoja nimelisema kwa sababu ni letu pamoja ili niweze kuendelea kabisa.

Halafu mimi nampa pole sana Mhe. Mwekilishi wa Chambani katika suala zima la walimu kuwa hawashiriki katika misiba ya walimu wenzao kule Pemba, sio vizuri kusema kweli amelisema kwa uchungu na mimi nampa pole sana ni vizuri walimu unapofanya kazi nao inapotokezewa na msiba tushiriki kwenye misiba.

Mhe. Mwenyekiti, muda umekwisha sitaki kuzungumza mengi pamoja yote nimeletewa mambo mengi tu hapa ninayoweza kuyajibu lakini naona wakati hautoshi, kwa hivyo ishaalla tutakutana kwenye bajeti nitajua tumetengeneza nini na nini limetushinda. Ahsane sana.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba Baraza lako tukufu liridhie kuweka kanuni kando ili Waheshimiwa Mawaziri waweze kumaliza hoja zao katika shughuli iliyopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wanaounga mkono hoja wanyanyue mkono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kufikiwa)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watoto: Mhe. Mwenyekiti pamoja na wajumbe kwanza na mimi nipate nafasi ya kukupongeza kwa kukalia kiti kwa mara ya kwanza na imekuwa kama umekikalia mara kumi, kwa sababu wajumbe wamechoka sana nitafafanua baadhi ya mambo makubwa yaliyojitokeza.

Kwanza niwapongeze na niwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Maendeleo ya Wanawake na Watoto, chini ya Mwenyekiti wao Amina Iddi Mabrouk, nikitaka nianze na mchango wa wajumbe kwanza nataka nianze na Waziri wa fedha ingawa amenisaidia lakini taka kuzunguzia suala zima la wazee wa nyumba za Sebleni, nyumba ya Welezo.

Mhe. Mwenyekiti sisi hapa sote tumezaliwa tuna wazee wetu hakuna hata mmoja aliyeshuka kwa kamba, tunapaswa tufanye jitihada kubwa ya kuwalee wazee wetu vyenginevyo kesho mbele ya Mungu *finnari jahanama*, serikali nayo pia imechukua jitihada za kuwaenzi wazee tokea mwaka 1964 wazee wanalelewa pale Sebleni hadi leo ni kweli nakubaliana na wajumbe waliochangia kwamba posho ni ndogo, lakini Mhe. Waziri wa fedha amejibu pale kwamba mambo haya yako juu ya meza yaaandaliwa vizuri wazee watang'ara sana katika awamu hii ya saba ya serikali ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti nyumba ya wazee imefanyiwa ukarabati kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin tumelijenga paa la kisasa kabisa linapendeza, tumeweka dari sasa hivi tuko katika hatua ya kuweka milango na madirisha ile nyumba iliyoungua moto baadae tutamalizia kwa kurudisha umeme kwa sababu nyumba iliungua, kupaka rangi, palasta kila kitu tayari hakuna matatizo.

Lakini pia kama alivyoeleza Mhe. Salmin Awadh Salmin ni kwamba tumefanya bajeti ya shilingi milioni 640 kwa ajili ya kuzihifadhi zile nyumba ili watu wasipate nafasi ya kupita pita ovyo na kuwaibia.

Jengine ninalotaka kulizungumzia ni suala la watoto walemavu nimeshauriwa kwamba kuna haja ya kwenda ndani zaidi kuwaona watoto walemavu kwa sababu kuna waze wengi wanawaficha watoto wao, wanaotangaza jamani nisaidieni tunawalaumu kwa nini ukatangaza hivi na vile unalaumiwa, kwa hivyo tutakwenda ndani zaidi ili kuwaangalia watoto walemavu na kuona serikali itashauri vipi ili wasaidiwe na wao wasiwe nyuma.

Lakini suala kubwa nalo ambalo linahusiana sana na Wizara hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana wanawake na watoto ni kuhusu suala zima la vikundi vya ushirika, nilikuwa naambiwa kwamba tuviangalie kwanza tunatoa pongezi kwa sababu vile vikundi vyote tumeshaviorodhesha na tuviangalie na tuvipe nguvu utaalam, hilo nalo tutajitahidi hivi sasa ratiba yetu iko juu ya meza tunataka tupite tukizungumza nawanawake kuhusu suala zima la vikundi vya ushirika, yale mambo ya kusubiri bwana haji huna hata sabuni inakuwa sio jambo zuri.

Lakini kuna hili suala la kwamba tumepitisha mswada huu hivi karibuni au juzi na mimi nawashukuru sana kwa sababu nilikuwa nikisema utapita huu, lakini kwa bahati nzuri mmeukubali nashukuru, lakini pamoja na hayo suala la huduma za mama na watoto hospitali kuwa liondoke hili mimi namuachia Mhe. Waziri wa Afya maana yeye ndie anayetoa hizo huduma zenyewe na kusema kwamba nitakwenda kuwalipia mie inakuwa ngumu kidogo.

Lakini pia sisi tuna tatizo kubwa la jengo la Wizara lakini Serikali yetu ina makati sasa hivi wa kujenga Wizara mbali mbali za serikali mpya, kwa hivyo naamini waziri wa Fedha hii Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Maendeleo ya Wanawake na Watoto ataipa umuhimu wa kwanza. Wajumbe wengi wametuombea kwamba wizara yetu ipewe bajeti kubwa ni kweli kwa sababu tunashughulikia na jamii nzima tukianzia na wazee, tunakuja na vijana, tunakuja na wanawake na watoto juu. Yaani ustawi mzima wa jamii tunao sisi pale sasa tukiwa na bajeti ndogo mtatulaumu kwa hivyo mimi nashukuru kwa hayo na nashukuru sana na nategemea kwa mwaka huu bajeti ya kwanza itakayokuwa kubwa ni yetu. *(Makofi)*

Mwisho nataka niwaambie ndugu zangu mimi naomba sana tushirikiane katika kufanya kazi zetu lakini zaidi naomba mashirikiano yenu kupitia kwenye Wizara yetu kupitia kwa kamati hii, sasa hivi tuna ule msaada wa Norway nilikuwa nawaambia wawakilishi hapa kwamba wao wamechaguliwa na watu na mna hakika vijana walikuwa mstari wambele, wawatayarishe vijana ili utakapofika wakati wa uchaguzi kwa sababu huu msaada ni endelevu basi kila mmoja asije akalaumu hapa kwamba mimi sikupata, na sisi wizara tuko tayari kusaidia juu ya jambo hili ili kila kijana aondokane na hali ngumu ya uchumi haya madawa ya kulevya, hayo mambo ya ubakaji hayo yanachangia pamoja na umasikini.

Ahsane Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia tena kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, nachukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia ripoti yetu hii na waliokuwa hawakupata nafasi watakuja kuchangia siku zijazo.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti yetu imepata nafasi ya kuchangiwa na Waheshimiwa wajumbe kumi kama ifutavyo:

i) Mhe. Salmin Awadha Salmin
ii) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
iii) Mhe. Ismail Jusa Ladhu

iv) Mhe. Hija Hassan Hija
v) Mhe. Omar Ali Shehe
vi) Mhe. Salum Abdalla Hamad
vii) Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
viii) Mhe. Mussa Ali Hassan
ix) Mhe. Ussi Jecha Simai
x) Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Mwenyekiti, masuala yaliyoulizwa na waheshimiwa wajumbe waheshimiwa Mawaziri husika wameyatolea ufafanuzi vizuri sana, imani yangu waheshimiwa wajumbe wameridhika sana na majibu yaliyotolewa. Basi nichukue nafasi hii kuwapongeza waheshimiwa Mawaziri wote kwa majibu na ufafanuzi walioutoa kwa waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wanaokubaliana na hoja wanyoonge mkono juu, wasiokubali. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima napenda kutoa shukurani zangu za dhati, kwa namna tulivyoshirikiana tokea mwanzo wa shughuli hii kwa jioni ya leo hadi tumeweza kufikia hapa. Hii ni mara yangu ya mwanzo katika historia ya maisha yangu kuweza kufikia pahala kama hapa na kuweza kukaa katika kiti kama hichi kikubwa, lakini *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutajifunza na tutaweza zaidi.

Baada ya maelezo hayo naomba kuchukua nafasi hii kukushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa pamoja nami kwa shughuli yote ambayo imepatikana leo hapa, pamoja na kuonyesha imani yenu na kuniamini kwa kunipa ridhaa ya kuweza kukaa kwenye kiti hiki. Baada ya maelekezo hayo sasa, kwa heshima na taazima naomba kuchukua fursa hii kuliahirisha Baraza hili mpaka tarehe 01/04/2011 saa 3: 00 za asubuhi.

(Saa 1.52 Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 01/04/2011 Saa 3.00 Asubuhi)